**Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA MBILI

**Kikao cha Pili – Tarehe 11 Juni, 2008**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

## MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama kawaida yetu, tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu na atakayeuliza swali la kwanza leo ni Mheshimiwa Bakar Shamis Faki.

Na. 11

### Bunge Kuahirishwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu

**MHE. ABUBAKAR KHAMIS BAKARY (K.n.y. MHE. BAKAR SHAMIS FAKI)** aliuliza:-

Kwa kuwa Bunge ni moja kati ya mihimili mitatu ya Dola ambalo lina bajeti yake ya kujitegemea; na kwa kuwa Mheshimiwa Spika ndiye Kiongozi wa mhimili huo:-

Je, kwa nini Hoja ya Kuahirisha Bunge inatolewa na Waziri Mkuu ambaye ni sehemu ya mihimili mingine badala ya Mheshimiwa Spika ambaye ndiye Kiongozi wa mhimili wa Bunge?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. PHILIP S. MARMO)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba nimjibu Mheshimiwa Bakar Shamis Faki, Mbunge wa Ole, swali lake kama ifuatavyo:-

Ni kweli Bunge ni moja ya mihimili mitatu ya Dola na hili limetamkwa katika Katiba yetu, mihimili mingine ni Serikali na Mahakama. Waziri Mkuu, akishathibitishwa na Bunge kushika madaraka yake Kikatiba, ndiye Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni na anatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Katiba, Sheria za Nchi na Kanuni za Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafasi ya kutoa Hoja ya Kuahirisha Bunge, baada ya Shughuli za Bunge zilizopangwa kufanyiwa kazi na Mkutano wa Bunge kumalizika ni kuzingatia matakwa ya Katiba. Ibara ya 52 na pia Sheria Na. 15 ya mwaka 1984, Ibara ya 9; kuahirishwa Bunge ni suala la Kikanuni na linaingizwa kwenye Orodha ya Shughuli za Kikao cha mwisho, kumpa fursa Mheshimiwa Spika, kumwita Waziri Mkuu kwa utamaduni tuliojiwekea, kutoa Hoja ya Kuliahirisha Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatimaye Mheshimiwa Spika, atalihoji Bunge ili kuafiki Hoja ya Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni. Hatua inayofuata hatimaye ni Mheshimiwa Spika analiahirisha Bunge.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, naomba niulize swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu ni Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni lakini sio Kiongozi wa mhimili ambaye anaongoza utaratibu wote, shughuli za Serikali zinakamilika baada ya Miswada yote kumalizika. Je, suala la Kuahirisha Bunge lina uhusiano gani na shughuli sio kazi ya Mhimili Mkuu huyo Kuahirisha shughuli za chombo chake?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. PHILLIP S. MARMO):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa wasomi waliobobea katika maeneo ya Kanuni za Bunge na wanafalsa wa Kanuni za Bunge, mwenye Mamlaka ya mwisho hatimaye katika kuamua mambo wala sio Kiongozi wa Serikali Bungeni na wala sio Mheshimiwa Spika ila ni Bunge hili.

Ndiyo maana hatimaye Wabunge wanahojiwa na kuamua hoja hiyo. Iwapo watakataa hoja hiyo kwamba, Bunge liahirishwe mpaka tarehe fulani na mahali fulani, wana uwezo huo na kupendekeza tarehe au mahali pengine wanapoona inafaa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mara ngapi Spika amewaambia wanaotaka kuendelea kukaa Dodoma waendelee? *(Makofi/Kicheko)*

Na. 12

**Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu – *CDA***

**MHE. EPHRAIM N. MADEJE** aliuliza:-

Kwa kuwa Ofisi ya *CDA* hivi karibuni ilitoa tangazo tarehe 29 Januari, 2008 kwamba, Mamlaka hiyo ilimilikishwa ardhi yote ya Manispaa ya Dodoma tangu mwaka 1987 na kwamba, ina uwezo wa kupanga matumizi na kutwaa ardhi hiyo bila masharti au fidia yoyote:-

(a) Je, ni kweli Serikali iliimilikisha *CDA* ardhi yote ya Manispaa ya Dodoma kama tangazo lilivyosema?

(b) Je, Serikali inayo habari kwamba, baadhi ya wakazi wa maeneo ya Tambukareli, Dodoma Makulu, Medeli, Kisasa, Chadulu, Ipagala, Swaswa, Mlimwa, Chinangali, Mbwanga na mengineyo hivi sasa ardhi yao inatwaliwa na *CDA* bila fidia?

(c) Je, Serikali inachukua hatua gani kuhakikisha kwamba, wananchi hao hawanyanyaswi na wanapewa fidia kutokana na maeneo waliyokuwa wanayamiliki kimila?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. PHILIP S. MARMO)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Ephraim Nehemia Madeje, Mbunge wa Dodoma Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c), napenda nitoe maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu *(CDA)*, iliundwa chini ya Sheria ya Mashirika ya Umma Na. 17 ya Mwaka 1969, kupitia Tangazo la Serikali Na. 230 la Mwaka 1973 na hatimaye kuchapishwa kwenye Gazeti la Serikali la tarehe 12 Oktoba, 1973.

Majukumu ya kuanzisha *CDA* ni pamoja na kutekeleza uamuzi wa Serikali wa kuhamisha Makao Makuu ya Serikali kwenda Dodoma; kuandaa na kutekeleza Mipango ya Maendeleo ya Dodoma kama Makao Makuu, ikiwa ni pamoja na Mpango Kabambe; na kumiliki ardhi na mali nyingine zisizoweza kuhamishika kutokana na Agizo la Rais.

Ili kusimamia vyema utekelezaji wa majukumu yake, Serikali iliimilikisha ardhi *(CDA)* ya eneo lote lililotengwa kwa ajili ya Ustawishaji Makao Makuu, mnamo Aprili, 1987 kwa kuipatia Hati ya Muda mrefu ya miaka 99, yenye Namba 4585 *DLR*, ambayo imehifadhiwa katika *Dodoma Land Rent Registry*. Dhumuni kubwa la kufanya hivyo ni kuiwezesha *CDA*, kusimamia vyema na kuleta tija na ufanisi katika utekelezaji wa Mpango Kabambe, ujenzi na uendelezaji wa mji kwa ujumla katika eneo lote la Mji Mkuu; upimaji na ugawaji wa ardhi; kutoa hati miliki za viwanja na kusimamia ujenzi; na uendelezaji mji kwa ujumla katika eneo lote la Mji Mkuu wa Dodoma. Hati hii inajumuisha eneo lote la Makao Makuu (*Capital City District),* ambalo pia ndiyo eneo zima la Manispaa ya Dodoma au Wilaya ya kiutawala ya Dodoma ya sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua wewe uko makini kwa muda, lakini kwa ajili ya umuhimu wa suala hili, naomba sasa nimjibu kwa kifupi Mheshimiwa Madeje, Mbunge wa Dodoma, swali lake kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli Serikali iliimilikisha *CDA* ardhi yote iliyotengwa kwa uendelezaji wa Mji Mkuu, ambalo ndiyo pia eneo la Manispaa ya Dodoma na eneo la Kiutawala la eneo la Dodoma.

(b) Maeneo ya Tambukareli, Dodoma Makulu, Medeli, Kisasa, Chadulu, Ipagala, Swaswa, Mlimwa, Chinangali, Mbwanga na mengineyo, yaliyo katika awamu ya kwanza ya uendelezaji wa mji, yalitwaliwa (*Acquired*) na Serikali na kulipwa fidia miaka ya 1970 na 1980. Kwa mfano, Mheshimiwa Madeje, atakuwa anakumbuka kulikuwa na mikikimikiki mingi sana ya kuhamisha wakazi wa Tambukareli, kazi ambayo ilifanyika miaka ya 1970; kuwahamisha watu hao kwenda kwenye eneo la Chinangali na baadaye walilipwa fidia. Wananchi waliendelea kukaa katika maeneo yaliyoorodheshwa hapo juu, kwa huruma tu ya Serikali kuwaacha waendelee kuyatumia maeneo hayo, kwa kulima mazao ya msimu ili mara maeneo hayo yatakapotakiwa kuendelezwa kwa matumizi yaliyokusudiwa, basi wananchi hao watatakiwa kusitisha shughuli zao na kuyaachia maeneo hayo bila madai kwa mara ya pili. Hata hivyo, katika maeneo mapya ya upanuzi wa mji na ambayo hayakuwa kwenye awamu ya kwanza, kama vile vijiji vilivyosajiliwa, ambayo yalikuwa yanaangukia kwenye Mamlaka ya Sheria ya Vijiji, maeneo hayo iwapo yatatakiwa kutwaliwa, itabidi fidia ilipwe.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, Serikali ilipoanza mchakato wa uendelezaji wa Mji Mkuu Dodoma, ilizingatia taratibu zote za kisheria kwa kutoa matangazo ya Serikali Na. 63 la mwaka 1978, Na. 99 la 1978, Na. 142 la 1979 na Na. 8 la 1980. Matangazo haya yalitangaza eneo jipya la Mpango Mji, kufuta utaratibu uliokuwepo, ikiwa ni pamoja na umilikaji wa maeneo hayo kimila na hivyo kutangaza utaratibu mpya wa umilikaji. Hivyo ni vyema ikatambulika kuwa, miliki za kimila katika maeneo ya mji yaliyotwaliwa kwa sasa ni batili, kwa sababu maeneo yote yaliyotwaliwa kwa uendelezaji wa mji, yalilipwa fidia chini ya sheria zilizokuwa zinatumika wakati huo. Hivyo, kuwaondoa watu wote wanaovamia maeneo kinyume cha taratibu si unyanyasaji bali ni kusimamia uendelezaji mji kwa kuzingatia taratibu na sheria. Tunawasihi viongozi wa ngazi zote katika Manispaa ya Dodoma, kuwaelimisha wananchi kuelewa taratibu na sheria za uendelezaji Mji Mkuu Dodoma ili kuepusha usumbufu na malalamiko yasiyo ya lazima.

**MHE. EPHRAIM N. MADEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri, kwa majibu yake. Hata hivyo, ninaomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Kutokana na maelezo yake Mheshimiwa Waziri na pia kutokana na hali halisi ilivyo, masuala ya fidia ya ardhi ya hapa Dodoma yanatawaliwa na Sheria Ndogo ambayo iliunda Mamlaka ya Uendelezaji wa Makao Makuu kupitia *Government Notice.*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu ni hili, je, kutokana na hili Serikali haioni kwamba Wananchi wa Dodoma wananyimwa haki zao za kimsingi na ambazo zipo katika Katiba kutokana na utaratibu huu ambao unawafanya wasitumie utaratibu wa Sheria za Ardhi kama wenzao wengine katika nchi hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, ibara ya 125(a) ya Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005, imeahidi kwamba, Sheria itatungwa ya kuitambua rasmi Dodoma kama Makao Makuu ya Serikali. Wananchi wa Dodoma wanaamini kabisa kwamba, Sheria hii ikitungwa itasaidia sana katika kuondoa utata ulio mwingi hasa katika masuala ya ardhi, lakini pia

katika kuwarudishia haki zao wananchi. Swali, je, Serikali itakamilisha lini mchakato wa kuitunga sheria hii?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. PHILIP S. MARMO):** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na swali la pili. Nakubaliana naye kwamba, wakati umefika sasa kutunga sheria mpya kwa ajili ya uendelezaji wa Makao Makuu Dodoma, kwa vile tangu mwaka wa 1973 mabadiliko mengi yametokea, ikiwa ni pamoja na kurejeshwa kwa Serikali za Mitaa. Mchakato huo unaendelea, tunaomba Mheshimiwa Madeje na Wabunge wengine, wavute subira.

Kuhusu swali lake la kwanza kwamba, pengine uendeshaji wa matumizi ya ardhi unavyotumika hapa Dodoma ni tofauti na maeneo mengine, kwa kweli tofauti sio kubwa sana. Ni kwamba, kwa maeneo mengine, ardhi inafuata masharti ya Sheria ya Ardhi, ambayo yapo chini ya Mamlaka ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi. Kwa Dodoma, mamlaka hayo yapo chini ya Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu Dodoma. Kimsingi, sheria za nchi zinafuatwa isipokuwa tu kwa Dodoma tuna vipaumbele maalum ili tuwe na mpangilio mzuri. Kuwe na mji wa kisasa unaovutia.

Tatizo letu kubwa hapa ni kwamba, *CDA* kwa muda kidogo haikuwa na fedha za kutosha na sasa hivi tatizo hili tunalitatua, lakini pia hatukuwa na rasilimali watu. Hivi karibuni mabadiliko yataonekana, itaanza kupima viwanja na kuwagawia wananchi; si chini ya viwanja 5,000 hadi mwishoni mwa mwaka huu, kwa hiyo, naamini tatizo hili litapungua.

**MHE. JOHN S. MALECELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza baada ya majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuiuliza Serikali; hivi suala hili la kuhamisha watu katika miji kwa nini linazuka utafikiri tumbo la kipindupindu; leo utasikia watu wamehamishwa Tabata, kesho utasikia watu wamehamishwa Chinyoya, keshokutwa utasikia watu wamehamishwa mahali pengine; ni kweli tunataka miji yetu iwe ni miji ambayo imepangwa vizuri, lakini kwa nini hatuwi na mpango endelevu; watu wakajua kwamba mahali fulani baada ya miaka fulani hawatatakiwa wawe pale na fidia zikalipwa na watu wakaondoka; lakini siku hizi ni kuvunja kwanza, mara nyingine kupigana na wananchi naambiwa halafu suala la fidia linakuja baadaye?

Ningependa kujua kwa nini Serikali haitengenezi mpango endelevu na ikaijulisha miji yetu yote, suala hili la bomoabomoa likaondoka ambalo linatuletea madhara kwanza ya kisiasa na pili linawafanya wananchi wetu wawe kama ni Wakimbizi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. PHILIP S. MARMO):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla tatizo la miji yetu ni kubwa zaidi ya tunavyoliona, hasa kwa vile hatuna fedha za kutosha za kupanga na kuandaa viwanja,

pamoja na miundombinu inayohitajika ili wananchi wawe wamehamia na kujenga katika maeneo ambayo ni ya kudumu. Tatizo ni fedha kwanza.

Lakini pia kama nilivyosema, kwa upande huu wa Dodoma ni rasilimali watu. Ni kweli kwa mfano, hapa Dodoma, kumekuwa na bomoabomoa katika maeneo ya Chang'ombe na Chinangali na tulifanya hivyo kwa sababu tuliona kwamba ni muhimu sana kwa wakati huu, kufanya hivyo. Hii imetokana na uharibifu unaoendelea kuwa mkubwa, misitu kuvamiwa na tena wanaofanya hivyo ni watu ambao wana nia ya kuhodhi ardhi na baadaye kuiuza, lakini baya zaidi ardhi hii miliki ya hatimiliki ni ya *CDA.*

Kwa hili la Dodoma, tupo pamoja na Serikali ya Mkoa na Wilaya na muda wote wamelifuatilia suala hili kwa karibu sana, isipokuwa maoni ya Serikali ya Wilaya na Mkoa wa Dodoma kwa bomoabomoa iliyokuwa inaendelea hivi karibuni kama ifuatavyo kwamba; viongozi wa ngazi za chini yaani Madiwani na viongozi wa Mitaa huwa na kauli zinazobadilika badilika, wakiwa na wananchi wanasema tofauti na wanapokuwa na viongozi wa ngazi za juu pia wanaeleza tofauti. Kwa kifupi, viongozi hao hawapo tayari kukemea, kukataza au kuzuia wananchi wasivunje sheria za ujenzi katika Mji wa Dodoma; matokeo yake *CDA* inaonekana kuelea kwa kuwa haina uwakilishi. Kwa hiyo, tunaomba sana ushirikiano wa viongozi wa ngazi zote.

**NAIBU SPIKA:** Wote mtakubaliana na mimi kuwa, swali hili limechukua dakika 15 kwa hiyo tunaendelea na swali linalofuata.

Na. 13

**Kuwapatia Maji Wananchi wa Kigoma-Ujiji**

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA (K.n.y. MHE. PETER J. SERUKAMBA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, maji ni muhimu kwa maisha ya binadamu; je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia maji Wananchi wa Kigoma-Ujiji hasa ikizingatiwa kuwa, maji yapo karibu sana na mji huo na kwa miaka mingi hawana huduma ya uhakika ya maji tangu tupate uhuru?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba, Mbunge wa Kigoma Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuboresha huduma ya maji katika Mji wa Kigoma-Ujiji, Serikali ina mipango ya muda mfupi na muda mrefu. Katika mpango wa muda mfupi, Serikali itafanya kazi za ukarabati au ujenzi wa miundombinu ya maji, ambazo

zitaleta matokeo ya haraka. Kwa Mji wa Kigoma-Ujiji, kazi hizo ni ukarabati wa mitambo ya kusukuma maji, mabomba ya kusambaza maji na ufungaji wa dira za maji 2,500. Mwezi Aprili, 2008 Mamlaka ya Majisafi na Majitaka ya Kigoma-Ujiji, ilifanya tathmini ya zabuni za Wahandisi Washauri ili kumpata atakayefanya usanifu wa kina kwa ajili ya kazi hizo. Tathmini ya zabuni hizo, imewasilishwa Benki ya Dunia mwanzoni mwa mwezi Juni, 2008 ili kupata ridhaa (*no objection*) ya Benki hiyo. Baada ya kupata ridhaa ya Benki ya Dunia, Mamlaka itasaini mkataba na Mhandisi Mshauri na usanifu unatarajiwa kuchukua miezi minne. Mchakato wa kutangaza zabuni hiyo hadi kumpata mkandarasi, unatarajiwa kuchukua miezi mitatu na ukarabati unatarajiwa kuchukua miezi 12.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 13 Machi, 2008 nilitembelea na kukagua hali ya miundombinu ya maji katika Mji wa Kigoma-Ujiji. Nilibaini kuwa, kazi ya kutoa huduma ya maji katika mji huo, imegubikwa na matatizo ya uchakavu na uwezo wa miundombinu iliyopo. Aidha, ukosefu wa umeme wa uhakika katika Mji wa Kigoma-Ujiji, unasababisha maji kupatikana kwa mgao. Serikali inaendelea kutafuta ufumbuzi wa matatizo haya ya maji. Kwa mfano, mwezi Februari, 2008 Wizara yangu iliipelekea Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Kigoma-Ujiji, shilingi milioni 69.9 kwa ajili ya ununuzi wa pampu moja na vifaa vyake na mabomba ya kutoa maji ziwani. Aidha, tayari Mamlaka imenunua tanki lenye ujazo wa mita 227 na mabomba yenye ukubwa tofauti. Hivi sasa Mamlaka inaendelea na taratibu za ununuzi wa pampu na vifaa vyake, kwa ajili ya kufunga kituo cha kusukuma maji kwenye chanzo cha Bangwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, upo Mpango wa muda mrefu wa kuwapatia maji Wananchi wa Kigoma-Ujiji, ambao ni sehemu ya mradi kabambe wa uboreshaji wa miundombinu ya majisafi na majitaka katika miji saba ya Babati, Bukoba, Kigoma yenyewe, Lindi, Mtwara, Musoma na Sumbawanga. Mradi huo unafadhiliwa na Mfuko wa Maji wa Jumuiya ya Ulaya *(ACP-EU Water Facility*). Mchakato wa kupata Wataalam Washauri wa kufanya uchunguzi na usanifu unaendelea na kazi inatarajiwa kuanza mwezi Julai, 2008 na kuchukua takriban miezi 18. Mfuko huo wa Maji, umekwishatenga *Euro* milioni 2.66 kwa ajili ya uchunguzi na usanifu huo. Baada ya hapo, tutaendeleza matengenezo na ukarabati wa miradi hiyo kwa kutumia Mfuko wa Kuendeleza Sekta ya Maji.

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, naona hali ambayo ipo kule Kigoma Mjini inafanana kabisa na hali iliyoko kwenye Jimbo la Mbinga Magharibi Ziwa Nyasa. Je, ni lini Serikali itafikiria kusambaza maji kutoka Ziwa Nyasa na kupeleka kandokando ya vijiji vyote vinavyoambaa Ziwa Nyasa ili wananchi waweze kupata maji safi?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, sio rahisi kabisa kusema ni lini sasa maji hayo yatatoka katika Ziwa Nyasa na kusambazwa, isipokuwa kama nilivyowaeleza, hii Programu yetu ya Kuendeleza Sekta ya Maji, inaangalia mambo yote ikiwa ni pamoja na vyanzo vipya vya maji na vyanzo vingine ambavyo vipo lakini maji bado hayajaweza kufika.

Kwa hiyo, utaratibu tulionao sasa ni huu wa kufanya upembuzi yakinifu, kuangalia ni jinsi gani maji yanaweza kutolewa katika Ziwa Nyasa na hasa ukizingatia kwamba, suala sio kuyatoa na kuyapeleka kwa wananchi, lakini baada ya kuyapeleka pia lipo tatizo la uendeshaji. Mahali pengine tunaangalia kwamba, tunahitaji kuweka miradi ya mtiririko badala ya kuyapampu kutoka huko yalipo na kuyapeleka juu kunusuru wananchi na gharama zile.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimuahidi Mheshimiwa Komba kwamba, programu yetu itaendelea na utafiti wa kina, kuangalia maji ya Ziwa Nyasa yaweze kutumika kama ilivyo kwa Ziwa Tanganyika.

Na. 14

**Matatizo ya Maji – Lindi Mjini**

**MHE. FATMA A. MIKIDADI** aliuliza:-

Kwa kuwa Halmashauri ya Mji wa Lindi inakabiliwa na matatizo makubwa ya maji kwa miaka kadhaa sasa kutokana na kuziba kwa mabomba yanayopitisha maji kwa sababu ya kutofanyiwa ukarabati mara kwa mara kwa miaka mingi na vyanzo vya maji kuwa mbali sana na Mji huo kutokana na kuzungukwa na Bahari ya Hindi; na kwa kuwa mahitaji ya maji kwa wakazi wa mji huo ni lita milioni tano lakini sasa wanapata lita1,400,000; na kwa kuwa tatizo hilo limewafanya watu wenye uwezo kununua maji toka Ndanda – Masasi umbali wa km 80 na kuyauza kwa Sh.1,000 kwa ndoo maji ambayo sio salama; na kwa kuwa Serikali ilikuwa imeahidi miradi mbalimbali ya maji tangu mwaka 2003 kwa nia ya kusaidia upatikanaji wa maji lakini haionyeshi mafanikio yoyote:-

Je, Serikali haioni kuwa, kuna haja na umuhimu wa kuchimba visima vya maji angalau kwa kila Kata kwenye maeneo ya Mitwero, Kineng’ene, Kitumbikwela, Mtanda, Ndoro, Rahaleo, Mikumbi Wailesi, Mtanda, Msinjahili, Matopeni na Makonde ili kunusuru maisha ya wananchi wa maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fatma Abdallah Mikidadi, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu ilifanya uchunguzi wa vyanzo vya maji chini ya ardhi kwa ajili ya Mji wa Lindi. Uchunguzi huo, ulifanyika katika maeneo mbalimbali yakiwemo aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge. Matokeo ya uchunguzi huo, yalionyesha kuwa maji chini ya ardhi katika maeneo mengi yana chumvi nyingi, kwa hiyo, hayafai kwa matumizi ya binadamu. Aidha, katika maeneo ya Mitwero, Mtanda na Kineng’ene, uchunguzi umeonyesha kuwepo maji

kidogo sana chini ya ardhi. Matokeo haya ya uchunguzi yanaashiria kuwa mkakati wa kuboresha huduma ya maji Mjini Lindi kwa kuchimba visima, hauna matumaini makubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu ina mipango ya muda mfupi na muda mrefu ya kupunguza matatizo ya maji katika Mji wa Lindi. Mipango hiyo itatekelezwa chini ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji.

Mpango wa muda mfupi, kama ilivyo katika baadhi ya miji mingine ni kuchukua hatua ambazo zitaleta matokeo ya haraka ya kupunguza tatizo la maji. Kwa mfano, Mwezi Februari 2008, Wizara yangu iliipelekea Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Mjini Lindi, shilingi milioni 70 kwa ajili ya ukarabati wa kitekeo cha maji cha Mongo na ununuzi wa mafuta ya kuendeshea mitambo ya kusukuma maji iliyopo Mitwero na Visima vya Kitunda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwaka 2005 Wizara yangu ilikamilisha usanifu wa kina na kutayarisha makabrasha ya zabuni kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu ya majisafi; ujenzi wa njia ya kupeleka umeme kwenye visima vya Kitunda; ukarabati wa kituo cha kusukuma maji cha Mtaa wa Kawawa; ufungaji wa mitambo mipya kwa ajili ya kituo hicho; na ukarabati wa kilometa 47 za mabomba katika maeneo mbalimbali Mjini Lindi. Mwezi Novemba, 2007 Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Mjini Lindi, ilitangaza zabuni ya kumtafuta Mhandisi Mshauri atakayesimamia ukarabati huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini ya zabuni za Wahandisi Washauri ilikamilika mwezi Februari, 2008, kinachosubiriwa ni ridhaa ya Benki ya Dunia (*no objection)*, kuiruhusu Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Lindi kuingia mkataba na Mhandisi Mshauri. Ridhaa hiyo inatarajia kupatikana kabla ya mwezi Julai, 2008. Hivi sasa Benki ya Dunia, inapitia makabrasha ya zabuni ya ujenzi, ikiridhia makabrasha hayo inatarajiwa kuwa, baada ya miezi miwili mkandarasi atapatikana na kufuatiwa na kazi ya ukarabati inayotarajiwa kuchukua takriban miezi 15.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa muda mrefu wa kuwapatia Wananchi wa Lindi huduma bora ya maji ni sehemu ya Mradi Kabambe wa Uboreshaji wa Miundombinu ya Majisafi na Majitaka katika miji saba ya Babati, Bukoba, Kigoma, Lindi yenyewe, Mtwara, Musoma na Sumbawanga. Mradi huo unafadhiliwa na Mfuko wa Maji wa Jumuiya ya Ulaya *(ACP-EU Water Facility*). Jumla ya fedha zitakazotumika kwa ajili ya kugharamia uchunguzi na usanifu, ambao utazingatia mahitaji ya huduma ya majisafi na majitaka kwenye miji hiyo hadi mwaka 2025, ni *Euro* milioni 2.66.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua iliyofikiwa hadi sasa ni Wizara kutayarisha kabrasha (*Request for Proposal)* la kuwaongoza Wahandisi Washauri, walioomba kupewa kazi hiyo katika kuandaa zabuni zao. Katika kutekeleza Mradi huo, maeneo yatakayofanyiwa uchunguzi wa kutafuta vyanzo vya maji ni Kitunda, Chipwapwa na Bonde la Ngongo. Hadidu za rejea za usanifu huo, zilikamilishwa mwezi Aprili, 2008 na kutumwa kwenye Mfuko wa Maji wa Umoja wa Ulaya. Mfuko huo ndio

utakaokamilisha taratibu za kumpata Mhandisi Mshauri na baada ya hapo, kazi inatarajiwa kuchukua muda wa miezi 18 katika hatua ya usanifu kabla ya hatua ya ujenzi kuanza.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa Halmashauri ya Mji wa Masasi haina tofauti sana kwa matatizo ya maji kama yalivyo kwenye Mji wa Halmashauri ya Lindi; na kwa kuwa Masasi inapata maji kutoka kwenye Chemchemi ya Mwena, ambapo miundombinu yake hasa mabomba na kadhalika yamekwishaharibika. Je, Serikali ina mpango gani katika utaratibu huu ili kuhakikisha kwamba Masasi nayo inakarabatiwa iweze kupata maji safi na ya uhakika?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu kwa kifupi swali la nyongeza la Mheshimiwa Mrope kwamba, Masasi nayo haina tofauti na Wilaya nyingine katika kutekeleza Programu ya Kuendeleza Sekta ya Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachotakiwa tu na ambacho Mheshimiwa Mbunge akielewe kwa ufupi ni kwamba, tunapotoa taratibu za kuomba miradi, basi ni jambo la maana sana kama Halmshauri hizi nazo zitaanza kufuata utaratibu ambao tunauweka ili ziweze kupata fedha hususan hizi za Programu ya Kuendeleza Sekta ya Maji na hasa hizi fedha za *World Bank.* Kwa kweli tatizo lililojitokeza sina hakika kama ni Masasi; lakini Halmshauri nyingi zimeshindwa kukidhi mahitaji yale ambayo yanatakiwa na *World Bank.* Kwa mfano, katika Halmashauri 131 ni Halmashauri 61 tu mpaka sasa ambazo zipo tayari ili washauri waweze kuteuliwa. Halmashauri nyingine zina hali mbaya, tumezirudishia kama Halmashauri 33 ili ziweze tena kupitia mchakato ule wa kuandaa watu au washauri watakaotekeleza miradi hii. Halmshauri zitakazobakia zote zimeshindwa kufanya kazi hiyo na kitakachofanyika sasa ni kuzirudishia zianze upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, sina hakika ya Masasi kwa sasa hivi, lakini naomba niseme kwamba, orodha ya Halmashauri zote ambazo zimefanikiwa kukidhi mahitaji, zile ambazo zinasahihisha na zile ambazo zimeshindwa kabisa na tunataka zianze upya, nitawasambazia Wabunge wazitambue.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, swali hili kama mme-*notice* limekuwa refu mno. Kwa hiyo, tunaendelea Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika.

Na. 15

**Panya Waharibifu Kutegua Mabomu**

**MHE. HAROUB SAID MASOUD** aliuliza:-

Kwa kuwa tarehe 16 Aprili, 2008 Serikali wakati ikijibu swali namba 84 linalohusiana na udhibiti wa panya waharibifu, ambapo Serikali ilikiri kuwepo kwa panya

hao na kuahidi kuwapunguza kwa kiasi cha kutowasababishia wakulima hasara kubwa, lakini imethibitishwa na wataalam wa Chuo cha Kilimo Sokoine *(SUA)* kuwa, panya hao wamepewa taaluma ya kutegua mabomu, jambo ambalo kama watatoweshwa kabisa itakuwa hasara kwa nchi yetu kutokana na umuhimu wao katika suala la kutegua mabomu.

(a) Ikiwa utafiti huo ni kweli, je, ni panya wangapi wameshapewa taaluma hiyo?

(b) Je, kuna nchi nyingine yoyote ambayo imeomba kupewa panya hao na taaluma ya kubaini mabomu toka Tanzania?

(c) Kama jibu ni ndiyo; je, ni fedha kiasi gani zinazotozwa kwa panya mmoja anayechukuliwa nje ya nchi kufanya kazi hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Mbunge wa Koani, napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna aina 25 ya panya waharibifu wa mazao hapa Tanzania. Kwa kipindi cha zaidi ya miaka kumi sasa ni panya wa aina tatu; hususan panya shamba *(Mastomys Natalensis*), panya dari *(Rattus Ruttus)* na panya majani (*Arvicanthis*), ambao wamekuwa wakisababisha uharibifu mkubwa wa mazao wanapotokea kwa wingi au milipuko na kusababisha Serikali kuingilia kati kuwadhibiti. Aina ya panya waliofundishwa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo *(SUA)* ni panya buku *(Cricetomys Gambianus).*

Aidha, Wizara inapenda kutoa ufafanuizi kuwa panya hao wanafundishwa kuvumbua eneo ambalo lina mabomu yaliyotegwa aridhini, kwa kunusa baruti yake na wala sio kutegua mabomu. Panya buku hawajafikia hali ya mlipuko, kwa hiyo, hawasabishi uharibifu wa mazao na mara watokeapo hudhibitiwa na wakulima wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Haroub Said Masoud, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Utafiti huu ni kweli na hadi sasa wapo panya wapatao thelathini, ambao wamefuzu mafunzo ya kuvumbua eneo ambalo lina mabomu yaliyotegwa ardhini. Panya wengine wapatao hamsini wapo katika hatua mbalimbali za mafunzo hayo.

(b) Utafiti huu unafanywa kwa kushirikiana na nchi za Ubelgiji na Msumbiji. Hadi sasa panya 18 wamepelekwa Msumbiji, kwa shughuli ya kuvumbua maeneo yaliyotegwa mabomu ardhini na hakuna nchi yoyote iliyokwishaomba utaalam huu mpaka sasa hivi.

(c) Panya hawa hawauzwi kwa sababu lengo la ufadhili huu ni kuhudumia jamii kuondokana na adha ya mabomu ya kutegwa ardhini na siyo lengo la kibiashara.

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa hawa wataalam wetu wa Chuo cha Sokoine wamefanya jambo ambalo limeiletea heshima kubwa nchi yetu; je, Serikali imefanya nini juu yao ili kuwazawadia wataalam hao?

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nataka kumpongeza sana Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na ya kina, kuhusu utafiti ambao umefanywa na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo. Kazi ya Vyuo Vikuu moja ni kufundisha, pili kufanya utafati na tatu kutoa ushauri. Kwa hiyo, haya ni majukumu yao wenyewe.

Serikali imefanya nini kuwazawadia na kuwatambua kwa kazi nzuri iliyofanywa; Serikali binafsi inatambua kazi nzuri waliyofanya na kwamba, imeiletea heshima nchi yetu na kuna taratibu za chuo ambazo panapokuwa na kazi nzuri zinazofanyika, basi wale waliofanya utafiti huo, hutambuliwa kwanza kabisa kwa kupandishwa vyeo. Chuo Kikuu hakipandishwi daraja moja kwenda lingine ila kwa utafiti. Kwa hiyo, wale waliofanya kazi nzuri, tayari wameshapandishwa vyeo na vilevile wanatambulika kimataifa. Ahsante sana. (*Makofi*)

Na. 16

**Mpango wa Kitaifa wa Ufugaji Nyuki**

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA** aliuliza:-

Kwa kuwa Tanzania ina makundi mengi ya nyuki watoa asali na sasa asali na nta zina bei nzuri sana kwenye soko la nje:-

Je, Serikali haioni kuwa ingekuwa jambo muhimu kuwa na mpango wa kitaifa wa ufugaji nyuki ili asali na nta zisaidie kuongeza Pato la Taifa?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Tanzania ina makundi mengi ya nyuki yanayokadiriwa kuwa milioni 9.2. Serikali baada ya kuona umuhimu wa shughuli za ufugaji nyuki nchini, iliandaa Sera ya Taifa ya Ufugaji nyuki ya mwaka 1998. Ili kutekeleza Sera hiyo, mwaka 2001 Idara ya Misitu na Nyuki chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii, iliandaa Programu ya Taifa ya Ufugaji Nyuki. Programu hiyo inatoa utaratibu wa nini cha kufanya na nani afanye. Aidha, Programu hiyo ilikusudia pamoja na malengo mengine, kuimarisha upatikanaji endelevu wa mazao ya nyuki; kuongeza mchango wa sekta ya nyuki katika Pato la Taifa na kuwezesha mfumo wa kisheria wa usimamizi wa sekta hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza Programu hiyo, Serikali ikishirikiana na washiriki katika maendeleo, imetoa mafunzo ya ufugaji nyuki endelevu na uzalishaji wa mazao ya nyuki yenye ubora unaotakiwa, utengenezaji wa mizinga sahihi, vifaa na mavazi ya kinga na kutoa mizinga na mavazi ya kinga ya mfano, pia kuhamasisha wafugaji wa nyuki na kutenga hifadhi za nyuki. Mafunzo na mbinu bora za ufugaji wa nyuki na utoaji wa vifaa kwa wafugaji wa nyuki, kuliongeza idadi ya mizinga kwa kila mfugaji nyuki kutoka wastani wa mizinga 6 kwa mfugaji mwaka 1998 hadi wastani wa mizinga 62 mwaka 2005. Wastani wa mizinga ya magome imeshuka toka mizinga 7 mwaka 2003/2004 hadi wastani wa mizinga 2 mwaka 2004/2005, wakati uzalishaji wa mazao ya nyuki uliongezeka toka wastani wa kg 349.6 mwaka 2000 kwa kila mfugaji nyuki hadi wastani wa kg 407 mwaka 2005. Aidha, mapato yatokanayo na nta na asali kwa wafugaji nyuki pia yaliongezeka kutoka wastani wa shilingi 180,000 mwaka 2000 kwa wafugaji kwa mwaka hadi 456,000 mwaka 2005.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Mheshimiwa Naibu Waziri amesema, kuna makundi ya nyuki yapatayo milioni 9.2. Swali la kwanza; je, anaweza akatueleza ni kiwango gani sasa makundi hayo yamekwishapata mizinga kwa wastani kama sehemu ya mafanikio?

Swali la pili, Naibu Waziri haoni kama huu sio wakati wa kufanya majaribio kwa sababu hakuna sababu ya kufanya majaribio ya mizinga na mizinga bora inajulikana; kwa nini hatuingii moja kwa moja kwenye ufugaji wa nyuki wa kibiashara?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, idadi ya mizinga ambayo makundi hayo yamepata takwimu halisi hapa siwezi kuitoa kwa sababu mizinga mara nyingi nyuki hao hupata makazi na baada ya muda huhama. Kwa ujumla ni kwamba, kuna mizinga mingi zaidi ya milioni sita ambayo ipo kwenye maeneo mbalimbali, lakini nyuki hupata makazi na baadae huhama. Kwa hiyo, kujua ni makundi mangapi kati ya hayo milioni 9.2 si rahisi kutaja kwa sasa.

Kuhusu mkakati wa kuwa na ufugaji wa kibiashara; kuna miradi mingi ambayo inatekelezwa na si majaribio; kuna miradi zaidi ya 23 ambayo inatekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na wafadhili mbalimbali katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu. Orodha ninaweza nikampatia, ambayo inalenga kuboresha sekta nzima ya ufugaji nyuki, lakini tuna hiyo miradi ambayo inaboresha na kuufanya uwe wa kisasa.

Na. 17

**Uwekezaji Kwenye Viwanja vya Ndege**

**MHE. DR. ALI TARAB ALI** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali inapitia mikataba mibovu ya wawekezaji:-

(a) Je, Mkataba wa Uwekezaji wa Kiwanja cha Ndege cha KIA na Moshi umeshapitiwa?

(b) Je, Serikali inasema nini juu ya madai kuwa, mwekezaji kwenye kiwanja hicho hulipa kodi ya shilingi 700,000 kwa mwaka?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali, Mbunge wa Konde, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Tanzania ina mkataba wa miaka 25, uliosainiwa mwaka 1998 kati yake na Kampuni inayoendesha Kiwanja cha Ndege cha Kilimanjaro *(Kilimanjaro Airports Development Company - KADCO)*. Mkataba huu una lengo la kuwezesha sekta binafsi kuendesha na kuendeleza Kiwanja cha Ndege cha Kilimanjaro. Serikali haina Mkataba wowote unaohusu uendeshaji wa Kiwanja cha Ndege cha Moshi. Kiwanja cha Ndege cha Moshi kinamilikiwa na kuendeshwa na Serikali, kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Serikali kuingia Mkataba wa *KADCO* na Mkataba huo kuanza kutekelezwa, iligundua kwamba, kuna vipengele vyenye utata ndani ya mkataba, ambavyo vilihitaji kupitiwa upya na kufanyiwa marekebisho au kufutwa kabisa. Hivyo, Serikali iliunda Kamati Maalum ambayo ilipitia upya vipengele vya mkataba vilivyokuwa na utata na kuviainisha. Katika kuupitia Mkataba huo, vipengele 49 viliainishwa kuwa na utata na hivyo kuanza mazungumzo na *KADCO* kwa lengo la kuelewana ili vipengele hivyo vifutwe au kufanyiwa marekebisho. Kati ya vipengele 49 vilivyoainishwa, 47 viliafikiwa na pande zote mbili kuwa vifutwe au vifanyiwe marekebisho na kutoa manufaa zaidi kwa Serikali. Vipengele vilivyobaki viwili ambavyo vinahusu suala la *exclusivity* kwa viwanja vya Arusha na Moshi kuondolewa kwenye Mkataba; na pendekezo la Serikali ya Tanzania la kutaka *KADCO* iwe inalipa ada ya upangishaji (*consession fee*), havikuweza kukubalika mara moja na mazungumzo yakaendelea kufanyika.

Hatua ambayo imefikiwa kwa sasa kuhusu vipengele hivyo viwili ni nzuri, ambapo *KADCO* imekubali kimsingi kufutwa kwa kipengele cha *exclusivity* kwa viwanja vya Arusha na Moshi kutoka kwenye Mkataba na pia kuanzishwa kwa ada ya upangishaji *(concession fee*).

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, *KADCO* inalipa malipo ya ukodishaji ardhi *(land lease rent)* ya shilingi 3,398,400 kwa mwaka tangu iliposaini Mkataba na Serikali mwaka 1998 na siyo shilingi 700,000 alizozisema Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. DR. ALI TARAB ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kuna madai kwamba Mwekezaji huyu ana chaji fedha nyingi kwa ndege ambazo zinatua KIA na hivyo kusababisha ndege nyingi zitue Nairobi badala ya KIA; je, Serikali inasema nini kuhusu hili?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, madai kwamba mwekezaji huyu anachaji malipo makubwa tumeyasikia, lakini tutaangalia kama kuna uwezekano wa kuzungumza nae katika vipengele vilivyoainishwa ili kuweza kulitatua tatizo hili.

Na. 18

**Watanzania Waliopotea na Meli ya *Reef Azania***

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED** aliuliza:-

Kwa kuwa kuna Watanzania wengi wanaofanya kazi na wengine wajasiriamali walioko nje ya nchi; na kwa kuwa tarehe 26 Juni, 2007 meli iitwayo *Reef Azania* ilipotea na ndani yake kulikuwa na Watanzania 17:-

(a) Je, Serikali inasema nini juu ya Watanzania hao waliopotea?

(b) Je, kuna utaratibu gani wa kisheria unaofanywa ili wamiliki wa meli hiyo wawajibike na kulipa fidia halisi kama wahusika wamepotea au kufa?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mbunge wa Wawi, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katikati ya mwezi Juni, 2007, meli ya *Reef Azania* iliyokuwa inamilikiwa na Kampuni ya *Zambezi Shipping* ya Dubai, wakati ikiwa safarini kutoka Dubai kwenda Visiwa vya Seychelles kupitia Zanzibar, ilipoteza mawasiliano na mmiliki wa meli hiyo kuanzia tarehe 24 Juni, 2007 na ilikuwa haionekani kwenye mtandao wa satalaiti. Mara ya mwisho ilikuwa imeonekana kwenye eneo la *Latitude* 16, kaskazini mwa *Equator* na *Longitude* 59 mashariki ya mstari wa *Greenwich.*

Meli hiyo ilikuwa na mabaharia 14 kati ya hao Watanzania walikuwa 8; saba kutoka Tanzania Zanzibar na mmoja kutoka Tanzania Bara.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kupata taarifa ya kupotea kwa meli hiyo, Serikali ilichukua hatua mbalimbali za kutafuta namna ya kuwaokoa mabaharia waliopotea. Miongoni mwa hatua hizo ni pamoja na kutoa taarifa kwa Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Kikosi cha Ulinzi katika eneo la bahari ya Uarabuni na kuwasiliana na mwenye meli ili kushirikiana nao katika kuitafuta meli hiyo. Juhudi kubwa za kuitafuta meli hiyo kwa ushirikiano baina ya mwenye meli na vikosi vya ulinzi katika eneo la ghuba kwa kutumia meli na ndege maalum za utafutaji, zilifanyika bila mafanikio yoyote. Kutokana na kushindikana kupatikana kwa meli hiyo, Kampuni ya *Lioyas Maritime Investigation Unit*, ilitangaza rasmi juu ya kupotea kwa meli hiyo na kila kilichokuwemo tarehe 30 Agosti, 2007 na hivyo kusitisha rasmi zoezi la utafutaji wa meli hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusitishwa rasmi kwa zoezi la utafutaji wa meli hiyo, Serikali ilihakikisha inachukua hatua za kufuatilia upatikanaji wa fidia kwa wahusika na ndugu waliopotea. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, mabaharia wa Kitanzania katika meli ya *Reef Azania*, wameshalipwa fidia zao. Serikali ilisimamia zoezi zima tangu kulipwa mishahara yao hadi kulipwa fidia ya kupoteza maisha. Fidia ya mabaharia hao, ililipwa rasmi mwezi Machi, 2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kusimamia kwa karibu ajira za Mabaharia wa Kitanzania katika meli za kigeni kwa kuhakikisha kuwa wanakuwa na mikataba inayolinda haki zao wanapokuwa kazini.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruhusa yako, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa taarifa aliyotoa Mheshimiwa Naibu Waziri sehemu nyingine si kweli; je, Waziri tutakapotoa taarifa ya kweli kwa sababu mimi ndiyo niliyesaidia kuwapeleka Mahakamani na kuzuia meli isiondoke Zanzibar ili Wahusika walipwe na si juhudi za Serikali; nitakapothibitisha hilo Waziri anaweza kukubali kwamba amelidanganya Bunge?

Swali la Pili; kwa kuwa Serikali ilipata taarifa mapema juu ya kupotea kwa meli hii na haikuchukua hatua yoyote mpaka pale wahusika walipotoa taarifa; na kwa kuwa nchi yetu inashirikiana na vyombo vingi sana vya ulinzi hasa vya magharibi; je, kwa nini Serikali haikuchukua hatua mapema na kuwaarifu Watanzania juu ya athari iliyopatikana kutokana na meli hii?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, kwanza lile swali la kwanza alichodanganya ni nini hatukuelewa?

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, Naibu Waziri amesema kwamba, Serikali ndiyo iliyosimamia kulipwa kwa haki zao. Mimi nilitafuta Wakili akaenda Mahakama Kuu ya Zanzibar, wakazuia meli ya mhusika, ndiyo mhusika akaweza kulipa. Nina ushahidi na kesi ipo na Wakili aliyeifanya kazi hiyo yupo. Kauli aliyoisema Mheshimiwa Naibu Waziri si sahihi.

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza nimesema kwamba, Serikali ilikuwa na jitihada za kuhakikisha kwamba, wahusika wanalipwa. Sasa kama Mheshimiwa Mbunge alishiriki, kwa kweli ilikuwa ni kusaidiana na jitihada za Serikali.

Kwa vyovyote vile, katika utaratibu wa malipo; malipo hayawezi yakafanywa bila uthibitisho rasmi kutoka kwenye Vyombo vya Serikali. Kwa hiyo, Serikali ilithibitisha

kwamba, kweli kulikuwa na upotevu huo. Vingenevyo, bila kuthibitisha ingekuwa ni vigumu sana kufanikiwa kwa malipo hayo.

La pili, niseme tu kwamba, Serikali kama nilivyosema, mara ilipopata taarifa ya kupotea kwa meli hii, ilianza kuwasiliana na vyombo mbalimbali na ilisubiri mpaka chombo rasmi kitoe tangazo kwamba, Meli hii sasa haionekani kabisa na ndipo hatua zikaanza kuchukuliwa. Kwa hiyo, haijachukua muda mrefu kama nilivyosema katika jibu la msingi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Siasa bwana, wanatafuta maeneo kwa nini usiseme ahsante sana kwa juhudi zako na yakaishia hapo. (*Kicheko*)

Na. 19

**Matibabu Nje ya Nchi kwa Askari Polisi**

**MHE. ISSA KASSIM ISSA** aliuliza:-

Kwa kuwa kumekuwa na taratibu ambazo zinachukua muda mrefu na kutopata mafanikio pale askari wa vyeo vya chini kwenye Jeshi la Polisi wanapopata ajali wakiwa kazini na wanapotakiwa kupatatiwa matibabu nje ya nchi, Jeshi la Polisi linapata kigugumizi kuwapeleka askari hao kwenye matibabu kama inavyoelekezwa na Madaktari husika:-

(a) Je, Serikali inaliambia nini Bunge juu ya askari hao wanaopata ajali wakiwa kazini na kutopatiwa matibabu yao kulingana na maelekezo ya Daktari; na ni kwa nini askari hao wananyimwa fursa hiyo?

(b) Je, ni fidia gani inayolipwa kutokana na askari kupata ajali akiwa nje ya kituo chake cha kazi?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Issa Kassim Issa, Mbunge wa Mpendae, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la kumhudumia askari yeyote anayeumia akiwa kazini ni la Serikali. Askari Polisi wanaopata ajali wakiwa kazini, hupatiwa huduma ya matibabu katika Zahanati, Hospitali na Hospitali za Rufaa za Serikali, zikiwemo zile za Polisi zilizopo Mikoani na hata nje ya nchi kulingana na ushauri utakaotolewa na Madaktari. Hivyo, askari yeyote ambaye itaelekezwa akatibiwe nje ya nchi, basi Serikali huchukua jukumu la kugharamia matibabu hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa matibabu hayo nje ya nchi ni kwamba, Wizara ya Afya inagharamia matibabu na Jeshi la Polisi hugharamia posho ya kujikimu na tiketi, kwa mujibu wa Kanuni za Utumishi Serikalini (1994) kifungu Na. K. 10.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Askari yeyote anayepata ajali akiwa kazini nje ya kituo chake cha kazi na baada ya kupata matibabu, hulipwa fidia kwa mujibu wa Sheria ya *Workman's Compensantion Act, Cap. 263 R.E 2002.* Taratibu zote za malipo zimeainishwa katika sheria hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na uwepo wa sheria hiyo, fidia inayolipwa kwa mtumishi anayeumia kazini na hata ndugu wa mtumishi anayefariki kwa ajali kazini ni ndogo. Changamoto iliyopo mbele yetu kama Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, tupo katika mchakato wa kutayarisha utaratibu mzuri wa kuwalipa fidia, askari wanaoumia wakiwa kazini kupitia mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya *The Police Force and Prisons Service Commission Act, CaP. 241 R.E 2002*.

**MHE. ISSA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa jibu zuri na imani aliyokuwanayo Mheshimiwa Naibu Waziri huyu.

Yupo askari D. 5686, Koplo Amour, aliumia Kigoma na akalazwa kwenye Hospitali ya Bugando kwa siku 21, akapata uhamisho kwenda Muhimbili na kulazwa kwa siku 14; Madaktari wakashindwa, ikabidi apate uhamisho wa matibabu nchini India, kwenye Hospitali ya Apolo. Hadi hii leo tangu alipopata ajali tarehe 10 Oktoba, 2007; je, tatizo gani lililotokea hadi leo hajapelekwa matibabuni India na hali anaathirika na ugonjwa huo wa kukatika uti wa mgongo?

Swali la pili; je, tatizo kama hili angelipata Askari wa cheo cha juu hadi leo angelikuwa akipata mateso hayo bila kupelekwa nje ya nchi?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, niseme tu huyo Koplo Amour, ajali aliyoipata, hakuipata akiwa Kigoma, isipokuwa hiyo ajali ilitokea Mkoani Kagera. Kitu ambacho kimefanyika ni kweli tulifuata taratibu kwa sababu kwanza alitazamwa katika Hospitali ya Bugando na baadaye alipelekwa Hospitali ya Muhimbili, ambapo Kituo cha *MOI* kilifanya jitihada za kuona kwamba, wanafanya utaratibu wa kumpa matibabu.

Kwa kuwa pale ilionekana kwamba, inapendekezwa apelekwe nje, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu na nimhakikishie ndugu yangu, Mheshimiwa Issa kwamba, taratibu zote zimefanyika kuhusu Koplo huyu na hivi tunavyozungumza, kibali tayari kimekwishapatikana kutoka Wizara ya Afya na Pasi ya Usafiri nje ya nchi ameshaipata na taratibu zote tunazikamilisha sasa hivi na nadhani wakati wowote anaweza akaondoka. Ningependa kumshukuru kuona kwamba ni Mbunge makini, ambaye anafuatilia ajali ambazo wanapata watu wake. Ahsante.

Na. 20

**Ongezeko la Ajali za Mabasi Nchini**

**MHE. PINDI H. CHANA** aliuliza :-

Kwa kuwa hivi karibuni kumekuwepo na ongezeko kubwa sana la ajali za mabasi ya abiria ambapo watu wengi wamefariki na wengine kupata ulemavu na majeraha ya kudumu; na kwa kuwa yapo mabasi yenye takwimu za kupata ajali mara kwa mara :-

(a) Je, Serikali ina mpango gani na makampuni yanayomiliki mabasi hayo?

(b) Je, Serikali haioni kuwa wakati umefika wa kutoa mwongozo wa udhibiti wa makampuni husika?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu :-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Pindi Chana, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo :-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haikuwa na utaratibu wa kuyachukulia hatua makampuni yenye mabasi yanayosababisha ajali mara kwa mara na badala yake, imekuwa ikichukua hatua ya kuwafikisha mahakamani madereva wa makampuni ambayo mabasi yake yamekuwa yakisababisha ajali. Madereva hao wanapothibitika kusababisha ajali, huchukuliwa hatua kali zikiwemo za kusitisha kwa muda au kufuta leseni zao za udereva au kifungo au vyote kwa pamoja.

Kwa kuwa suala la udhibiti wa huduma za usafirishaji lipo mikononi mwa Mamlaka ya Udhibiti wa Nchi Kavu na Majini (*SUMATRA*), Serikali kupitia Mamlaka hiyo, imeandaa kanuni zitakazotoa mwongozo utakaosaidia udhibiti katika Sekta ya Usafiri wa Barabara ukiwemo udhibiti wa makampuni yanayotoa huduma za usafirishaji abiria. Kanuni hizo ni pamoja na:-

(i) Kanuni za leseni za usafirishaji kwa magari ya abiria za 2007.
(ii) Kanuni za viwango vya ubora na huduma kwa magari ya abiria za 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, kanuni za leseni za usafirishaji kwa magari ya abiria za 2007, tayari zimeshaidhinishwa na kanuni za viwango vya ubora na huduma kwa magari ya abiria za 2007, zipo katika hatua za mwisho za uchapaji. Utekelezaji wa kanuni hizo, utasaidia kudhibiti makampuni yanayotoa huduma ya usafirishaji wa abiria na kupunguza ajali barabarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwa na kumbukumbu sahihi za mabasi ambayo yanasababisha ajali mara kwa mara, Jeshi la Polisi linaandaa mfumo wa teknolojia ya kisasa ya kukusanya na kutunza takwimu hizo. Kupitia utaratibu huo, Jeshi la Polisi litatoa taarifa na takwimu za mabasi yanayosababisha ajali kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (*SUMATRA*) na kuishauri Mamlaka hiyo kusitisha au kufuta leseni za mabasi au makampuni ambayo yatabainika kusababisha ajali mara kwa mara.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Naibu Waziri, ambaye tumekubaliana kwamba, hatuna utaratibu wa kuzuia leseni za mabasi, lakini tulikuwa tuna utaratibu wa kunyang'anya leseni kwa dereva aliyesababisha ajali ; na kwa kuwa Naibu Waziri ametueleza kwamba, Serikali inafanya jitihada kupitia Jeshi la Polisi kuweka utaratibu kabambe ambao ni *computerised* wa kuangalia magari yanayopata ajali; ningependa kujua, utaratibu huo utakamilika lini?

Ningependa vilevile kuishauri Serikali, kwa sababu magari yale ambayo yanapata ajali mara kwa mara, maana yake yamepoteza sifa za kusafirisha abiria, yaani Watanzania ; na kwa kutambua hilo, Serikali itakubalina na ushauri wangu kwamba ikitokea kampuni ya usafirishaji wa binadamu, mabasi yamepata ajali zaidi ya mara mbili au mara tatu na inakuwa imepoteza sifa ; basi kampuni hiyo ifungiwe kusafirisha abiria?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI :** Mheshimiwiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu ambao nimeutaja hapo awali, ambao Jeshi la Polisi linajaribu kutengeneza na kubaini wa kuweza kuhakikisha kwamba, takwimu zinakusanywa kuhusu mabasi ambayo yanasababisha ajali barabarani, ni mpangilio wa Wizara yetu kuhakikisha kwamba, pindi ifikapo mwaka wa fedha, mwaka kesho, zoezi hili litakuwa limekamilika. Hili ni zoezi ambalo kwa kweli linahitaji fedha ili kuweza kulikamilisha.

Kwa hiyo, tunajitahidi limekwishaanza, lakini ni kitu ambacho kinakwenda jinsi ajali zinavyotokea. Ningependa kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, ifikapo mwaka kesho kipindi cha bajeti kama hiki, tutakuwa tumekamilisha utaratibu huo.

Kuhusu swali la pili, makampuni ambayo yana mabasi ambayo yamekuwa yanasababisha ajali mara kwa mara barabarani kwamba, yachukuliwe hatua kali ; hiyo ni katika mapendekezo yaliyopo na ushauri wake tutauzingatia wa kusema kwamba, yale ambayo yamepindukia zaidi ya mara mbili, mara tatu, yafungiwe; nadhani kwa upande wangu naweza kusema kwamba ni ushauri ambao ni muhimu na ni bora. Kwa hiyo, naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutauzingatia. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yameisha. Tumechukua muda wa dakika tano zaidi, kutokana na maswali mawili majibu yake kuwa marefu. Sasa tuna wageni hapa mbele yetu kwenye *Public Galle*ry. Kwanza kabisa, tuna mgeni wa Mheshimiwa Raynald Mrope, ambaye ni mtoto wake, Bwana Ray Mrope, Jr. asimame aliko.

*(Hapa mgeni aliyetajwa alisimama)*

**NAIBU SPIKA:** Huyu ni mwanaye Bwana Mrope, ambaye yupo masomoni Marekani.

Tuna wageni wa Mheshimiwa Savelina Mwijage; wapo watoto wake watatu hapa na wifi yake. Naomba wasimame walipo. Ninaambiwa leo hawajafika, watafika kesho.

Ninao wageni wa Waheshimiwa Wabunge wa Mwanza, Waziri wa Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Lawrence Masha, Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mheshimiwa Maria I. Hewa na Mheshimiwa Anthony Diallo, ambao ni madiwani 25, watendaji 15 ambao wameongozwa na Naibu Meya wa Jiji la Mwanza. Kwanza, tumwone Naibu Meya wa Jiji la Mwanza Mstahiki John Minja, asimame.

*(Hapa Mstahiki Meya aliyetajwa alisimama)*

**NAIBU SPIKA:** Madiwani kwanza, wasimame.

*(Hapa Madiwani waliotajwa walisimama)*

**NAIBU SPIKA:** Halafu Watendaji wasimame.

*(Hapa Watendaji waliotajwa walisimama)*

**NAIBU SPIKA:** Mtu anasema ku-*declare interest,* basi niwaambieni Kichama mimi ni Mlezi wa Mkoa wa Mwanza, kwa hiyo na mimi ni wageni wangu. Karibuni sana.

Waheshimiwa Wabunge, tunao wanafunzi 50 na walimu wao kutoka Shule ya Msingi ya Southern Highlands Mafinga. Naomba msimame na walimu.

*(Hapa Walimu na Wanafunzi waliotajwa walisimama)*

**NAIBU SPIKA:** *Wonderful!* Tunafurahi kwamba, mmetoka mbali kuja kushiriki katika mambo haya ya Bunge, karibuni sana.

Halafu ninaye mgeni wa Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya, mama yake mzazi, Mama Kuluthumu Ruhwanya. Karibu sana mama. *(Makofi/Kicheko)*

Bada ya hapo, nina matangazo ya kazi. Kwanza kabisa, Waheshimiwa Wabunge ambao ni Wajumbe wa Kamati ya Uongozi, wanaagizwa na Mheshimiwa Spika kwamba, leo saa 7.30 baada ya kuahirisha kikao hiki, kutakuwa na kikao katika Ukumbi wa Spika.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Spika, anawatangazia Wajumbe wa Kamati ya Uongozi kuwa, kutakuwa na kikao cha Kamati leo saa 7.00 mchana. Kamati ya Uongozi ni Wenyeviti wote wa Kamati mbalimbali.

Tangazo lingine, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, anawataarifu Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi kuwa, kuna kikao muhimu cha Kamati leo tarehe 11 Juni, 2008, saa 7.00 mchana katika ukumbi namba 231, ghorofa ya pili. Wajumbe wote wa Kamati hiyo wahudhurie.

Mheshimiwa Job Ndugai, ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, anaomba Wajumbe wake wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira

kwamba, leo saa 7.00 mchana kutakuwa na kikao cha kamati katika ukumbi namba 428, ghorofa ya nne. Wajumbe wote wanaombwa wahudhurie.

Mheshimiwa George Mkuchika, Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, anawatangazia Wabunge wote wanaopenda kwenda Dar es Salaam Siku ya Ijumaa kwa madhumuni ya kuona na kuishangilia timu yetu ya Taifa *(Taifa Stars)*, inaposhindana na Cameroon; waorodheshe majina yao hapo *reception*. Lengo ni kujua idadi yao ili kuandaa usafiri wa kuwapeleka na kuwarudisha. Zoezi hili litaratibiwa na Mheshimiwa Joel Bendera, Naibu Waziri. Siku ya Ijumaa ni baada ya kusoma Bajeti, kutakuwa hakuna kazi za Bunge. Kwa hiyo, wanaopenda kushiriki katika mchezo huo, wajiandikishe pale nje na Mheshimiwa Joel Bendera ataratibu zoezi hilo.

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Ukaguzi wa Hesabu za Umma wa Mwaka 2008 *(The Public Audit Bill, 2008)*

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

*(Muswada uliotajwa hapo juu ulisomwa Bungeni kwa Mara ya Kwanza)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mtatambua kwamba, tunao Muswada huu wa Sheria ya Ukaguzi wa Hesabu za Umma wa Mwaka 2008 *(The Public Audit Bill, 2008)*, Kusomwa Mara ya Kwanza na hatua nyingine zote. Sasa, Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 93(1), (2) mpaka ya (3), inasema Bunge halitashughulikia hatua zaidi ya moja kwa Muswada wowote wa Sheria katika Mkutano mmoja wa Bunge. Hiyo ni Kanuni ya kwanza katika Kanuni ya 93. Kanuni ya pili ; Bila ya kuathiri masharti ya fasili ya kwanza ya Kanuni hii, Bunge linaweza kushughulikia Muswada wa Sheria katika hatua zaidi ya moja endapo:-

(a) Hoja mahususi itatolewa kwamba Muswada huo ushughulikiwe katika hatua zaidi ya moja;

(b) Spika ataridhika na hoja hiyo; na

(c) Bunge litaafiki hoja hiyo kwa kupiga kura.

Kifungu cha 3 ; masharti ya fasili ya kwanza ya Kanuni hii hayatatumika kwa Muswada wa Sheria ya Fedha, Muswada wa Matumizi ya Fedha na Muswada wowote unaowasilishwa kwa hati ya dharura. Kwa mujibu wa Kanuni hii, namwita Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, anayeshughulikia shughuli za Bunge, aweze kutoa hoja ili tuweze kuendelea na Muswada huu, ambao unatakiwa kusomwa hatua zote kwa kipindi hiki hiki. Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa maelezo yako, sasa kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu, litengue Kanuni yote ya 93 ili kuwezesha Muswada wa Sheria ya Ukaguzi wa Hesabu za Umma wa mwaka 2008 *(The Public Audit Bill, 2008),* kusomwa kwa hatua zake zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKINOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Hoja ya kutengua Kanuni ya 93 ilipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Wote mmeafiki na tume-*compile* kanuni ya 93 (2) (a), (b) mpaka (c).

**Muswada wa Sheria ya Ukaguzi wa Hesabu za Umma**
**wa Mwaka 2008 *(The Public Audit Bill, 2008)***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**NAIBU SPIKA:** Kama mnavyofahamu, kusomwa Mara ya Kwanza Muswada unakuwa umetimiza siku zake 21, wananchi wanaweza kuufikia na Kamati inaweza kuushughulikia. Kusomwa Mara ya Pili, ndiyo hatua tunayoendelea hii.

Sasa Muswada huu ulishachapwa kwa mujibu wa taratibu zetu, lakini haukuwa umetangazwa na kwa sababu ya ahadi ya Serikali kwamba ulipaswa uwe umeletwa kipindi fulani haikutimizwa, kwa hiyo, imebidi sasa tuanze na Muswada huu kabla ya kesho kipindi cha bajeti. Kwa hiyo, sasa tunaingia hatua ya pili, kwa sababu maandalizi mengine yote yamefanywa kama inavyostahili.

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba, Muswada wa Sheria ya Ukaguzi wa Hesabu za Umma *(The Public Audit Act, 2008),* pamoja na marekebisho yake, sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi, chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Dr. Abdallah Omar Kigoda, Mbunge wa Handeni, kwa kuujadili kwa kina Muswada huu na kutoa ushauri wakati Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi ilipokutana Mjini Dar es Salaam tarehe 03 Juni, 2008 na tarehe 06 Juni, 2008. Nawashukuru pia Mheshimiwa John Momose Cheyo (Mb), Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali, kwa mchango wake wa maandishi na pia Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa (Mb), Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa, kwa michango yao waliyoitoa kwenye mkutano wa wadau

wa kujadili Muswada huu, uliofanyika Mjini Dar es Salaam tarehe 02 Juni, 2008. Vilevile nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali na Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa, kwa michango yao waliyoitoa wakati wa mkutano huo, bila kuwasahau wadau mbalimbali waliotoa michango yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, tumezingatia michango ya Kamati ya Fedha na Uchumi na ile iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge wa Kamati zote mbili, waliohudhuria mkutano wa wadau, pamoja na wadau mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la Muswada huu ni kutunga Sheria ya Ukaguzi wa Hesabu za Umma ili kutekeleza matakwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na kuleta ufanisi katika kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, hususan kumwezesha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kutekeleza majukumu yake kwa uhuru pasipo kuingiliwa na mtu au mamlaka yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, inaainisha kuwepo kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mwenye jukumu la kufanya ukaguzi na kutoa taarifa juu ya ukaguzi wa hesabu za Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Aidha, ibara ndogo ya tano ya ibara ya 143, imeweka bayana kwamba, majukumu na madaraka mengine ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, yatabainishwa katika Sheria husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa majukumu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, yamebainishwa ndani ya Sheria ya Fedha za Umma, Sura 348, Sehemu ya Nne, badala ya kuwa na Sheria inayojitegemea kwa mujibu wa matakwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, kwa mujibu wa makubaliano yaliyofikiwa na Shirikisho la Asasi za Ukaguzi wa Umma Duniani *(International Organization of Supreme Audit Institutions – INTOSAI)*, pamoja na Shirikisho la Asasi za Ukaguzi wa Umma katika nchi za Afrika zinazozungumza Lugha ya Kiingereza *(African Organisation of Supreme Audit Institutions – AFROSAI)*, ambazo Tanzania ni mwanachama. Nchi wanachama zinapaswa kuwa na Sheria inayojitegemea kuhusu Ukaguzi wa Hesabu za Umma ili kukidhi mojawapo ya viwango vilivyowekwa Kimataifa. Aidha, Tanzania ilifanyiwa tathmini na *AFROSAI* mwaka 2006 na kuwekwa katika nafasi ya mwisho katika kufikia viwango vya ukaguzi wa umma Kimataifa, kutokana na kukosekana kwa Sheria inayojitegemea kuhusu Ukaguzi wa Hesabu za Umma.

Mheshimiwa Spika, ili kuiwezesha Tanzania kufikia viwango vinavyokubalika Kimataifa katika ukaguzi wa hesabu za umma, Serikali inakusudia kufanya marekebisho hatua kwa hatua, ambapo kwa kuanzia, Serikali imewasilisha Muswada huu wa kutunga Sheria inayojitegemea ya Ukaguzi wa Hesabu za Umma pasipo kufanyia marekebisho vifungu vya Katiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, madhumuni ya Muswada huu kama nilivyoeleza hapo awali ni kutekeleza matakwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977, kwa kutunga Sheria inayojitegemea ya Ukaguzi wa Hesabu za Umma, yenye kuzingatia Viwango vya Kimataifa *(International Best Practices)* katika taaluma ya ukaguzi wa hesabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya mambo muhimu yaliyozingatiwa katika Muswada huu ni kama ifuatavyo:-

(i) Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kutekeleza majukumu yake kama Taasisi huru pasipo kuingiliwa na mtu au mamlaka yoyote.

(ii) Sheria imepanua wigo wa ukaguzi ili kumwezesha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya ukaguzi wa mazingira *(Environmental Audit)*, ukaguzi wa utambuzi *(Forensic Audit)*, ukaguzi wa ufanisi *(Performance Audit)* na kaguzi nyinginezo ili kusimamia na kudhibiti ipasavyo, matumizi ya fedha za umma.

(iii) Kuweka mfumo madhubuti wa ukaguzi wenye kuzingatia uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma.

(iv) Kubainisha taratibu za uteuzi wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Kaimu Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, sifa, majukumu, taratibu za kuondolewa madarakani na ukomo wa madaraka ambapo anaweza kukaa madarakani kwa vipindi viwili vya miaka mitano mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu umegawanyika katika sehemu Tisa:-

Sehemu ya Kwanza, yenye Kifungu cha kwanza hadi cha tatu, inahusu utangulizi unaobainisha jina la Sheria, muda wa kuanza kutumika kwa Sheria na ufafanuzi wa maneno mbalimbali yaliyotumika katika Sheria hii. Aidha, katika sehemu hii, yamefanyika marekebisho ili kuongeza tafsiri ya jina la Ofisi ya Ukaguzi wa Taifa.

Sehemu ya Pili, yenye Kifungu cha 4, kama kilivyorekebishwa hadi cha 19, inabainisha uteuzi wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kufafanua uteuzi wake, kazi na majukumu yake na muda wa kuwepo madarakani. Kadhalika, kifungu hicho cha nne pia kimeweka sharti la uraia wa Tanzania, kwa mtu atakayeteuliwa kuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kifungu cha 6(1), kimefanyiwa marekebisho kwa kuondoa kigezo cha umri unaofaa kwa uteuzi wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kubainisha muda wake wa kukaa madarakani kuwa ni kipindi kimoja cha miaka mitano, ambapo kinaweza kuongezwa kipindi kingine cha pili.

Sehemu hii pia inabainisha uteuzi wa Kaimu Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, madaraka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, uhuru na hadhi ya ofisi yake, kinga ya kisheria dhidi ya kushtakiwa, haki ya kupata taarifa, mamlaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali na inaweka viwango vya

ukaguzi, pamoja na maadili ya kitaaluma na utozaji wa ada za ukaguzi.  Vilevile sehemu hii inaweka bayana misingi ya uwajibikaji na uwazi kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika utekelezaji wa majukumu yake.

Sehemu ya Tatu  ya Muswada yenye Kifungu cha 20 hadi cha 25, inazungumzia kuendelea kuwepo kwa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi na jinsi itakavyofanya kazi zake kwa uhuru, kwa mujibu wa matakwa ya kifungu cha 143(2) cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na ajira ya wafanyakazi wa Ofisi hiyo, ambayo itazingatia Sheria ya Utumishi wa Umma, pamoja na majukumu ya wafanyakazi hao.

Sehemu ya Nne ya Muswada, inabainisha aina mbalimbali za kaguzi zinazofanywa na zitakazofanywa na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.  Aidha, sehemu hii yenye Kifungu cha 26 hadi cha 29, imebainisha kaguzi hizo kuwa ni ukaguzi wa taarifa za fedha *(Regularity Audit)*, ukaguzi wa utambuzi *(Forensic Audit),* ukaguzi wa ufanisi *(Performance Audit)* na kaguzi nyingine.

Sehemu ya Tano yenye kifungu cha 30 hadi cha 33, inahusu ukaguzi wa hesabu za Mashirika na Taasisi nyingine za Umma, uwasilishaji wa taarifa za hesabu, mamlaka ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali kuteua mkaguzi au kampuni ya ukaguzi yenye sifa zinazokubalika kufanya ukaguzi wa hesabu kwa niaba ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Sehemu ya Sita, inahusu utoaji wa taarifa za ukaguzi.  Sehemu hii yenye Kifungu cha 34 hadi cha 40, inabainisha taratibu za utoaji wa ripoti za ukaguzi za mwaka, ikiwa ni pamoja na ripoti za kaguzi za utambuzi na ufanisi, kaguzi maalum na kaguzi za Mashirika na Taasisi nyingine za Umma.  Aidha, sehemu hii imefuta kifungu cha 38 ambacho kilikuwepo kabla ya marekebisho na kuweka bayana taratibu za kujibu hoja za ukaguzi, ushiriki wa Kamati husika za Bunge katika kujadili ripoti za ukaguzi, taratibu na ukomo wa muda wa kujibu ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na namna ripoti hizo zitakavyotolewa kwa umma baada ya kuwasilishwa Bungeni.

Sehemu ya Saba, kama ilivyorekebishwa yenye kifungu cha 41 hadi cha 46, inahusu masuala ya kifedha na ukaguzi wa hesabu za Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, uteuzi wa Afisa Masuhuli, taratibu za utayarishaji wa ripoti za fedha za mwaka, utayarishaji wa makadirio ya maduhuli na matumizi ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, ambapo ripoti itaandaliwa baada ya mashauriano baina ya Waziri mwenye dhamana ya masuala ya Fedha na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali. Aidha, sehemu hii inatoa mamlaka kwa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali, kuteua mkaguzi mwenye sifa aliyesajiliwa na Bodi ya Wahasibu ya Taifa, ili kukagua mahesabu ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi.

Sehemu ya Nane, kama ilivyorekebishwa yenye Kifungu cha 47 hadi cha 49, inahusu masuala ya ujumla ikiwa ni pamoja na makosa na adhabu zitakazotolewa chini ya Sheria hii, taratibu za kiapo na uandaaji wa Kanuni za Utekelezaji wa Sheria hii. Aidha, chini ya kifungu cha 47 kama kilivyorekebishwa, adhabu ya faini kwa mtu yeyote

atakayepatikana na hatia ya kutenda makosa chini ya sheria hii imeongezwa kutoka shilingi milioni moja hadi shilingi milioni tano.

Sehemu ya Tisa na ya mwisho, kama ilivyorekebishwa yenye vifungu vya 50 na 51, inapendekeza kufanyia marekebisho Sheria ya Fedha za Umma, Sura 348 hususan vifungu vya 26 hadi 41 na aya namba (d), (e) na (f) ya kifungu cha 43 ili kuepusha mgongano wa vifungu baina ya Sheria hizi mbili. Aidha, sehemu hii imeweka bayana kwamba, amri na maamuzi yote yaliyofanyika kupitia vifungu vya sheria vilivyofutwa, yatabaki kuwa ni halali, kama ambavyo amri na maamuzi hayo yatakuwa yametolewa chini ya Sheria mpya ya Ukaguzi wa Hesabu za Umma hadi hapo Sheria hii itakapotamka vinginevyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, naomba Bunge lako Tukufu, liujadili Muswada huu na hatimaye likubali kuupitisha kuwa Sheria. Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono, sasa nitaomba Mjumbe wa Kamati iliyohusika kuujadili Muswada huu, aje awasilishe maoni ya Kamati. Maana yake nini; Mheshimiwa Mwenegoha, mbona unakaa mbali?

**MHE. HAMZA A. MWENEGOHA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruhusa yako, naomba sasa niwasilishe maoni ya Kamati ya Fedha na Uchumi, kuhusu Muswada wa Sheria wa Ukaguzi wa Hesabu za Umma wa mwaka 2008 *(The Public Audit Bill, 2008).*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa ya kutoa maoni ya Kamati yangu, juu ya Muswada wa Sheria hii, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 86(5), Toleo la Mwaka 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 84(1), uliipatia Kamati yangu jukumu la kupitia na kuuchambua Muswada huu wa Sheria na hatimaye kutoa maoni na mapendekezo kwa Serikali, juu ya Muswada huu. Ninapenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Kamati imetekeleza jukumu hilo na hatimaye Muswada huu kuletwa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hatua za kuchambua na kupitia Muswada wa Sheria ya Ukaguzi wa Hesabu za Umma (*The Public Audit Bill, 2008),* Kamati ilishirikiana vyema na wadau mbalimbali wa Ukaguzi, Wizara ya Fedha, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Wanasheria kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, wote kwa pamoja walitusaidia sana katika kupata uelewa na ufafanuzi na majibu ya hoja mbalimbali za Wabunge katika kuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taaluma ya Ukaguzi inakuwa siku hadi siku. Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imekuwa ikifanya jitihada katika utendaji wake wa kazi ili kuweza kufikia vigezo vinavyokubalika Kimataifa katika Sekta ya Ukaguzi, hivi sasa ofisi hiyo ipo katika hatua ya kwanza, ambayo ni ya chini kabisa kwa vigezo vya Shirikisho la Asasi Kuu la Ukaguzi wa Hesabu za Umma *(International Organization Supreme Audit Institution – INTOSAI)*, pamoja na Shirikisho la Asasi za Ukaguzi wa Hesabu za Umma katika Nchi za Afrika zinazozungumza Lugha ya Kiingereza *(African Organization Supreme Audit Institution - AFROSAI*), ambazo Tanzania ni Mwanachama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wanachama katika Asasi hizi, wanatakiwa kuwa na sheria inayojitegemea kuhusu Ukaguzi wa Hesabu za Umma; kuanzishwa kwa Sheria hii kutaiwezesha Tanzania kusogea hatua kadhaa mbele na hivyo kuisogeza karibu na viwango vya juu vya Kimataifa vya Ukaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu umekuja wakati Muafaka, hasa ikizingatiwa kuwa sasa Tanzania ni moja ya Nchi zinazounda Jumuiya ya Afrika Mashariki. Katika Jumuiya hii, Nchi Wanachama zimeanzisha Umoja wa Forodha na baadaye zitakuwa na soko la pamoja na sarafu moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hali kama hii ni vyema Tanzania ikajiweka sawa katika maeneo ambayo ipo nyuma na hasa katika taratibu za kifedha. Kenya na Uganda tayari wanazo Sheria zinazojitegemea kuhusu Ukaguzi wa Hesabu za Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria hii pia inalenga kutambua Mamlaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, kama ilivyoainishwa katika Katiba. Hata hivyo, si nia ya Muswada huu kuleta Mabadiliko katika kipengele chochote cha Katiba hivi sasa. Hii ni kwa sababu, mbadiliko yatawezekana tu pale ambapo Ofisi ya Mkaguzi Mkuu itafikia hatua ya tano ya Viwango vya Kimataifa kiutendaji, kwani hivi sasa ipo katika kiwango cha kwanza na tathmini ijayo ya kujua kiwango kinachofikiwa na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Tanzania Kimataifa, itafanyika mwaka 2009 mwishoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri wa Kamati ni kwamba, katika kukamilisha kazi uliyoitoa kwa Kamati hii, kwa mujibu wa Kanuni ya 84(1) ya mwaka 2007 na kwa mujibu wa Kanuni ya 84(2), Kamati yangu iliungana na Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa (*LAAC*), Kamati ya Hesabu za Serikali (*PAC*) na wadau wengine wa Ukaguzi toka sehemu mbalimbali ili kupata maoni juu ya kuborsha Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni mbalimbali yaliyotolewa yaliisaidia sana Kamati katika kufanya kazi yake. Nafurahi kukufahamisha kuwa, Serikali ilikubali mapendekezo yote muhimu yaliyotolewa na Kamati na kufanyiwa Kazi katika Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Sheria hii mpya, Serikali imepanua wigo wa Ukaguzi ili kuendana na hali halisi ya Dunia ya sasa. Sheria hii inatamkwa kuanza rasmi kwa ukaguzi wa mazingira *(Environmental Audit)* na ukaguzi wa utambuzi ili kuweza kudhibiti vyema matumizi ya fedha za umma. Kamati inaipongeza sana Serikali katika

hili, kwa kuwa sasa hata zile fedha ambazo zitatumika katika hali tatanishi, uwezekano wa kujua nyendo zake utakuwa mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na unyeti, ugumu na umuhimu wa kazi za Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Kamati imeona kuna umuhimu wa Serikali kuangalia uwezekano wa kuboresha mazingira ya kazi kwa Watumishi wa Ofisi hii, hasa kimaslahi ili kuweza kuwabakisha katika Ofisi hii vinginevyo, wataalamu wa fani hii wataendelea kukimbilia katika asasi binafsi za ukaguzi, zinazolipa vizuri na hivyo kuikosesha Ofisi nguvu kazi ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuandaa Kanuni zinazoendana na Sheria hii mpya, Kanuni hizo ziwe na kifungu kinachomtaka Mlipaji Mkuu wa Serikali na Maafisa Masuhuli, kutoa taarifa ya utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati zinazosimamia fedha za umma; (*PAC*), (*POC*) na (*LAAC*), baada ya mapendekezo ya Kamati hizo kukubaliwa na Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hitimisho, Kamati inapenda kumshukuru Waziri wa Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Mustafa Mkulo, Naibu Mawaziri wa Fedha na Uchumi; Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee na Mheshimiwa Jeremiah Sumari, pamoja na Wataalamu wao, kwa umahiri wao katika kuwasilisha Muswada vizuri kwa Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kamati inamshukuru sana Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Watendaji wake, kwa ufafanuzi wa masuala mbalimbali ya Kikaguzi yaliyojitokeza wakati wa Mjadala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pia inawashukuru sana, Maofisa kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, wakiongozwa na Mwandishi Mkuu wa Sheria, Ndugu Kasmil Kiuki, kwa kuwezesha Muswada huu kueleweka kwa Wajumbe wa Kamati yangu na kwa kutoa ufafanuzi wa Kisheria katika masuala mbalimbali, hatimaye kutuwezesha kuujadili na kuutolea maoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nawashukuru wadau wote walioitikia wito, kwa kutoa maoni kwa Kamati hii, juu ya Muswada huu. Kwa namna ya pekee kabisa, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi, ambao wameweza kutoa maoni na michango ya mawazo yao mbalimbali katika kuboresha Muswada huu ili hatimaye uletwe mbele ya Bunge hili Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie nafasi hii, kuwatambua Wajumbe wote kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Dr. Abdallah O. Kigoda - Mwenyekiti, Mheshimiwa Hamza A. Mwenegoha - Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Fatma Abdulhabib Fereji, Mheshimiwa Josephine J. Genzabuke, Mheshimiwa Athumani S. Janguo, Mheshimiwa Siraju J. Kaboyonga, Mheshimiwa Eustace O. Katagira, Mheshimiwa Devota M. Likokola, Mheshimiwa Clemence B. Lyamba, Mheshimiwa Anna M. Komu,

Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Dr. Binilith S. Mahenge, Mheshimiwa Monica N. Mbega, Mheshimiwa Felix C. Mrema, Mheshimiwa Anthony M. Diallo, Mheshimiwa Mossy S. Mussa, Mheshimiwa Damas P. Nakei, Mheshimiwa Richard M. Ndassa, Mheshimiwa Dr. Omari M. Nibuka, Mheshimiwa Sijapata F. Nkayamba, Mheshimiwa Martha J. Umbulla, Mheshimiwa Suleiman A. Saddiq, Mheshimiwa Elizabeth N. Batenga na Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kutoa shukrani kwa Kaimu Katibu wa Bunge, Dr. Thomas Kashililah, pamoja na Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge, kwa kuwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake. Aidha, napenda kuwashukuru Ndugu Anselem Mrema na Ndugu Michael Chikokoto, Makatibu wa Kamati hii, kwani sote kwa pamoja tumeweza kukamilisha maandalizi ya Muswada huu wa Ukaguzi wa Hesabu za Umma *(The Public Audit Bill, 2008*) kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. FATMA ABDULHABIB FEREJI (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya yote, naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipa afya njema na kuweza kuwa hapa katika Bunge la Kumi na Mbili la Bajeti ya Mwaka 2008/2009, ili niweze kumwakilisha Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani ambaye pia ni Msemaji Mkuu wa Wizara ya Fedha na Uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, natoa shukrani zangu kwako binafsi, kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani, kuhusu Muswada wa Sheria ya Ukaguzi wa Hesabu za Umma *(The Public Audit Bill, 2008)*, kwa mujibu wa Kanuni ya 53(6) (c) na kifungu kidogo cha 86(6), Toleo la 2007 la Kanuni za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, madhumuni makubwa ya Muswada huu, ulitakiwa ukidhi mambo makubwa matatu ambayo ni kama ifuatavyo:-

(1) Ni kutekeleza matakwa ya Katiba ya kutambua kuwa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali imeanzishwa na Katiba na hivyo kuna umuhimu wa kuwa na Sheria yake.

(2) Ukaguzi wa Umma unakidhi matakwa ya Viwango vya Kimataifa vya *INTOSAI* na *AFROSAI-E*, ambavyo vinataka wanachama wake kuwa na Sheria zao wenyewe za ukaguzi ili kuwa na utendaji mzuri, yaani *best practices*.

(3) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, kuwajibika kwa Bunge badala ya Rais kama ilivyo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mambo hayo matatu makubwa, ambayo ndani yake yamo mambo ya uteuzi wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu kuthibitishwa na Bunge, kuwa na bajeti inayojitegemea, kuwa na uwezo wa kuajiri na kufukuza katika Muswada

huu hayamo; hivyo, bado Muswada huu haujafikia hata hatua ya pili ya matakwa ya Kimataifa, kwa sababu Serikali imekataa kufanya mabadiliko ya Katiba ili yaendane na Sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani kwa takriban miaka karibu sita sasa, tumekuwa tukiitaka Serikali, ilete Sheria ya kuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, awe na taasisi iliyo huru katika utendaji wake wa kazi, lakini Serikali kwa sababu wanazozijua wao, wamekataa kwa kudai kuwa hiyo inahitaji marekebisho ya Katiba ambayo eti yanahitaji mlolongo mrefu wa kupata mabadiliko hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho mengi ya Katiba yamefanyika pale tu ambapo Serikali imeona kuna kuondolewa kwa maslahi yake. Kwa mfano, mabadiliko ya 13 ya Katiba ya Kumwondoa Rais wa Zanzibar kuwa Makamu wa Rais na leo kuwa Waziri asiyekuwa na Wizara Maalum katika Serikali ya Muungano, hakukuwa na kikwazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi inaamini kuwa, suala hili la kubadili Katiba, halihitaji mchakato mrefu kama ambavyo Serikali inadai, kwani utaratibu wa mabadiliko ya Katiba ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mabadiliko ya Katiba ni sawa na Sheria nyingine, isipokuwa kupitishwa kwake kunahitaji wingi maalumu.

(a) Kwanza, kwa masuala ya Muungano kunahitaji theluthi mbili ya Wabunge kutoka Zanzibar na theluthi mbili ya Wabunge kutoka Tanzania Bara. Pili ni kwamba, kwa masuala yasiyo ya Muungano, huhitaji theluthi mbili ya Wabunge wote.

(b) Kuandaa Waraka, yaani *White Paper* kwenda kwenye Baraza la Mawaziri; na

(c) Baraza la Mawaziri Kuandaa Waraka kwenda kwenye Bunge. Bunge kupitia Kamati inayohusika, inafanya taratibu zake za kawaida na kisha linajadili, ikishapitishwa na theluthi mbili ya Wabunge wote, tayari mabadiliko ya Katiba yamekuwa yameidhinishwa rasmi.

Kambi ya Upinzani inaamini kabisa kuwa, kama kweli Serikali ilikuwa na nia hasa ya kuifanya Ofisi hii ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwa Taasisi Huru na hivyo kuifanya iweze kutimiza majukumu yake kwa ufanisi, basi ingewezekana kufanya mabadiliko ya vifungu vilivyotakiwa ndani ya Katiba ili kuruhusu uhuru wa Ofisi ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali, kama ilivyo kwa Nchi Wanachama wa *INTOSAI* na *AFROSAI.*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza na uchambuzi wa Muswada huu; kwanza kabisa, kuna maneno yaliyotumika katika Muswada huu ambayo hayakufafanuliwa au kuelezwa ipasavyo nayo ni *policy of the highest thrift,* kama yalivyotumika katika

kifungu cha 11(2(d). Kambi ya Upinzani, inataka ipatiwe ufafanuzi juu ya maana halisi ya maneno hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 11(1)(e) cha Muswada huu, kinampa nguvu Mkaguzi Mkuu katika kutekeleza kazi na majukumu yake yaliyowekwa na sheria hii, kupokea maoni ya kitaalamu, ushauri wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali au mtu yeyote mwenye ujuzi wa Kitaalamu katika mambo ya Kisheria, Uhasibu, Ukaguzi wa Hesabu au jambo lolote lile. Wakati huo huo, kifungu cha 16 kinampa nguvu ya kumwita mtalaam au mtu mwingine mwenye ujuzi katika kutekeleza majukumu yake, hapa hakuna haja ya kuwa na kifungu cha 16 kinachojitegemea, bali kingeweza kuingizwa kama sehemu tu katika kifungu cha 11.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 15(6)(a) ni vyema kuondoa neno "*advise*" na kuweka neno "n*otify:* au "g*ive notice*" na kwa hivyo, hiyo Ibara isomeke *"notify the person in writing of the nature of the information or give notice on the nature of the information."*

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 18(1) kinachompa nguvu ya kuchagua *Auditing Standards,* kitakuwa knapingana na kuingilia nguvu ya *NBAA* ambayo kwa Tanzania ndiyo imepewa jukumu la kuchagua *standards* hizo, hivyo *harmonization* katika Sheria na Mamlaka mbili hizi ifanyike.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 25(1) cha Muswada huu, hakionyeshi majukumu *(obligations),* bali kinatoa haja ya kuwa na taaluma na ujuzi wa kitaalam. Hivyo basi, Kambi ya Upinzani inapendekeza kifungu kipya cha 25(1)(a) kisomeke kama ifuatavyo: "*The Officers of the National Audit Office in handling Audit Matters shall utilize reasonably their professional knowledge and skills with the Audit work they engage in.*" Vifungu vya (2), (3) na (4) vibaki kama vilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 36 cha Muswada huu, kikisomwa pamoja na Ibara ya 143(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuna mgongano kidogo katika vifungu hivi viwili. Ibara ya 143(4) inasema, Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atawasilisha kila ripoti aliyoiandaa kwa mujibu wa Ibara ndogo ya (2) katika Katiba hii kwa Rais na Rais baada ya kuipokea, atamwamuru mtu anayehusika kuiwasilisha ripoti hiyo Bungeni na ni pale tu Rais akishindwa kuchukua hatua za kuiwasilisha taarifa hiyo Bungeni, basi Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu atawasilisha taarifa hiyo kwa Spika wa Bunge, ambaye ataiwasilisha taarifa hiyo Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, ataiwasilisha ripoti hiyo kwa Spika wa Bunge au Naibu Spika, iwapo nafasi ya Spika ipo wazi au hawezi kutekeleza majukumu yake, ambaye ataiwasilisha ripoti hiyo Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma ibara ndogo hiyo ya 143(2)(a), (b) na (c), kimantiki inajumuisha ripoti zote; ziwe maalumu au za mwaka, kwani akitekeleza

majukumu yake chini ya ibara ndogo ya 2(b) na (c), anaweza kuona jambo ambalo lingepaswa kuletwa katika *attention* ya Bunge ikawa ndiyo *special report*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyotolewa na kifungu cha 36(1) cha Muswada huu na kifungu kidogo cha 36(3); kuitambua ibara ya 143 ya Katiba, hivyo vifungu viangaliwe kwa kuweka mfumo bora wa uwasilishaji wa ripoti ya Mkaguzi wa Hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ibara ndogo ya 4 ya Katiba, inampa nguvu Rais kupokea na kuamuru kuwasilishwa kwa Ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu Bungeni, wakati huo huo vifungu vya 34(2) na 35 vinatoa nguvu kwa Waziri kuwasilisha Ripoti Bungeni na siyo kwa kufuata *directions* za Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaona hapa kuna haja kubwa ya kubadili Katiba, kwa kuwa Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali anapofanya Ukaguzi wake katika Wizara ya Fedha, maana yake anamkagua Waziri wa Fedha au Serikali, hivyo kwa maneno mengine anayekaguliwa ni Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo la kustajaabisha anayekaguliwa halafu yule yule apewe taarifa hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 42(1), kinaeleza kuhusu vyanzo vya mapato vya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi. Katika ibara ndogo ya 42(1)(c), inaeleza miongoni mwao itakuwa ni fedha kutokana na mapato ya uwekezaji, yaani *income from investment*, lakini uwekezaji huu ambapo mapato hayo yatatoka na kuwa sehemu ya Mfuko wa Ofisi hii, hayakuonyeshwa wazi itakuwaje; hivyo, kipengele hiki bado kina utata na kinahitaji maelezo ya kutosha kuhusu namna ambavyo ofisi hii itapata *income from investment*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 47(1), kinatoa ushiriki wa *Public Accounts Committee* kama taasisi pia ya kutekeleza sheria hii. Hivyo ni wazi kuwa, taasisi za msingi katika Sheria hii ni *National Audit Office* na *Public Accounts Committee*, Kambi ya Upinzani inaona tatizo la msingi ni kuwa *Public Accounts Committee* haikutajwa na kuonyeshwa katika sehemu nyingine yoyote ya Muswada huu, kwa mfano, katika tafsiri kama moja ya Taasisi ndani ya Sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, inakubali kuupitisha Muswada huu kwa sababu tu kwamba, hatua ya kwanza ya kuwa na Sheria inayojitegemea ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu imepatikana na Kamati zetu za Bunge za *oversight* zitapata kutambuliwa na kufanya kazi zake kwa mujibu wa Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kambi ya Upinzani inaamini kuwa, Serikali sasa itaona umuhimu wa kuidurusu upya Katiba yetu ili yale maeneo yanayohitaji mabadiliko kama Kambi ya Upinzani kutokutajwa ndani ya Katiba; kuthibitishwa kwa Viongozi mbalimbali ndani ya Bunge na kadhalika ili mara baada ya Bunge la Bajeti kumalizika, mchakato huo uanze.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, kwa heshima kubwa naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru. Tunao wachangiaji kama kumi, kwa kuanza nitamwita Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali, Mheshimiwa John Momose Cheyo.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa fursa ya kuanza mjadala huu wa Muswada huu wa *Public Audit Office.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nataka kutumia nafasi hii, kuwatakia wakulima wangu wa pamba, mwanzo mzuri wa msimu na ninatumaini Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, atahakikisha kwamba, bei itakuwa zaidi ya shilingi 500.

Jambo la pili, nataka kutumia nafasi hii kushukuru sana kwamba, angalau Serikali sasa imetimiza ahadi yake ya muda mrefu. Pia nashukuru kwa kazi nzuri ambayo imefanywa kwa kushirikiana na Kamati ya Fedha, Kamati ya Mashirika ya Umma na Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa katika kujadili Muswada huu na kutoa maoni juu ya Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa leo nataka kukazia mambo machache; jambo la kwanza ni kweli kazi nyingi ambazo tunaziona za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali ni kuangalia Hesabu ambazo tayari zimeshafanyika *(Postmortem Work).* Kazi ambayo tunaiangalia ni je, alikufa namna gani tunapasua tunacheki, lakini kama ni fedha imekwenda, kama ni matumizi mabaya yameshatendeka, kama ni kazi mbovu imeshafanyika; kwa hiyo, kwa upande mmoja inasadia lakini kikubwa zaidi tuimarishe Ofisi hii kuhakikisha kwamba, inakuwa chanzo cha kuzuia maovu. *Prevention is better than cure*, siyo watu wameshamaliza mambo yao halafu ninyi mnaanza kupekua mabuku na mara nyingine ni miaka miwili, mitatu, haiwezi ikasaidia maamuzi muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika nchi yetu, kuna mambo mengi ambayo yanapaswa kuzuiwa. Nimefurahishwa sana, kwa sababu kwenye *article 12* ya Muswada huu, inazungumzia juu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, kuweza kutoa maoni na ushauri juu ya matumizi mbalimbali hata ya mali za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mali ya Serikali ni pana zaidi ya fedha za Serikali. Mali ya umma ni pamoja na ardhi ya umma, mashirika mbalimbali, madini; kwa hiyo, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, aimarishwe sana afanye kazi hii iliyopo katika *article* 12 ili aweze kuzuia maovu.

Mheshimiwa Naibu Spika, maovu yapo mengi tu ambayo yameshatupata katika Taifa hili. Mimi sijui kwa nini tumepoteza fedha nyingi sana katika mikataba mbalimbali ya Madini?

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, angeweza kuangalia mikataba hiyo ya Madini, akaieleza Serikali kwamba kwa njia hii mnayoenda mtapoteza fedha nyingi katika sekta ya Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo jambo halikufanyika, pamoja na kwamba, Serikali imeondoa *additional allowance on unredeemed expenditures*, lakini tayari madhara makubwa yamefanyika, si ajabu kutakuwa na migodi ambayo itaweza kumaliza shughuli zake bila hata kulipa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, maamuzi kama haya, yangeweza kwenda kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali akatusaidia; tumemaliza Madini tunachoona sasa hivi nchi hii imevamiwa katika sekta ya wanyamapori, sasa hivi ningemshauri Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali aingilie kati suala hili mapema, kwa sababu tunaanza kuona kwa mfano, Serengeti imeanza kugawanywa katika visehemu vidogovidogo, ambavyo watu wanaviita *private land.*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi mwenyewe nimeshuhudia. Tumeenda Mugumu nia yetu katika kuangalia sehemu hizo za wanyama ilikuwa ni kuona je tunapata pesa ya kutosha kutokana na uwekezaji katika mbuga zetu za wanyama, lakini katika Hoteli ya *VIP* Kamati yako ya Hesabu za Serikali ilikatazwa kuingia!

Umeona wapi Tanzania hii, tunakuwa na sehemu ambapo watu wanaanza kujikatia Kitanzania chao wenyewe?

Sisi tulitaka kwenda kuangalia pale kwa sababu kuna mambo mengi yanayosemwa; kwanza, tunaambiwa kuwa yule mwekezaji ameweka malambo makubwa na wanyama wanapokwenda pale wanachomwa sindano na wanapelekwa Marekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeambiwa huyu Mwekezaji anataka sehemu yote iwe mali yake na Barabara igeuzwe ipitie Loliondo ifike Musoma; haya maamuzi kwa nini yasiwe *subjected* kwa *Controller and Auditor General,* ayaangalie kama kweli ni maamuzi endelevu?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaambiwa Ngorongoro sasa hivi kuna *lobby* kubwa sana na hili ningependa kuiambia Serikali, mjaribu kumsaidia Rais; kama Rais kila wakati atakuwa *subjected* kwa washawishi wengi wa Kimataifa katika kugawanya mali ya Serikali kama vile Ngorongoro na Serengeti, tutamaliza Marais wetu.

Kila Rais atakayekuwa anamaliza awamu yake, atakuwa na majina ya kila aina; kama vile ambavyo sasa tumeanza kuona. Nawaomba mnaoisaidia Serikali, msaidieni Rais kwa upande huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka kukazia jambo hili ni muhimu sana, tuimarishe Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali ili kuhakikisha kwamba, anafanya kazi zaidi ya kuangalia vitu ambavyo vimepita

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni kwamba, nimeangalia Sheria hii *part one*, inazungumzia juu ya kuanza wakati ambapo Mheshimiwa Waziri atakapotoa taarifa kwenye Gazeti la Serikali, lakini haina muda.

Kwa hiyo, Sheria hii haimlazimishi Mheshimiwa Waziri, kutoa habari au uamuzi kwamba Sheria hii ianze mwaka huu ama miaka miwili ijayo na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili si kwamba nalitengeneza, sasa hivi una habari kuwa tunazungumzia juu ya *National Assembly Administration Bill*.

Tumetunga Sheria ya *National Assembly Fund*, haijatengenezewa *regulations*, kwa hiyo, Sheria imekaa pale lakini haiisaidii Bunge. Nimeona hapa kwenye *article* namba 50, kwa mfano, kuna *regulations* za kufanyika; je, zitafanyika lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona kwamba, kuna *National Audit Fund;* je, hii itakuwa na utaratibu gani na itamalizika lini?

Ningeshauri kwamba, tunapotunga Sheria tuwe pia na *timeframe*, siyo tunatunga Sheria inaendelea ku-*hang* tu; kama Sheria haiwezi kufanyika katika mwaka huo ambao inatungwa, Sheria hiyo inakuwa haina maana yoyote wala haiisaidii Taifa hili.

Kwa hiyo, ningehimiza kwamba sheria hii basi ianze mara moja. Sisi tungependa kujivuna sisi kama *Public Accounts Committee* pia tuna mashirika mbalimbali ambayo tunashirikiana na Kimataifa na hii imekuwa ni mojawapo ya kikwazo kila tukienda tunauliza je, ninyi mna *Public Audit Act* inayofanya kazi, tunasema hakuna. Kwa hiyo, hii ikianza mapema itakuwa imetuondolea adha hiyo.

Jambo ambalo limesisitizwa vizuri la upande wa upinzani nalo ni juu ya *reporting*. Ni kweli kwamba *article 143 Sub Section 4* ya Katiba inaweka utaratibu ulio wazi kabisa kwamba ripoti zote za *Controller And Auditor General* mwisho wake ni Bunge. Hii imewekewa uzito zaidi na article 10 ya Muswada huu kwamba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali anafanyakazi kwa niaba ya Bunge.

Kwa hiyo, jambo hili ningeshauri kwamba lisipindishwe. Tumeona kwa mfano katika ripoti ya *EPA* kama hiyo ripoti ya *EPA* imefanywa na *Controller and Auditor General* ripoti hiyo lazima ije katika Bunge lako, hatuwezi tukasema kwamba eti hii ni *special audit*. Haya mambo ndiyo nimeshukuru kwamba katika Muswada huu

umezungumzia *a special audit* katika *section* 38 na kama hivyo. Yenyewe imeambiwa kwamba itafuta utaratibu kama ule ambao umezungumzwa katika Katiba Ibara ya *143 sub section 4.*

Kwa hiyo, kama ni hiyo naomba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu aachiwe afanye kazi yake kwa niaba ya Bunge. Kama anatengeneza ripoti, ripoti zote, siyo tu ripoti ya hesabu za mwaka *any report*. Ripoti yoyote ambayo inayofanya sasa hivi umetuambia uwigo umepanuka, kuna *forensic*, kuna mambo ya *performance audit* na *any other audit* na kuna *special audit* basi yote haya yasifike tena kwa *administration* yaje Bungeni. Hilo jambo ningependa kusisitiza.

Jambo la mwisho ambalo ningependa kuzungumzia inahusu adhabu, adhabu kwa maafisa masuuli. Nimeona katika Sub Section 4 Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali ataripoti lakini baada ya wewe kupeleka taarifa pamekuwa na hiki na hiki ni kitu gani, meno yako wapi, nilitegemea kwamba katika Muswada huu pangekuja na meno makubwa sana ya kuwawajibisha watu ambao hawafuati utaratibu wa kihasibu ambazo wanapoteza mali ya umma.

Mwisho kabisa nataka kusema huu ni mwanzo mzuri najua bado kuna mapungufu mawili, matatu lakini naona Bunge sasa tumetimiza shabaha yetu ya kuweza kumsaidia Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kufanyakazi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono kwa dhati kabisa Muswada huu ili uweze kupitishwa na Bunge hili. Nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na mimi kunipa nafasi niweze kuchangia Muswada wetu. Kwanza na mimi kama mwenzangu aliyenitangulia nishukuru kwa dhati kabisa Muswada huu umeletwa na Kamati zetu na hasa Kamati yetu ya *LAAC* ambayo huko nyuma haikuwa imetajwa kwenye sheria sasa kwa mara imetajwa kwa hiyo, tunapata silaha nzuri ya kufanyakazi. Nashukuru sana kwa hilo. La pili ninashukuru pia kwamba hii Serikali imetaja ni hatua ya kwanza kuimarisha Ofisi ya *CAG*. Mimi ninaamini kabisa pamoja na wenzangu kwenye Kamati kwamba Ofisi ya *CAG* inapokuwa imara na usimamizi wa mali nyingi za umma, fedha za umma pia utaimarika sana. Sasa baada ya kusema hayo niseme mawili, matatu kwanza ya vifungu halafu niseme mengine ya jumla. Nitasema kwa haraka kidogo ili nipate muda wa kusema haya mengine.

Katika kifungu cha 1 (2) mimi ningelipenda Mheshimiwa Waziri afafanue zaidi na aweze kuonyesha wazi haya anayoita *relevant professional qualifications*, ni muhimu sana tunapoingia kwenye Ofisi nyeti kama hii bila kuwa na *relevant professional qualifications* kuelezwa huko mbele nina hakika tunaweza kuwa na tatizo. Kwenye ukurasa wa 10 kifungu cha 9 mimi nimesikitishwa pamoja na kwamba ninaelewa mantiki ya kuondoa lile neno linalosema *and their accounting officers*. Mimi ningependa sana hiki kifungu kirudi kwa sababu ukipitia taarifa zote za CAG unachogundua ni kwamba

kuna mambo yanayofanywa na *accounting officer* ambaye anasababisha kwa kiwango kikubwa taarifa isiwe sahihi.

Sasa ukiwaondoa hawa, hoja yenyewe ni kwamba *responsible for examine inquiring into to auditing and reporting on the accounts of all ministries independent partners of government agencies and their accounting officers* kwa maana ya kwamba na *accounting officers* kama utendaji wao ni mbovu *CAG* naye anatakiwa kuwa-*report*. Sasa usipowaripoti unawapata wapi wale ambao wamesababisha mambo hayo. Kwa hiyo, mimi ningesisitiza sana hiki kipengele kirudi. Ni bahati mbaya sana sisi tulitakiwa kuwemo wakati Muswada huu unajadiliwa, lakini bahati mbaya pia kuwa tulipewa majukumu mengine na Ofisi yako Naibu Spika, kwa hiyo hoja yetu hatukuweza kuitetea kule ndani. Lakini tungependa hilo lisiondoke.

Katika ukurasa wa 14 linapozungumziwa kifungu cha 15 (3) nina furaha kwamba *internal auditor* ameambiwa *shall submit copies of internal audit report, shall submit* kwa hiyo, si hiari. Nafurahi na hilo lakini ningependa kuona anawekewa muda maalum. Labda tangu amewasilisha ripoti yake kwa a*ccounting officer* wake, basi *within three weeks* aweze kuwasilisha kwa yule wa juu. Ili tuachane na hiki alichosema Mheshimiwa Cheyo, sisi sasa hivi tunafanyakazi ya postmortem tunapasua mauti ambaye amekufa labda mwaka mmoja uliopita. Sasa hii kazi ili tuondoke ni lazima tudhibiti mapema na *internal auditor* ni moja wa watu ambao wanatusaidia sana kudhibiti mapema na *CAG* akiyapata mapema anaweza kufanya *intervention* kuokoa upotevu wa mali ya umma. Kwa hiyo, ningependa hapo awekewe muda maalum.

Vile vile ningependa katika kifungu cha 19 (4) watu wote katika kifungu 2 a, b, c, d na hata cha tatu wameambiwa wakifanya uzembe watalipa faini, lakini watendaji wa Serikali wamesamehewa. Sasa mimi ninaona kwamba ukitazama ripoti za *CAG* hata Halmashauri zetu kwa mfano moja ya watu ambao wanasababisha hati chafu ni watendaji. Sasa ukisamehe hawa watu wasilipe fees kwa kweli una-*encourage* uzembe.

Mimi ningeomba fee ziwepo wale wahusike walipe siyo Serikali ilipe. Lakini mhusika kwa kiwango cha uzembe wake yeye mwenyewe. Ningelifikiri vile vile katika ukurasa wa 27 lile suala la any person *convicted of an offence under this act*. Hii *one million shilling audit imprisonment for term not acceding two years* mimi nafikiri hii hela ni kidogo sana, inapaswa kuangaliwa upya ili tuwe na kiwango ambacho ni *deterrent* kwa watu ambao wanasababisha mambo hayo. Sasa hayo nadhani niyaachie hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kuhusu marekebisho hatua ya pili. Mimi ningependa kuona Ofisi ya *CAG* inaimarishwa kwa kiwango kikubwa sana. Ninataka kusema hivyo kwa sababu gani, nataka nitumie mfano, nisamehe kama nitatumia mfano, *CAG* anapokuwa chini ya mwingine anapokuwa chini ya Serikali na siyo chini ya Bunge na hii ina maana ya kwamba ripoti ya *CAG* wala si lazima iende Bungeni, kwa sababu *CAG* anaisaidia Bunge kusimamia Serikali, sasa unapopeleka tena kwa Rais huyo huyo ambaye ndiyo mkuu wa Serikali hupati usimamizi ulio imara. Kwa hiyo, nataka nitoe mfano, kwa mfano katika taarifa ya *BoT* tena kipindi hicho hicho chenye mgogoro

mkubwa cha mwaka 2005/2006 kwenye kitabu hiki kizuri kikubwa kilichofungwa vizuri sana kinapendeza. Ukurasa wa (iv) kuna taarifa iliwasilishwa kwa Waziri wa Fedha Septemba, 29 mwaka 2006.

Lakini kwenye kitabu hicho hicho kwenye ukurasa wa 100 kwanza nirudie ile tarehe Septemba, 29 mwaka 2006 kwenye kitabu hicho hicho ukurasa wa 100 kuna saini ya ndugu yangu na ninamheshimu sana Ludovick S. L. Utoah *Controller and Auditor General* ya Juni 2007. Sasa mtaniambia Waheshimiwa Wabunge, ni muujiza gani taarifa ya 2007 inaingia ndani ya kitabu kilichowasilishwa kwa Waziri Septemba, 2006? Huu ni muujiza. Huu muujiza ingekuwa mambo ya Kikatoliki ningesema na naomba Wakatoliki wanisamehe ni sawa na mimba ya bikira Maria iliyotoka kwa roho Mtakatifu. Kitabu kimefungwa, kimechapwa kikamilifu inakwenda kupelekwa kwa Waziri tarehe 29 Septemba, ndani yake kuna ripoti ya 2007. Sasa kilirudishwa nyuma kikafumuliwa ikiingizwa ripoti ya CAG au ikafanyika nini? (*Makofi*)

Sasa mimi naelewa kilichotokea hapa na hiki ni kosa la jinai kwa sababu kuna *forgery* hapa ndani. *Forgery* ni kosa zito sasa Wabunge tumegawiwa kitabu hiki sijui kama tuliona, kwa bahati mbaya tunawekewa vitabu vingine wala hata hatuvioni. Sasa hapa kilichotokea ni aidha walitaka ku-*meet* ile *deadline statutory* ya kisheria inayotaka ndani ya miezi mitatu taarifa iwe imewasilisha. Hawakui-*meet* na nasema hivyo kwa ushahidi, kwa sababu tarehe 21 taarifa ya audit haikuwa tayari, mimi nina-*draft* yake. Nina-*draft report* ya Desemba 21 mwaka 2006. Sasa iliingiaje hapa? Kamati ya Bunge imepelekewa tarehe 14 Julai, 2007 sasa hii iliyowasilishwa kwa Waziri wa Fedha ni kitu gani? Hayo ni mambo mazito ambayo hatuwezi kuyaachia. Wabunge ni lazima tuwe wakali kwa vitendo vya aina hii. (*Makofi*)

Humu ndani kuna taarifa ya Mwenyekiti wa Bodi wa BoT 2007 iliingiaje? Haya yanawezekana kwa sababu *CAG* hayuko peke yake, hayuko huru, yuko chini ya Waziri na Waziri ndiye anayewasilisha hiyo taarifa. Kwa hiyo, chochote kilichoweza kufanyika hatujui kimefanyikia wapi. Kwa hiyo, tukipata *independence* ya *CAG* hawajibiki chini ya mtu mwingine kama Katiba inavyogusia kusema. Lakini baadaye haisisitizi sana. Kama Katiba hii ikiimarishwa tutapata *CAG* ambaye ni jicho la Bunge na atasimamia kwa uwazi kabisa fedha na rasilimali za Taifa hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hili halihitaji kuelezwa zaidi kwa sababu kitabu hiki ni shahidi nadhani kila mmoja anaweza kulitazama Wabunge, Wabunge wote waligawiwa, kila atazame jinsi tunavyohitaji marekebisho makubwa ya Katiba. Mara nyingi tunapozungumzia marekebisho ya Katiba watu wanafikiri ni agenda ya Upinzani. Lakini unapofika kitu kikubwa namna hii kinafanyika kinaletwa Bungeni Wabunge, mnakipitisha mimi nadhani tuna tatizo kubwa sana na ndiyo maana narudia hoja iliyotolewa na Kambi ya Upinzani kwamba marekebisho ya Katiba yafanyike mara moja kuimarisha ofisi hii.

Nashukuru Waziri alitamka hapa kwamba hata kule kwenye mikutano ya kimataifa tulipewa ripoti kwamba sisi ni wa mwisho katika *international standard.* Sasa hatutegemei tena tuendelee nchi yetu tuambiwe kwamba sisi ni wa mwisho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, niligusia tu hili alilosema Mheshimiwa Cheyo. Mheshimiwa Cheyo ametupa kitu ambacho kama tuko makini ni lazima wote tuone uchungu. Hivi Kamati ya Bunge ambayo inadhaniwa kufanyakazi kwa niaba ya Bunge zima, ina mamlaka ya Bunge kwa mujibu wa sheria namba 3 ya mwaka 1988 inakwenda kutembelea mahali, inakwenda kukagua rasilimali za nchi hii inakataliwa na mtu anayejiita mwekezaji katika nchi hii. Ni wapi duniani hata alikotoka huyo mwekezaji na kama ni huyo wa *VIP* nafikiri anatokea Marekani, ni wapi duniani na ni katika hali ipi kule Marekani *Congress* inaunda Kamati au Kamati ya Kudumu ya *Congress* inatembelea mahali au inamuita mtu anasema sitaki kuongea na nyie. Hili ni tusi kwa taifa hili na hatuwezi Watanzania kuendelea kutukanwa katika nchi yetu na rasilimali zetu. (*Makofi*)

Hakuna nchi yoyote mimi nimetembelea bahati nzuri nchi hizi zote hakuna hata moja ambayo sijatembelea. Nimetembelea Marekani, nimeishia Ulaya, ninafahamu huko Ulaya wanavyotu-*treat* sisi na hata wawekezaji wanavyokuwa *treated*. Sheria yao ni kitu cha kwanza ni lazima nchi yao iheshimiwe. Lakini Watanzania unaambiwa hatuzungumzi na nyie, sasa wanazungumza na nani? Naomba Waziri atusaidie wanazungumza na nani baadaye katika nchi hii? Kama Bunge ambalo ni msimamizi kwa niaba ya wananchi hawataki kuzungumza naye, basi watuambie wanazungumza na nani naamini Serikali itatujibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kurudia kwamba hili fumbo la Roho Mtakatifu nililolisema kwenye kitabu hiki naomba Waziri anijibu baadaye ni namna gani taarifa ya mwaka 2007 inaingia kwenye kitabu cha 2006. Niwashukuru tena naomba kabisa kwamba Ofisi hii itakapoimarika Bunge litakuwa limeimarika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

**MHE. ZUBEIR ALI MAULID:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nami niungane na wale wote ambao wametangulia hapa kwa kuipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu. Napongeza uletwaji wa Muswada huu kwani utakuwa msaada mkubwa sana na kama ulivyotamka mimi ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali. Kwa hiyo, ni nyenzo mojawapo ya utendaji kazi katika Kamati yangu kama ambavyo ametangulia kuzungumza Mwenyekiti wangu wa Kamati Mheshimiwa Cheyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, umuhimu wa Muswada huu kama ambavyo wamezungumza wenzangu mimi labda nianze kwa kuchangia baadhi ya maeneo machache ndani ya Muswada wenyewe ambayo yangehitaji kuangaliwa vizuri.

Kifungu ambacho ningependa kukizungumza kwanza kuna kifungu cha 30 (3) (d) ambacho ndani ya Muswada kinazungumza kwamba Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali apewe mamlaka ya kukagua (d) inasema *anybody in which the*

*Government is the majority shareholder* na hii ina maana kwamba sehemu yoyote ambayo Serikali itakuwa ina zaidi ya asilimia 50 ya hisa kwa hiyo hapo ndiyo akague Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Lakini ninachotaka Serikali inaweka fedha zake sehemu nyingi tu ambazo sehemu nyingine *shareholder* ya Serikali si asilimia 50.

Lakini fedha hizi tukumbuke bado ni yale yale makusanyo ya kodi za wananchi. Kwa hiyo, tungeshauri hapa kidogo ikaondoka hii na iwe mahali popote ambapo kuna investment ya Serikali Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali aruhusiwe kwenda kuangalia pale. Kwa hiyo, hapa nafikiri wenyewe Mawaziri wanaweza wakaangalia ni namna gani wanaweza wakatusaidia katika kurekebisha sehemu hii. Isiwe *majority shareholder* tu lakini hata kama kuna sehemu ambapo Serikali ina asilimia 10 kwa mfano basi Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwa faida ya wale walipa kodi aweze na kwenda kuangalia sehemu ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu nyingine kama walivyozungumza wenzangu ni zile ambazo zitahitaji mabadiliko katika Katiba zetu. Lakini hili ni bora Serikali ijitayarishe tu kwa sababu kwa ghafla sasa hivi sidhani kama tunaweza tukaleta mabadiliko ya Katiba. Lakini huu ni ule umuhimu wa kuweza kupandisha hadhi ya chombo hiki kwa sababu kwa hivi sasa kama tunavyofahamu katika lile shirika la kimataifa la *INTOSAI* na hata hili la Afrika *AFROSAI* sisi tuko chini kabisa. Nafikiri wenyewe wanaita ni la kwanza lakini ni kiwango cha chini kabisa. Kwa hiyo, angalau tuweze kunyanyuka na kufikia sehemu ambazo baadhi ya nchi za wenzetu wameweza kufikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi pia nitachangia kwa masikitiko hivi karibuni tulikuwa tunafanya ziara za kukagua maeneo mbalimbali kama Kamati ya Hesabu za Serikali na katika kukagua baadhi ya miradi tulifika Serengeti Mugumu na tulipohitaji kwenda kukagua kule Hoteli ya Sasako tuliambiwa ni *VIP* kwa kweli majibu tuliyoyapata yanashtua sana kwamba ndani ya nchi kuna mtu anaweza akaliambia Bunge kwamba sisi hamuwezi kuja kwa sababu wageni wetu hawapendi usumbufu. Yaani Kamati ya Bunge haiwezi kwenda sehemu kwa sababu kuna watu hawatakiwi wapate usumbufu.

Sasa kwa ghafla nilijiuliza hawa wageni ambao hawataki usumbufu wanatoka katika Sayari gani *Jupiter* au *Satan* kwa sababu ikiwa hawa watu ni wanadamu, kwanza unaizuia Kamati ya Bunge kufanyakazi ambayo iko kisheria na Katiba, kwa jawabu dogo tu la kwamba tuna wageni ambao hawawezi kupata usumbufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nashauri sana tunapoingia Mikataba na hawa wawekezaji, tuwe waangalifu sana kwa sababu hatua hii inakiweka kipande kile cha ardhi, maana yake ni kama nchi nyingine ndani ya Tanzania ambapo mtu mwingine hawezi kuingia mpaka awe na kibali au labda na *passport* ndiyo aweze kuingia katika eneo lile. Sasa ikiwa Kamati ya Bunge haiwezi kuingia kule je, mwananchi Mtanzania wa kawaida katika eneo lile ataingia? Kwa sababu tuna habari hata huyo Mbunge mwenyewe wa Serengeti ambaye kwa bahati mbaya ni Naibu Waziri sidhani kama amewahi kufika katika eneo lile kwa sababu haruhusiwi kuingia kule kwa sababu kuna

wageni ambao hawataki usumbufu. Sasa vitu vya aina hii tuwe makini navyo kama Serikali, ni matusi kama alivyozungumza mwenzangu mmoja hapa tena kwa chombo kizito sana kama hiki cha Bunge kwa sababu Kamati za Bunge zinafanyakazi kwa niaba ya Bunge.

Kwa hiyo, ni sehemu ya Bunge ambayo inafanyakazi kwa sababu sote hatuwezi kufanyakazi ya aina moja. Kwa hiyo, ni kama Bunge limekwenda pale halafu likakataliwa kwenda kuona kile kinachoendelea pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu suala lingine la kujiuliza huku kuna kitu gani ambacho huyu mtu hataki kionekane, ni nini? Na huu mkataba wake ambao Serikali tumefungiana naye ni mkataba wa aina gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naishauri Serikali kwa kweli vitu vya aina hii tuwe waangalifu na wawekezaji wa aina hii. Lakini kwa hili la huyu kwa kweli hili tutaendelea nalo na tunahitaji maelezo kutoka kwa yeye mwenyewe na Serikali pia itusaidie tueleze kuna nini na kwa nini chombo kingine chochote cha Serikali hakiwezi nani anaweza kwenda kule?

Maana ikiwa Bunge haliwezi kwenda nani anaweza kwenda kuangalia kinachoendelea? Vitu vya aina hii ni kuviangalia kama mkataba wake una kikomo ukimalizika mtu wa aina hii asiongezewe mkataba mpaka mrekebishe baadhi ya vipengele vya aina hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kwa ujumla Muswada nauunga mkono na nina ukubali na nilitaka kuzungumza. Kwa kweli kubwa nililotaka kuongea lilihusiana na hili la kwamba kuna baadhi ya maeneo ya nchi baadhi ya vyombo tena vizito kama Bunge haviwezi kufanyakazi.

Kwa kweli tuwe na mazingira mazuri ya kazi na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu maana atakayekwenda kule siyo Mbunge, watakwenda maofisa wa ofisi hii ya Ukaguzi ili waweze kupata rukusa ya kuweza kwenda na ndiyo nilikuwa nasisitiza kile kipengele kwenye sheria kwamba isiwe tu sehemu ambayo tuna asilimia 50 lakini hata *investment* ya asilimia 10 au asilimia 5 ya fedha za wananchi walipa kodi basi mdhibiti na Mkaguzi Mkuu apate *access* ya kuona fedha zile za wananchi zinatumika vipi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, mimi nilikuwa na mchango huo mmoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. ESTHERINA J. KILASI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi angalau ya dakika chache ili niweze kusema machache.

Mimi naomba nianze kwa kusema kwamba naupongeza sana Muswada huu ambao umeletwa na Serikali kwa sababu kimekuwa ni kilio chetu cha Kamati hizi kwa muda mrefu niseme chanzo kikubwa kwa Kamati ya *PAC* baada ya Bunge lako Tukufu kuliruhusu liweze kutembelea sehemu mbalimbali kuona wenzetu wanafanya nini kwenye shughuli hizi za ukaguzi.

Lakini mambo muhimu ambayo yalitupelekea hasa kuomba kwamba *CAG* awe na sheria pekee ni mambo muhimu yalikuwa matatu ambayo ndiyo tulikuwa tunategemea yaonekane katika Muswada huu.

La kwanza kwamba chombo hiki kiwe na wajibu wa kuajiri chenyewe na kupanga mishahara na kuweza ku- *discipline* wafanyakazi wake na hata kuwaondoa wafanyakazi pale ambapo inabidi. Wasifuate sheria ya utumishi wa umma.

Lakini la pili ni upande wa uwajibikaji wa *CAG* kwamba tunaamini kabisa chombo hiki ni msaada wa Bunge na ni haki yetu sisi Wabunge kwamba *CAG* aripoti moja kwa moja kwenye Bunge bila kupita kwenye chombo ambacho yeye mwenyewe anakikagua. Kwa hiyo, ndiyo lilikuwa lengo kubwa sana hili.

Lakini lingine lilikuwa ni upande wa uwajibikaji wa maafisa wahasibu kwamba sasa chombo hiki kilikuwa hakina meno, sasa tulitaka sheria iweze kutoa meno kwa chombo hiki kwamba pale ambapo wanakagua isiwe nafasi ya kushauri tu Serikali na iwe na uwezo wa kufuatilia kwa ukaribu kuona yale yote ambayo mapungufu yamepatikana yanafuatwa na yanachukuliwa hatua. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi naomba niipongeze Serikali hii kwa kweli kwa kuwa sikivu sana kwa maombi ambayo Wabunge tumeyasemea na nafikiri kwa wananchi kwa ujumla. Mimi nimepata uzoefu angalau kwa Kamati tumetembelea Uingereza, tumetembelea Denmark, tukiwa kwenye Kamati ya *PAC* tumekuwa kila wakati ukiulizwa sheria yenu inasemaje kuhusu *audit/ controller and auditor general* wenu anakuwa *appointed* na nani. Je, anawajibika vipi?

Lakini bado tumekuwa na kigugumizi. Leo nina faraja kubwa kabisa kuona kwamba sheria hii imeletwa mbele ya Bunge lako tukufu na inapitishwa na inapitishwa.

Kwa hiyo, niwaombe Wabunge waiunge mkono kwa asilimia zote ili kusudi hii sheria iweze kufanyakazi haraka iwezekanavyo.

Lakini niungane na Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC* kwamba *timeframe* huwa ni muhimu sana kwamba tukipitisha kwamba hii sheria itaanza lini kutumika, kama ilivyojieleza kwamba huyu *CAG* aliyeopo sheria itakapo-*take place* maana yake *automatically* na kipindi chake kitaanza kuhesabiwa kuanzia hapo tu sheria itakapoanza kufanyakazi lakini kanuni huwa mara nyingi sana huwa zinachelewa. Sisi tuna hamu sana kuona kwamba hii sheria inatekelezwa mapema iwezekanavyo.

Sasa mimi kama makamu Mwenyekiti wa *POC* nilikuwa nimeguswa na mambo fulani kwenye Muswada huu, hii ya kukagua mashirika yaani *CAG* awe na uwezo wa kukagua kule ambako Serikali imewekeza asilimia 50 au zaidi ya 50% lakini kuna hela nyingi sana ambazo Serikali imewekeza kwenye kiwango cha chini ya asilimia 50%.

Tukichukulia makampuni machache ukiangalia *Celtel* na makampuni mengine kuna asilimia 40 huko tunahitaji kupata gawio kubwa sana. Kwa hiyo, ni wajibu wa *CAG* hisa hizi ambazo zimewekwa hata kama ni chini ya asilimia 50 aweze kukagua na kuona ni kiasi gani kimepatikana huko ili kuchangia pato la taifa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kifungu hiki kwa kweli 30 (d) nilikuwa napendekeza kabisa kiweze kurekebishwa awe na uwezo wa kupita kote huko kwa mfano Kamati yangu sasa inaangalia tulikuwa na uwezo wa kuangalia tu kwenye mashirika umma ambayo yana asilimia 50 na kuendelea huku chini tulikuwa bado tulikuwa bado hatuna uwezo kwa sababu hayaleti hesabu kwetu, kwa sababu hesabu hizi hazipiti kwa *CAG* inakuwa siyo rahisi kwa Kamati ya *PAC* kuweza kupitia hesabu hizo.

Lakini ni haya tu ambayo tunayapitia tumeona kuna mapungufu je, huku ambako *CAG* hataona ni kiasi gani ambapo gharama za uendeshaji zinakuwa kubwa ikionyesha kwamba hazipati faida na kwa maana hiyo Serikali itakuwa haipati gawio lolote kwa miaka mingine yoyote na ndiyo haya ambayo yanajitokeza sana. Lakini nipongeze kwamba sasa Sheria hii itaruhusu Kamati zetu zitambulike kisheria na hata hili ambalo limewapata wenzetu wa *PAC* halitatupata tena baada ya hii sheria kupita. Kwamba itakuwa mtu lazima aheshimu chombo cha Bunge aheshimu Kamati kwamba tunafanyakazi kwa niaba ya Bunge na kwa niaba ya wananchi ambao wametuweka madarakani. Kisiwe tu kwamba Wabunge wanaleta usumbufu. Kwa hiyo, hili lilijitokeza wakati fulani tulipokwenda Mwadui, tulitembelea kampuni ya madini pale Mwadui nikiwa *PAC* lilijitokeza hili unakuta mwekezaji hana ari ya kuwaambia ukweli wa mambo ambayo yanajitokeza pale. Lakini tukija tukapata faida kwa mwekezaji mwingine tu mswahili mwenzetu. Sasa hili kwa kweli sheria iweke wazi watambue kwamba hizi *oversight committee* ni muhimu sana kwa Serikali, ni muhimu sana kwa Bunge, ni muhimu sana kuangalia mali ya Serikali kuona kwamba haipotei bure.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niseme tu kwamba *CAG* sasa sheria hii imepita. Lakini la msingi kabisa ni chombo hiki kipate uwezo. Kwa muda ambao tumekuwa nao hali imekuwa siyo nzuri sana, labda kwa sababu itawaruhusu kwamba wanaweza kuajiri wafanyakazi wao, kiwezeshwe kabla ya kuanza rasmi. Ukilinganisha wakaguzi binafsi kwa sababu sasa hivi ni biashara huria anachukuliwa kwenda kukagua mahesabu yale yale ambayo *CAG* imechagua kutokana na kukagua, kunakuwa na tofauti kubwa sana. Sasa tungependa ili *CAG* sasa awe na uwezo wa kukagua na taarifa yake iweze kukubalika badala ya kutafuta kingine cha nje kuja kufanyakazi hiyo hiyo ambayo *CAG* ameifanya basi chombo hiki kipewe uwezo zaidi na kuweza kujua kwamba kinafanya kwa niaba ya Bunge.

Kwa hiyo, hilo ningependa sana nilisisitize na tumepata uzoefu sana unapopitia Hesabu na Mkaguzi wa Nje anapotoa taarifa ukalinganisha na uzoefu wa wakaguzi ambao anao *CAG* bado kuna tofauti kubwa sana. Lakini naamini sasa watapewa nguvu, watapewa uwezo wa kujiendesha wenyewe na watawajibika.

Lakini hili hili bado kulikuwa na marekebisho kidogo kwenye nafasi ya Waziri wa Fedha anaonekana bado ana nguvu sana kwa chombo hiki. Kwa sababu hapa ni kushauri, sasa ni lini, kwa sababu tunaamini Rais ndiyo mwenye mali zote anatakiwa aripoti huko. Lakini sasa kadri tunavyoendelea, angalau tuangalie kama kutatokea marekebisho hapa sasa, *CAG* moja kwa moja atoe ripoti yake, akishakamilisha taarifa ampelekee Mheshimiwa Rais, lakini ripoti iletwe moja kwa moja Bungeni, iwasilishwe ndani ya Bunge. Badala tena ya ku-*challenge* kwa sababu sasa inategemea kama ni *special report* Mheshimiwa Rais anaweza akaisoma akasema ataipeleka, lakini Sheria inamwambia baada ya siku 7 iwe imepelekwa mle ndani ya Bunge. *(Makofi)*

Lakini inategemea sasa anayepewa kuleta huku atailete lini, lakini akipewa uwezo wa kuileta mwenyewe itatusaidia sana, na yeye itampa nguvu ya kuwa na moyo wa kufanya kazi kwa kadri ya utaalam wake alionao na kadri ya *profession* inavyomruhusu. Kwa hiyo, hili ningependa nisisitize sana kwamba bado tunaomba Serikali iendelee kuangalia kukipa uhuru zaidi chombo hiki cha kuweza kuleta moja kwa moja ndani ya Bunge na masuala yote yaweze kwenda haraka. Lakini vile vile kwenye upande wa tozo, tumekuwa tukihangaika sana Kamati hizi, unapomkuta Afisa Mhasibu *Accounting Officer*, au Afisa Masuhuli, kumekuwa na mapungufu. Sheria ya Fedha inasema utamshauri Waziri, sisi Kamati tutamshauri Waziri kwamba Afisa Mhasibu fulani amefanya mapungufu fulani. Kwa hiyo, tunaomba apewe tozo na hiyo inaandikwa kwenye ripoti. Sasa inategemea Waziri na wepesi ni kiasi gani ataamua kumpa na kwa kiwango gani atampa adhabu ile Afisa Mhasibu.

Ni lini basi hizi Kamati zenyewe kama *PAC, POC, LAAC* watapewa meno wanaposema tutoe tu kwamba Afisa Mhasibu amekosea kama ni asilimia 5 ya mshahara wake hiyo adhabu imepita moja kwa moja badala tena ya kwenda kumshauri Mheshimiwa Waziri kwamba atoe hiyo. Adhabu zitolewe moja kwa moja na Kamati kama tunavyotoa mapendekezo ndani ya Bunge. *(Makofi)*

Hayo mapendekezo tukiyaleta Bungeni, Bunge likipitisha maana yake hiyo adhabu tayari imeshachukua hatua ya kutekelezwa kwa yule ambaye anahusika. Badala ya kumshauri Waziri, Waziri naye ailete Bungeni, imechukua mlolongo mrefu sana. Kwa hiyo, ni vifungu hivi vichache ambavyo vinabidi virekebishwe ili kwa kweli hii Sheria iweze kuleta manufaa kwa nchi yetu kwa Bunge na wananchi waliotuchagua. Lakini niseme tu nilikuwa na hayo machache, la msingi nina furaha kubwa sana kwa kuona sheria hii leo imepita na itaanza kutekelezwa. Kwa hiyo, ninachomwomba Waziri mwenyewe dhamana hii ya Fedha na Uchumi atusaidie kuhakikisha kwamba muda ambao wa kuanza kutekeleza unakuwa mapema iwezekanavyo kwa maana ya Kanuni ziwekwe haraka iwezekanavyo.

Baada ya kusema hayo naomba niunge mkono kwa asilimia moja. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie kuhusu Muswada huu. Mimi kwa kweli kama wenzangu waliotangulia niseme naunga mkono mia kwa mia kwa kuletwa kwa Muswada huu leo, pamoja na kwamba umechelewa lakini niipongeze Serikali imeona umuhimu wa kuiachia *Audit Office* ili ijitegemee. *(Makofi)*

Muswada huu utasaidia sana kufanya Ofisi yetu ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali kufanya kazi kwa uhuru kamili. Uhuru ambao unaendana na mabadiliko ya dunia. Sasa hivi Kitengo cha Ukaguzi ni Kitengo ambacho kinaaminika sana duniani kote na kitengo ambacho kinafanya kazi nzuri kuhakikisha wote wanaotumia fedha za umma wanafuata taratibu zilizowekwa na siyo kuchezea tu fedha za wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niseme tu kwamba Ofisi yetu ya Ukaguzi wa Taifa imepiga hatua kubwa na sasa hivi hawababaishi au hawafanyi kazi kwa mazoea kama walivyokuwa wanafanya kule mwanzo na walikuwa wanafanya hivi kwanza kutokana na ukosefu wa vitendea kazi, kutokana na watu ambao hawana elimu ya kutosha, lakini sasa hivi kwa kweli nawapongeza sana. Sasa hivi wameamua kwa kushirikiana na Kamati hizi tatu za Bunge kufanya kazi kwa uhakika zaidi. Sasa hivi wanakagua *value for money* na wanafanya *performance audit* na sisi Kamati zetu tumeshirikiana nao kwa karibu na tumekwenda kushuhudia mambo yanaofanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi, wakaguliwa wote wamekuwa wajanja kuandika vitabu vyao vizuri. Ukipitia vitabu bila kwenda kule miradi inakofanyika utaona ni mambo mazuri kweli kweli. Lakini sasa hivi tunapokwenda kufanya *performance audit* au *value for money* utashangaa mambo yanakofanyika. Watu wanajenga nyumba za Serikali chini ya viwango vilivyowekwa, wanatumia *soft wood* ambayo hairuhusiwi na Serikali. Wanatumia mabati geji 30 ambayo kwa kweli Serikali haikubaliani na hilo. Kwa hiyo, mimi naomba hii Sheria ipitishwe mapema na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali awe na mamlaka kamili. Mimi naipongeza Serikali kwa hatua hii iliyofikia ile inayosubiri kubadili Katiba tusiwe na haraka nayo. Kwanza tuanze na hatua hii ya kwanza. Tuende nayo na nina imani kazi nzuri tu itafanyika na

hapo Katiba itakapobadilishwa hiyo hatua nyingine itakayofikia nina imani tutakwenda kwa kasi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimesikitika sana kusikia kwamba Kamati ya Bunge ilikwenda kwa mwekezaji wakazuiwa kuingia na kuangalia kinachotokea. Hili ni jambo la aibu kwa Bunge letu, ni jambo la aibu kwa Serikali yetu na mimi kwa kweli napendekeza kabisa yule mwekezaji achukuliwe hatua haraka iwezekanavyo. *(Makofi)*

Kama Watanzania, kama chombo kilichotumwa na wananchi wa Tanzania kinazuiwa kuingia kwenda kuangalia mradi ulioko kwenye nchi ya Tanzania, basi hili Bunge litakuwa halifanyi kazi yake vizuri. Kwa kweli wananchi hawatatuelewa na sisi tunataka Serikali na Bunge lichukue hatua haraka sana. Anaficha nini, kuna nini ambacho Bunge na Serikali haviwezi kuona.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nikuambie hilo eneo nalifahamu. Nilipokuwa Mkuu wa Chuo cha Pasiansi ilikuwa eneo letu la mafunzo pale. Pale pana utajiri mkubwa sana wa wanyama. Ni eneo ambalo tusipoliangalia uchumi wetu utakuwa unapitia pale unakwenda kwa watu wasiohusika.

Kwa mimi naomba Serikali ichukue hatua, na pale hii Kamati iende pamoja na Wakaguzi wetu waende waone kuna nini kinafanyika pale. Na siyo hapo tu kunaweza kuna maeneo mengine. Sasa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali aingie maeneo yote ambayo Serikali inawekeza. Mimi napingana na lile mnalosema kwamba inapowekeza zaidi ya asilimia 50 hapana. Fedha yote ya Serikali inapoingia mahala hata kama ni ndogo ni lazima wahusika wafuatilie. *(Makofi)*

Kwa mfano sasa hivi taarifa tulizonazo haya makambi yetu ya simu za mikononi, Serikali ina hisa kwenye baadhi ya makampuni haya. Nani anakwenda kuangalia hisa zetu zimefikia wapi. Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali ndiyo anakwenda kwa niaba ya Bunge hili na kwa niaba ya Serikali yetu kuangalia nini kinaendelea na sisi kama Wabunge ni lazima tumtake Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali hiyo kazi kwa makampuni yote ambayo Serikali ina mkono wake ianze kazi mara moja kuangalia hizo hela ziliwekwa toka lini mpaka sasa gawio la Serikali linakwenda wapi. Inaweza kuwa hizi fedha haziendi Serikali zinaishia hewani.

Kwa hiyo hilo mimi ningeomba sana Mheshimiwa Naibu Spika, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali aingie mara Sheria hii itakapoanza kutumika. Tumwombe tu Mheshimiwa Rais, kwa sababu Sheria hii imekuja kwa wakati na inahitajika haraka apatapo nafasi aidhinishe mara moja na ianze kutumika. Vile vile Kanuni zisichelewe, Kanuni ndiyo zinaweka vikwazo kwenye Sheria nyingi hapa tunapozipitisha. Kwa hiyo, tunaomba haya mambo yaanze haraka ili Sheria hii ianze kufanya kazi na vile vile niwapongeze sana wenzetu wa Sweden na Mashirika mengine wanaosaidia Ofisi yetu ya Ukaguzi. Kwa kweli wanafanya kazi nzuri. Tulikwenda Babati kuona *performance audit*. Ni kazi ya kusifiwa na ni kazi ambayo inaleta heshima kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niwaombe tu wahusika wote na sisi Wabunge na hasa hizi Kamati tatu *POC, PAC* na *LAAC* tumsaidie na Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali ili nchi yetu ipate maendeleo ya haraka. Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Spika. *(Makofi)*

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana kunipa nafasi hii. Kwanza niseme tu kwanza kabisa mimi napenda nichukue nafasi hii kuunga mkono Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze Serikali kwa kuuleta Muswada huu katika kipindi hiki ambacho dunia katika maendeleo ya ukaguzi imefikia hatua ya juu, hali ambayo inatufanya sisi Tanzania tushindwe hata kuwepo katika *level* yoyote katika *standards* za kimataifa. Lakini pia katika *standards* za Afrika. Labda baada ya kupitishwa kwa Sheria hii tunaweza tukaangaliwa kama na sisi tumefikia *level* ipi, lakini mpaka sasa hatupo kwenye *level* yoyote ya kiukaguzi.

Kwa maana hiyo ni kwamba kwenye taarifa kama alivyosema Mheshimiwa Waziri wakati anawasilisha Muswada huu sisi hatupo *rank* yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Muswada huu unakuja katika kipindi hiki ambacho unahitajika sana na ni matumini yangu kwamba Muswada huu baada ya kupitishwa utaanza kutumika haraka iwezekanavyo. Kwa maana ya kupitishwa kwa hatua zinazofuatia. Lakini nina mambo kadhaa ambayo ningependa na mimi kuchangia katika Muswada. Roho ya Muswada huu ni kukifanya chombo hiki cha ukaguzi katika nchi yetu kiweze kujitegemea zaidi na kiweze kuwa na maamuzi bila shinikizo lolote lile. Kwa maneno mengine ni kwamba Muswada huu roho yake hasa ni kufanya chombo hiki kiwe *autonomous*. Sasa *autonomous* kwa namna gani. Autonomas ya chombo chochote inaanzia na uteuzi au uchaguzi wa kiongozi wa chombo husika. Ni kweli viko vikwazo vya kikatiba vinavyoeleza namna ambavyo uteuzi unatakiwa kufanyika, na hivyo Sheria hii imejitahidi kufuata vile lakini tufike mahala tukubaliane kwamba kwa namna yoyote ile Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali ni Afisa wa Bunge. Ni Afisa wa Bunge katika kiwango kwamba yeye ndiye jicho la Bunge, Bunge ambalo linawakilisha wananchi. Kwa hiyo taarifa yake ni taarifa ya Bunge na kwa mantiki hiyo basi katika uteuzi kunatokea hapa mapungufu kwamba ilipashwa basi kama ambavyo Bunge linathibitisha uteuzi wa Waziri Mkuu basi Bunge lingethibitisha uteuzi wa Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali. *(Makofi)*

Kama tunathibitisha uteuzi wa Waziri Mkuu kwa nini tuthibitishe uteuzi wa Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali. Maana yake hili ndiyo jicho letu sisi Bunge. Yote tunayozungumzia hapa ni taarifa ambayo ni kwa niaba ya wananchi. Taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali ni taarifa ya wananchi, wakisikia hela yao inaliwa Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali anapotoa taarifa kwamba kuna mahala fulani kuna upotevu wa hela au kuna taarifa ambayo haieleweki kwamba fedha zinapotea au vinginevyo taarifa ile ni kwa ajili ya wananchi.

Kwa hivyo ni lazima kwa kweli tufike mahala tukakubaliane kimsingi na ninaamini kwamba maumivu kwa katiba hata kama jambo hili litakubalika si makubwa kwa kiasi hicho kama Bunge litamthibitisha *Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali.*

Mengine katika mapungufu yanayotupelekea kufika kwenye *standards* zinazotakiwa ni makubwa, lakini hili si kubwa kwa kiasi hicho. Nimeisoma katiba na nimeona si kubwa kwa kiasi hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninalo jambo lingine linalohusiana na wigo wa ukaguzi, *scope of audit*, ambayo imesemwa sana katika *Section* ya 30 na *part* ile mzima. Huu wigo wa ukaguzi ni jambo pana kidogo. Lakini hapa Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali anaruhusiwa na sheria hii kukagua pale ambapo Serikali ina *share* za asilimia 50 na kuendelea. Hivi *share* ya asilimia 40 siyo fedha nyingi kwa Serikali? Hivi kweli tuache kwamba ile tuiache tu, sijui inatumika kwa misingi gani katika ku-*determine position* ya pato lile, tuacha vile vile hili jicho na mali hii ni mali ya wananchi wa Tanzania, na jicho lao wananchi wa Tanzania ni Wabunge na Wabunge ndiyo wanaopokea ripoti hii ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali, tunaiacha ile hatuwezi kuiangalia. Mimi nadhani huu ni upungufu mkubwa na ni vizuri Sheria hii ikaiangalia hii na ni vema Serikali ikakubaliana na mawazo yaliyotolewa na Wabunge wengi na mimi nasema kwa kweli itakuwa ni busara kuangalia. Najua ziko *technicalities* za mambo ya *finance* katika suala zima la uendeshaji wa makampuni na masuala ya *science* ya *shares* na kadhalika.

Lakini kwa kweli katika msingi wa sasa wa uwazi na ukweli Bunge linapaswa lipate taarifa hii, hata kama Serikali inamiliki *share* chini ya 50. Kwa hiyo, mimi nasema kuna haja ya kuiangalia sehemu hiyo. Lakini jambo lingine katika sehemu hiyo pia ni kwamba kwa kiasi kikubwa kama walivyosema wenzangu kinachofanyika na Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali ni kama *postmoterm*. Mimi nina wasiwasi kwamba hata kama Ofisi ya *CAG* ana uwezo wa kujua hata mapato kwa kiasi cha kutosha kama inavyojua matumizi yake. Kwa kiasi kikubwa inafuatilia matumizi kuliko mapato yake. Sasa huwezi ukakagua matumizi kama hujui mapato kwa kiasi cha kutosha. Ziko *Public Authorities* ambazo kwa mfano *this time* walikagua tumeona kwenye taarifa, wamekagua mashirika kama 91 kati ya 158.

Katika mashirika haya 91 kati ya 158 utaona kwamba kwa mfano *NSSF* na mashirika mengine, huyu Mkaguzi hawezi akajua *exactlly* mapato yanayopatikana. Kwa hiyo, ni vizuri kabisa kwamba katika hii *scope of auditing* basi aweze kujua na mapato kwa ufasaha yanayopatikana na kisha aangalie na matumizi. Hili jambo nilipenda pia Sheria hii iliangalie. Lakini nizungumzie pia kina cha matumizi yenyewe ambacho Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali anayaangalia. Utakuta karibu asilimia 80 ya matumizi ya Serikali yanapotelea kwenye *procurement.* Na *procurement* sina hakika kama kupitia *PPRA* na Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali nani anaweza akaenda *dipper* kuweza kujua hali halisi ya *procurement processes* na *system* zinazofanya kazi katika mashirika yetu ikiwa na pamoja na Halmashauri na sehemu zote ambazo Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali anafika. Mimi

nasema kuna upungufu mkubwa *procurement* ni lazima Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali lazima awe na *access* pamoja na kwamba yuko *PPRA* ambayo wanaangalia *regulations* wanaangalia taratibu na kama haya mambo yanafanyika lakini kwa maana ya kimahesabu na kujua matumizi yale ya *procurement* na ukizingatia kwamba mengi yanafanyika kwa kununua huduma ile kwa sababu hapa nchini kwetu hatuna Idara za *Procurement* katika mashirika yetu, katika Wizara zetu kwa kiasi cha kutosha. Mengi tuna hire na kufanya vitu vya namna hiyo. Kwa hiyo, fedha nyingi sana inapotea na ndiyo utakuta hata miradi ya maji ambayo sasa inachelewa na tunaambiwa *World Bank, World Bank* ni kwa sababu ya upungufu wa *procurement*.

Kwa hiyo, mimi nadhani Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali angefika hata kuangalia hizo *procurement process* kwa maana ya kihesabu na taarifa za kujua *procurement* zinafanyikaje ingetusaidia lakini siyo kusema *PPRA* peke yao wanaweza wakashughulikia hili la-*administrativeslly* lakini pia wakaiangalia hata katika suala zima la kihesabu. Mimi nadhani kuna haja katika ile *scope* tukasema pia Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali pale kwenye *section* ile kwamba anaruhusiwa pia kuangalia katika masuala hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, limezungumzwa hapa katika sheria hii, *Section* ya 28 hasa *Part* ya 4 suala zima la namna ya ukaguzi. Namna ya kukagua ukizungumzia kwa mfano tu ile *performance audit* peke yake, utaona kwamba kazi ya *performance audit* ni kubwa na sina hakika kama kwa kiasi cha kutosha wote tunafahamu *performance audit*. Nilipata ya kwenda
Uingereza na tukajifunza hiyo *performance audit* na tukaweza kuona *extent* zake *elements* zake. Kimsingi kweli *performance audit* ilipaswa kupewa mkazo katika nchi yetu, hasa nchi zinazoendelea kwa kila jambo. Tumeona mfano wa Babati, unaweza kuona matatizo kwa sababu *performance audit* ina-*appreciate economies, efficience* na *effectiveness.* Sasa utaweza kuona mji wa Babati hata ulivyobuniwa na waliosema mji wa Babati ukae pale ilikuwa ni makosa. *Performance audit* ipo lakini sina hakika ni kwa kiasi gani Serikali imetumia taarifa ile ya mfano ambayo *CAG* ameitoa toka 2006/2007 kama imefanyiwa kazi ya kutosha. Hakuna kilichofanyika ni kwa sababu bado nadhani Serikali haiko *aware* hata kama inafanyika haina hatua za kuchukua za haraka juu ya taarifa hizi za *performance audit.* Kwa hiyo, mimi ningeshauri kwamba chombo hiki kiwezeshwe vya kutosha Sheria peke yake haitoshi, lakini chombo hiki kiwezeshwe vya kutosha ili kiweze kufanya kazi zake vizuri. *Performance audit* inahitaji wataalam waliobobea, inahitaji mainjinia, inahitaji watu mbalimbali wenye ujuzi mbalimbali ili kuweza kufikia mwisho wa *audit* ya namna hii. Ni kitu cha maana na kwa kweli ungekuta miji mingi isingekuwa na matatizo yanayotokea sasa hivi kama tungeruhusu *performance audit* kufanyika na Serikali ikaweza kufuata. Ningeshauri sana kwamba pamoja na kuipitisha Sheria hii lakini tuangalie pia namna ambavyo tutakavyokisaidia chombo hiki kiweze kuwa na uzito unaolingana na kujipatia Sheria yake. Jambo la mwisho ambalo limenifanya niwe na *concern* na mimi hapa ni suala zima lililozungumzwa na wenzetu waliokwenda kutembelea *VIP Hotel.* Jambo hili linasikitisha, ni aibu kwa nchi, ni aibu kwa wananchi, ni aibu kwa viongozi, ni aibu kwa Serikali. Kama mtu anayekuja kuwekeza anakuwa wa maana kuliko sisi wenye ardhi na maliasili. Hii ni aibu. Mimi nasema, naomba niseme zaidi ya wenzangu walivyosema,

wapo waliosema wachukuliwe hatua. Mimi nasema hiki kiburi cha huyu kinatokea wapi? *(Makofi)*

Ni kwa namna yoyote labda kuna sababu, sisi tungependa kama Bunge, na mimi ningeshauri kwamba mkataba wa huyu mtu uletwe hapa Bungeni. Mkataba wa wawekezaji hao uletwe hapa Bungeni tuone ni kiburi cha kawaida au ni kiburi kinachotokana na sababu nyingine. Naamini hilo ni eneo moja lakini yako maeneo mengi ambayo Watanzania wananyanyaswa, Watanzania wanakuwa kama wakimbizi kwenye nchi yao kwa sababu ya uwekezaji, uwekezaji. Mimi nasema ipo haja tukafika mahala tukakubaliana na Serikali kwamba wakati mwingine mambo mengine tusaidiane. Sisi kama Bunge ni kwa niaba ya wananchi, Serikali ya Tanzania ni Serikali ya wananchi. Kwa kuwa tunafanya kazi moja basi tukubaliane katika mambo kama haya ambayo yanaonekana kwamba ni ya kutolea mfano kama hili la *VIP*. Mkataba uletwe tuweze kujiridhisha wote, kiburi kinatokea wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Ahsante sana. Naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. ATHUMANI S. JANGUO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie kwenye Muswada huu muhimu. Nitangulize kwa kusema kwamba nauunga mkono Muswada huu mia kwa mia. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi. Kwa hiyo, maoni mengi ambayo yalikuwa yametolewa na Makamu wetu kwa kweli yametokana na sisi na tunamwunga mkono moja kwa moja. Sababu ya kusimama hapa ni kwamba nilikuwa nataka tu niweke mkazo katika maeneo fulani fulani na ya ziada pengine kama yalikuwa hayakuonekana wakati wa Kamati. Sheria ya Fedha ya mwaka 2001 Sura 348 ililenga kuongeza nguvu za Sheria na uwezo wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Muswada huu unafanya hilo hilo pamoja na kufuata masharti ya Katiba na kwenda na wakati. Lakini utaona kwamba ameongezewa nguvu na Muswada huu, bali niseme kama walivyosema baadhi ya wenzangu walionitangulia. Nadhani pana haja siku za mbele kumpa nguvu zaidi na kumpa nguvu zaidi ni kwamba sasa hivi hawajibiki mbele ya wawakilishi wa umma, yaani Bunge anawakilishwa na Waziri wa Fedha. Sasa nauliza Waziri wa Fedha amekuwa Waziri Mama, hivi atakapoikagua Hazina halafu akawa na maoni tofauti na hali ilivyokuwa, Waziri huyo anaweza akawasilisha sawasawa wakati yeye ndiye aliyesahihishwa? Kwa hiyo pana haja ya kuhakikisha kwamba najua kwamba hili pengine litahitaji kufanyiwa marekebisho katika Katiba. Sikubaliani na baadhi ya wasemaji hasa kutoka Upinzani kusema kwamba ibadilishwe Katiba kwa sababu ya tukio moja. Lakini tunaishauri Serikali huko tuendako wameshawahi kufanya marekebisho. Sasa watakapofikia kufanya marekebisho hii ni eneo moja ambalo linahitajika kuangaliwa vizuri ili kusudi Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali aweze kuwajibika mbele ya Bunge moja kwa moja kama ilivyo kwa *AG.* Baada ya kusema hilo, ningependa niende kwenye maeneo mengine madogo madogo ambayo kwa kweli yanahitaji kufanyiwa marekebisho. Naona lipo Jedwali la marekebisho, lakini nadhani hata hilo nalo linahitaji liangaliwe upya katika maeneo fulani fulani. Nianze na pale katika kifungu cha 9 ambacho kina (a) na (b) na sasahivi kwenye rekebisho imewekwa (c). Nakubaliana na marekebisho yaliyofanywa lakini ningependa niongeze tu katika hali hii ilivyo nafikiri ama unaiacha ile yote inakuwa ile (b) na (c) unazifuta halafu zote zinakuwa chini ya (a) au sivyo kama unataka kuweka (b) na (c) maneno ubadilishe kidogo Mheshimiwa Waziri, kwamba (b) huwezi kuanza na *any authority or body required by law.* Kwasababu haya yanatawaliwa na *The Controller and Auditor General shall be,* sasa *shall be any* haiji ni lazima useme ama *shall be auditing* bla bla bla, *any authority* na kuendelea na hivyohivyo kwa (c). Ama lile neno *conduct* unaliweka *conducting* ili kusudi unasema kwamba *the Controller and Auditor General shall be conducting* lakini haiwezekani ukaruka kwenda pale. Lakini ukiyaacha chini ya (a) basi maana yake ni kwamba yoote hayo yanatawaliwa na ile *opening sentence* inayosema *reporting on the account of* halafu unaendelea huko mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ningependa kulisahihisha ni pale kwenye 11 (f) tunasema yeye ata *accept as correct without further correction.* Mimi naona tutamfunga mikono, kama tunataka kumpa uhuru wake tumuachie yeye, akitaka kufanya *examination* afanye asipotaka anaweza akaendelea hivyohivyo lakini ukimuambia *without further examination* mimi nafikiri munamfunga mikono na hiyo inakwenda kinyume na kile kifungu cha 6 kinachosema *subject to any duty imposed on him by any written law that the Controller and Auditor General shall have complete*

*discretion,* sasa hii *complete discretion* iko wapi wakati unamuambia kwamba wakati anapopata ripoti hizi nyingine basi asifanye *further examination.*

*S*ehemu nyingine ambayo ningependa kuitolea maoni ni kifungu cha 15 (3), kinachozungumzia habari ya *internal Auditor of any Auditory Body which is subjected to auditing by the Controller and Auditor General* atakuwa anapeleka taarifa zake kwa *Controller and Auditor General.* Ukizingatia uwingi wa taasisi ambazo zinakaguliwa na huyu halafu uwe unasema kwamba ripoti zote za ndani ziwe zinapelekwa kwake, kwanza hiyo kazi hataiweza au sivyo baadhi ya hizo ripoti zitakuwa zinaishia kwenye madroo.

Mimi nafikiri tungempa kikomo ama tuseme *annual report* za *internal audit* au *semi annual reports* ili kusudi ziwe chache. Kwa mfano *Internal Auditor* akiwa anatoa ripoti ya miezi 6 akaipeleka kule ita *cover* na yale mengine yote. Maana kuna taasisi zingine zinatoa *internal reports* kila mwezi, nyingine kila *quarter* halafu uchukue na Serikali yote, Idara zinazojitegemea, mashirika, Serikali za mitaa na na kadhalika. Kwa kweli mzigo utakuwa mkubwa. Mimi nafikiri hapa panahitaji kufanya marekebisho ili kuwe na kikomo cha zile taarifa ambazo zinatolewa. Sehemu nyingine ambayo nadhani vilevile marekebisho yaliyofanywa hayakuzingatia vizuri ni pale kwenye kifungu cha 33 (3) ambapo naona kwenye marekebisho inakuwa mbaya zaidi, wameondoa lile neno *solely* wakaweka *sole.* Mimi nafikiri haiji kwa lugha, ama unalibakisha hilohilo la kama hulitaki basi liondoe hilo weak neno lingine kama *entirely.* Lakini huwezi uka *qualify verb* na *adjective.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye kifungu 37 (2) kimefanyiwa marekebisho ni mazuri tu, lakini mimi naona kifungu 37 (2) na kifungu 38 vyote hivi vinasema kitu kimoja. Kwa hiyo namshauri Mheshimiwa Waziri, aangalie ama anaondoa kifungu cha 2 ama anaondoa kifungu kidogo (2) cha 37 au anaondoa kifungu cha 38 kwasababu yanayosemwa pale ni yaleyale. Kifungu cha 42 (1) kimefanyiwa marekebisho mahala lakini mimi ninashauri kwamba kile kifungu kidogo (1), *the funds and resources. H*ebu tuongezee pale kwasababu haiwezekani ikawa *the fund and resource.* Baada ya hapo kuna kifungu cha 48 (4) kimefanyiwa marekebisho. Badala ya *not exceeding 1,000,000* imewekwa *5,* mimi nakubaliana nalo lakini basi na ile sehemu ya kifungo vilevile ibadilishwe. Maana ilipokuwa adhabu ya 1,000,000 ililinganishwa na uzito wa miaka 2, unapandisha kwenye 5,000,000 unalinganisha na uzito wa miaka 2. Mimi nafikiri hapo haiji ingekuwa ni vizuri tukatazama uwezekano wa kusema miaka 3 au 4.

Nikirudi katika jedwali la marekebisho, samahani huenda nikajirudia rudia, lakini nafikiri kuna mambo ambayo nadhani nimeyazingatia. Nimeshazungumzia habari ya kifungu cha 9 na marekebisho yake ya (b) na (c) lakini katika kifungu cha 17 ambacho kinatawaliwa na marekebisho. Tume *re-number sub clause 2* halafu *as sub clause 17,* hapana. Nafikiri itakuwa *sub clause 2 as sub clause 1.* Halafu katika kifungu cha 30 kinachotawaliwa na pale, nafikiri kwenye ile sehemu ya *inserting immediately after the paragraph (a) the following paragraph.* (b) unasema *which the government has invested its' monies. N*afikiri kuna haja ya kuanzia na neno *in which the government has invested money.*

Kifungu L kwenye ukurasa wa 3 pale jedwali la marekebisho, nilikwishakizungumzia habari yake ile *solely*. *K*wa hiyo, sitaki kurudia lakini chini ya N nilikwishasema vilevile unarekebisha kwa kuangalia uwezekano wa ama kufuta kifungu cha 38 au 37. Halafu katika kifungu cha 41, kifungu hiki hasa pale kwenye (3) kwenye mabano, kuna maneno ambayo yanasema *where the estimates of revenues and expenditure have been agreed upon by the Public Accounts Committee and the Minister, the estimate shall be presented to the Minister.* Tutawakilisha mara ngapi kwa Waziri? Mimi nafikiri itakuja vizuri zaidi ukishamaliza pale *the Minister* badala ya kusema kwamba *the estimate shall be presented to the Minister*. Ukayachanganya yale na kile kifungu cha 4 kwa kusema *and the Minister shall submit the accounts to the National Assembly for approval* kwisha. Badala ya kuweka kifungu cha 3 na 4 kisha ukasema unarudia ku *submit* kwa Waziri mara mbili mbili.

Mwisho ningependa na mimi kujiunga na wenzangu waliotoa lawama kwa mwekezaji ambaye alizuia Kamati ya Bunge kutokuingia katika maeneo ambayo yeye ni mwekezaji. Mimi nafikiri hatua zote kali zichukuliwe dhidi ya watu wa namna hiyo ili kusudi iwe mfano kwa wawekezaji wengine. Haya maeno ni ardhi ya Tanzania, haiwezekani mwekezaji aje hapa na vihela vyake kisha aweze kunyanyasa hata chombo cha wawakilishi wa Tanzania nzima. Nashukuru ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nitoe mchango wangu kidogo. Awali ya yote napenda kushukuru sana na kupongeza Serikali kwa jumla, lakini zaidi Waziri wa Fedha kwa kutuletea Muswada huu wa sheria ambao ni muhimu sana kwa sababu shughuli za *Control and Auditor General* zilikuwa zimeingizwa katikati ya shughuli nyingine kwahiyo hata kufanya *reference* iwakati mwingine unaona tabu kwahiyo naipongeza sana serikali kwa hatua hii. Nina mambo ya jumla tu, kwanza; katika ule ukursa wa 5, nimefurahishwa sana na Muswada huu jinsi ulivyoandikwa, kuwekwa maelezo ya msingi au ile *preamble*. Hii wamechukua kabisa mfano wa Katiba, nadhani hili Waheshimiwa Wabunge, tungesema basi miswada mingine inayokuja iwe na maelezo ya msingi kama haya; ni uboreshaji mzuri sana, naipongeza sana hatua hii *(Kicheko).*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo kwa muda mrefu niolikuwa nalitafutia mahali nilizungumze ni hili la *gazetement* ya miswada. Kwamba katika Katiba anayetambuliwa katika ibara ya 60 ni *Secretary of the Cabinet* au Katibu wa Baraza la Mawaziri, kwahiyo Katibu Mkuu Kiongozi au *Chief Secretary* hayupo kabisa katika suala la kutunga sheria. Ambaye tuna uhusiano naye wa kutunga sheria ni *Secretary to Cabinet,* kwahiyo ningeomba hili kwasababu halina sheria libadilishwe twende na utaratibu. Hicho kifungu 60 ndio kinachomtamka *Secretary to Cabinet* lakini *Chief Secretary* haonekani popote pale katika Katiba, nashukuru sana kwa hilo.Nina mambo mengine madogomadogo, hayo nitangojea wakati wa kukaa kama Kamati ya Bunge manaake kuna koma koma hizo na nini naona tusizilete saahizi tuzilete baadaye. Nitakwenda kwenye ukurasa wa 11 wa Muswada. Katika ukurasa huu wa 11 kifungu cha 11 (c) kinachosema *seek the professional opinion or advise of the Attorney General,* kule kwenye *interpretation Attorney General* hayupo. Kwahiyo, naomba aingizwe kule na tutumie *interpretation* iliyoko kwenye Katiba katika ibara ya 59. Tungeichukua hiyo, tuiweke kule kwasababu haijaonekana mahali popote kwenye ile *interpretation Attorney*

*General* katika kifungu hicho. Eneo lingine ambalo ningependa kuchangia ni ukurasa wa 12 katika ukurasa wa 12 ni muendelezo wa kifungu hicho cha 11 (4) pale chini kabisa ambacho kinasema kwamba, *in every case where the Controller and Auditor General makes a report under this section he shall notify the treasury.* Mtu ambaye anahusika na masuala haya mwenye madaraka ukiweka *treasury, treasury* pale ni nani hii kubwa sana lakini hapa nadhani ingekuwa ni *Pay Master General* au *PMG* ambaye amepewa *interpretation* kule kwenye *section* ya 3, kwenye hiyo badala ya *treasury.* Na popote pale inapotokea *treasury* iwe ni *Paymaster General* ndiye anahusika. Ndiye mwenye hiyo dhamana kubwa hiyo ya mambo ya kutoa amri za fedha kwamba zitoke hapa ziende pale, taarifa hii ishughulikiwe hivi. Sio ile kazi yake ya kawaida ile ya kiutawala ile ya Katibu Mkuu, wa fedha au *Treasury Permanent Secretary.* Eneo lingine ambalo nilikuwa nichangie ni katika ukursa wa 13 wa kifungu hicho cha 11 (7), kipo katika ukursa wa 13. Nilitaka kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge kwamba imeundwa Kamati mpya ya Hesabu za Mashirika ya Umma, haikuundwa Kamati ya Mashirika ya Umma. Kwahiyo, maelezo sahihi pale kwenye kifungu hicho cha 7 ule mstari wa *sentence* ya 4 pale katikati panapoanzia na *the Parastatal Organisation, s* iongezwe pale halafu iongezwe *Accounts Committee,* ndio hiyo iliyoundwa na nadhani kutumia Kamati ya Mashirika ya Umma ndiko kunakoleta muingiliano na Kamati za ki-Sekta kwamba wanakwenda kutizama kitu kimoja. Kamati za ki-sekta zinaangalia mipango na utekelezaji wa jumla. Hii *Public Organizations Accounts Committee* inakwenda kutizama hesabu zilizokaguliwa na *Controller and Auditor General* na zile *specific audits.* Kwa hiyo hapa ingewekwa waziwazi ili sisi tusiendeleze muingiliano huu kwenye Kamati.

Mchango wangu mwingine uko katika ukursa wa 25, kifungu cha 46 ambacho kilikuwa 47. Hapa kidogo naona kama kuna mchanganyiko kidogo, inakuwaje *Public Accounts Committee* ipewe jukumu la kuteuwa *Auditor?* Mimi nadhani twende na hizi *checks and balances. Public Accounts Committee* kazi yake nikutizama hesabu zilizokakuguliwa. Sasa Mkaguzi wa *Control ler and Auditor General* mimi napendekeza kwamba angeteuliwa na *Paymaster General,* yule ambaye anatoa *releases* za fedha ndiye amteuwe. Bunge lisiingie kwenye michakato ya ku *appoint* watu itakuwa kwa kweli tumeingia kwenye kazi nyingine, na hapa nadhani *Paymaster General* ana nafasi yake nzuri kabisa hapa ya kuweza kuendeleza kwamba ametoa *favour,* na *CAG* ana uhuru wake lakini kuna *checks and balances* kwa maana atateuliwa *Auditor* ambaye atakwenda kumkagua kwa hizi fedha alizopewa. Sasa *Public Accounts Committee* inakwenda kuangalia nini *Controller and Auditor General* amefanya kwenye hizo hesabu zake, sasa ikiwa tena huyohuyo ndio anateuwa *Auditor* itakuwa kidogo inaleta mchanganyiko. Kifungu kingine ambacho ningependa kukisemea ni kile cha 45 ambacho kwa sasa ni 44 ukurasa uleule pale juu, hiki nacho kinaleta mchanganyiko kidogo. Tuna Kamati za kisekta, tuna Kamati ya Fedha na Uchumi, *Finance and Economic Affairs Committee,* hiyo ndio ambayo ingepitia *estimates* na mapendekezo ya makusanyo ya mapato. Sasa hii kazi tena ukiipa *Public Accounts Committee* umewaleta mapema zaidi, wangojee hizo zikafanye kazi halafu waletewe hesabu, kwahiyo hiki kifungu nacho kingetizamwa hiki ili kisilete mwingiliano wa shughuli. Hiyo shughuli ya kuangalia *estimates* na *revenue* zinazoingia hizo ile Kamati ya kisekta ndiyo ifanye hizo kazi na Waziri wa Fedha, halafu *Public Accounts Committee* inangojea hesabu zimekaguliwa

baada ya matumizi. Tusichanganye vitu vingi kwa wakati mmoja tunaweza kujiletea matatizo.

Nitarudi kidogo kwenye ukursa wa 22 pale, kuna jambo ambalo nilitaka kulizungumzia. Katika kifungu cha 39 ambacho katika marekebisho ni 38 ukurasa wa 22, pale ambapo tunasema *the Public Accounts Committee, Local Authorities Accounts Committee, Parastatal Organizations Committee,* ambayo sasa mnasema inakuwa *Accounts Committee and any other Parliamentary Sectoral Committees as the case may be shall discuss the reports of the Controller and Auditor General.*

Sasa hapa tena tunaingiza *sectoral committee* kwanini? Kwasababu kuna mgawanyo wa madaraka vizuri sana kwamba *sectoral committee* zitashughulikia mipango, utekelezaji wa kawaida lakini hizi Kamati tatu *PAC, LAAC, POAC,* hizi zinashughulikia *Audited Accounts* na zile kaguzi nyingine maalum. Sasa hapa nadhani tusichanganye haya mambo, tukiyachanganya changanya sana haya yatatuletea matatizo. Kuna vitu vingine vidogo vidogo naona nikichukua hapa muda tutapunguza muda wa wenzangu kuchangia, nitakuja kuvidokeza wakati wa kukaa kama Kamati ya Bunge zima kwenda kifungu hadi kifungu. Ni vitu vingi vidogo vidogo. Kwa mfano kimoja hiki nadhani Mheshimiwa Waziri, angekiangalia ili akirekebishe, *Control and Auditor General* tuliyenaye sasa ni mwanaume lakini kuna uwezekano akaingia mwanamke, sasa humu ndani zimejaa *his, his, his,* kuna sehemu moja tu ndio wamesema *he or her. K*wahiyo, nadhani hili lingetizamwa ni la jumla hili. Nakushukuru sana na ninaunga mkono Muswada huu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, wakati wa chakula haya mapendekezo ya *section* 45, 46, 47, kayafanyie kazi na ningependa Mheshimiwa Shellukindo ushiriki kwasababu ni kweli kwamba *Committee* tatu ni *watchdog Committees. K*amati zingine ndio *Sectoral Committees* ndio maana unakuta hata Muswada huu haikuletwa *Public Accounts Committee* wala haikuletwa *POC* wala nini, imeletwa na *Sectoral Committee.* Kwa hiyo, mkaangalie uhusiano huu usilete kugongana kwenye sheria. Tunaomba ushiriki au ukileta *amendments* zako itakuwa ngumu, ukishiriki kule itakuwa vizuri zaidi. Tunaendelea na mchangiaji mwingine, Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, halafu Mheshimiwa Mwijage ajiandae, halafu mwingine ni Mheshimiwa Mwanawetu naye pia ajiandae.

**MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia Muswada ulio mbele yetu. Kwanza niishukuru Wizara kwa kuleta huu Muswada muhimu na ulikuwa unategemewa kwa muda mrefu ili tuweze kufanya mabadiliko katika ukaguzi wa mahesabu ya Serikali. Vilevile nipongeze hii hatua ya kuwapa uhuru kamili Ofisi ya *CAG* kuweza kukagua hesabu za Serikali bila ya kuingiliwa na mtu yeyote. Hii itasaidia sana katika kudhibiti fedha za umma ambapo sisi Wabunge ni wadau na ni majukumu yetu kuhakikisha kwamba pesa za wananchi zinatumika vizuri kwa maana ya *value for money.* Mimi kwanza nijaribu kusema kwamba miradi ambayo Serikali inapitisha na Wizara ya Fedha, inapotoa fedha zake kwenda kutekeleza miradi hii, kuna miradi mingine inachukua muda mrefu sana kwa kukosa fedha kwa maana ya kwamba kukatisha fedha zile za kwenda

kwenye miradi na hatimaye miradi hii inachukua muda mrefu na inakuwa inagharimu Serikali au ina gharimu fedha nyingi sana za wananchi. Utakuta mradi unaanza kwa 1,000,000,000/= kwaajili ya kucheleweshwa hatimaye kutokana na *inflation* na mambo mengi yanayojitokeza, miradi ile inapanda na kufikia mpaka kama 7,000,000,000/=. Nitatoa mfano halisi, tumetembelea mradi wa bwawa la Mugumu kule Serengeti. *Initial budget* ilikuwa ni *1.4 billion.* Mradi ule umechukua miaka 31 haujakamilika kwasababu kulikuwa hakuna *constant flow* ya pesa kwenye mradi ule na hatimaye mradi ule sasa gharama yake imeshafikia karibu 7,000,000,000/=. Sasa *un necessarily* tumeongeza gharama kubwa katika mradi wakati mradi ule ungegharimu fedha kidogo sana za wananchi lakini wakati huohuo wananchi wa eneo lile wameteseka kwa kiwango kikubwa kwa kutokukamilika mradi ule mpaka sasa kwasababu ya fedha kwenda katika miradi mingine. Lakini vilevile kuna miradi mingine ambayo imesimama kwasababu ya mkandarasi kushindwa kutekeleza ile miradi. Inafika pahala anapewa tenda, anachukua mradi, mradi ule anaushindwa kuukamilisha katikati anajiondoa, inabidi sasa kuwe na ucheleweshaji mwingine. Mimi niishauri Serikali sasa hivi kwamba Wakandarasi wa aina hiyo wanapojitokeza na wakashindwa kutekeleza ile miradi, wasipewe tena miradi mingine. Wanatuharibia mipango yetu ya maendeleo katika nchi hii. Na wakati mwingi sana wananchi wanalalamika na Wakandarasi wengi wazalendo wanalalamika wanasema kwamba hatupewi miradi, baadhi yao wanapopewa hii miradi wanashindwa kuitekeleza. Sasa kwa utaratibu huo Serikali itajiondoa katika lawama kwamba unapewa mradi umekushinda usiombe tena mradi ili uweze kuushughulikia. Hili ni tatizo la kuongeza gharama ya mradi bila ya sababu za msingi. Ninaiomba sana Wizara ya Fedha, na hasa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kusimamia jambo hili kuhakikisha kwamba hii miradi inayoanzishwa, Serikali itoe pesa kwa mujibu wa ratiba iliyowekwa na hatimaye ule mradi ukamilike mapema iwezekananvyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, iliongelewa hapa wawekezaji wanaokuja kuwekeza katika maeneo yetu Tanzania na hatimaye kwa mfano suala zima lililojitokeza kule Serengeti katika Hoteli ya *VIP*, sitaki nirudie. Lakini mimi niseme kwamba wale lazima wawe *summoned* waje mbele ya Kamati tuwaulize kwanini mumekataa Kamati ya *PAC* isije katika eneo lenu na hatimaye sasa baada ya hapo waigharamie wao wenyewe Kamati iende kule kwa gharama zao ili tukafikishe lile lengo ambalo kwamba sisi tulikuwa tunataka tulijue.

Mheshimiwa Spika, nikizungumzia *value for money* kwa pesa zinazotolewa na Serikali katika miradi, bado kuna tatizo. Wakandarasi wanaongeza gharama wanapokuta kwamba zile *estimate* walizofanya wao na wakashinda *tender* na jambo la kwanza tumeshalisema hapa la kuchelewesha fedha kwenda katika miradi limesababisha barabara nyingi zilizojengwa hasa zile barabara za kusini za kuanzia Mingoyo, maeneo ya Lindi kwenda mpaka Nangurukulu mpaka Somanga, zime *shoot* kutoka *initial estimate* na kwenda mara mbili yake, hili ni tatizo lingine. Kwahiyo tunaomba sana Serikali tusipoteze pesa za wananchi kwa kuchelewesha.

Kama Serikali inaona haina fedha za mradi sasahivi ni bora tusiingie mkataba mpaka tuwe na uhakika kwamba tumetenga fedha kamili kwa kiwango ambacho mradi

ule utatekelezwa na hatimaye uweze kutekelezwa vizuri na kupunguza gharama za mradi wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye ibara ya 30 katika muswada wa sheria pale inapozungumzia kwamba Serikali ni *share holder* katika miradi ya Serikali. Kuna miradi mingi ya Serikali ambayo imeanzishwa kwa ubia na wawekezaji. Na Serikali, nikiizungumzia Wizara ya Fedha, kwamaana ndio msimamizi wa fedha za nchi hii wanatafuta mapato kwaajili ya maendeleo ya nchi yetu katika maeneo mbalimbali. Lakini utakuta miradi ile ya ubia mingine inasimama ni kwasababu tu ambazo mimi naziona sio za msingi. Kwamba tunapotaka sasa kuzalisha, kwa mfano *gas.* Nichukue mradi wa *Mnazi Bay*, *potential* ya *gas* iliyoko pale katika nchi yetu inaweza ikatutosheleza kwa miaka 600 ijayo. Ule mkataba ni mzuri, 30% mwekezaji 70% Serikali.

Ule mkataba ni mzuri 30% mwekezaji 70% Serikali hivi ni sababu zipi Serikali isitumie nafasi ile juu ya ile gesi tukaweza tukapata mapato *income* aidha kwa kuuza gesi aidha kwa kuitumia ile gesi katika mambo mbalimbali katika viwanda vyetu ndani ya nchi na Watanzania wenyewe wakapata miradi wakatumia gesi ile hivi sasa tunatumia gesi ya kutoka Songo songo ambayo inatugharimu kweli kweli ambayo sasa inatumika katika kiwanda cha *cement* pale Dar es Salaam kwa sababu mikataba mibaya. Je, huu mkataba wa Mnazibay Serikali inafanya nini? Kutumia gesi ile yenye *potential* kubwa kuingiza pesa katika nchi hii hatimaye tupate maendeleo wakati bandari ya Mtwara iko pale *natural harbour* na ile gesi iko palepale gharama zake labda ni kutengeneza bandari na hatimaye peke yake vile visima ni *collector* ya kutosha kwa ajili ya kukopa pesa na hatimaye kujenga *infrastructure* kwa ajili ya kuuza ile gesi nje na gesi nyingine itumike katika kuzalisha umeme na hatimaye kanda yote ile ya Mtwara *corridor* iweze kuinuka na hatimaye ni kuongezamapato katika nchi na hatimaye mapato yale yaweze kutumika kwa faida ya wananchi. Lakini mpaka sasa hivi gesi ile imebaki *dormant* haiendelezwi, hakuna kinachofanyika kila mmoja hajui nani mwenye maamuzi ya mwisho. Hili limetusikitisha kwa kuona kwamba tuna *potential* na kuacha tu gesi na mambo mengine tuna *agriculture* hatuna utalii na mambo ni hayo hayo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Spika, Muswada, hili linahusianaje na Muswada? Hebu tusaidie kidogo linahusianaje na Muswada.

**MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, lengo langu nilikuwa nataka kusisitiza kwamba *Controller* na *Auditor General* anapokagua mahesabu ya Serikali na mahesabu haya saingine tunapata matatizo katika kukamilisha miradi ni kwa sababu ya ukosefu wa fedha. Sasa nilikuwa najaribu tu kwamba mimi nataka kusema kwamba fedha zipo lakini Wizara ya Fedha yenyewe haifuatilii katika haya mambo ya kupatikana kwa fedha kwa ajili ya ufanisi wa mambo ya maendeleo kwa sababu *Controller and Auditor General* kazi yake ni kudhibiti fedha hizi za Serikali ziwe zinatumika vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuuliza wakati fedha zinapokaguliwa na *Controller and Auditor General*, *fedha* za bajeti na bajeti mwaka wa bajeti

unapomalizika kuna pesa zinazobakia zinatakiwa zirudi kwa mlipaji mkuu wa Serikali lakini taarifa haitolewi kwa mkaguzi mkuu wa mahesabu ya Serikali juu ya fedha hizi zinazorudi na hatimaye fedha hizi zinaporudi zinajumuishwa vipi katika Bajeti mpya ili mkaguzi mkuu wa hesabu za Serikali apate kujua ni kiasi gani kimebakia na kimerudi kiasi gani na ngapi zimerudishwa tena katika Bajeti. Hili ni kasoro ambalo tumeliona inabidi Serikali upya suala hili ili tupate taarifa kamili juu ya Bajeti na mkaguzi na mdhibiti mkuu wa hesabu za Serikali anapokagua ajue ni pesa gani ngapi zimebakia na hatimaye zimerudi kwa mlipaji mkuu na hatimaye ziingie katika taarifa ili hatimaye tujue mahesabu kamili yanavyokwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa na hayo machache ya kuchangia na ninaunga mkono Muswada huu ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru mimi nitachangia sehemu chache tu kwa sababu mambo mengi hotuba ya kambi ya upinzani imeshatosheleza.

Niko kwenye Kamati ya *PAC*, nimesikitishwa na mambo mengi sana kuhusu mwekezaji huyu na nitaomba Mheshimiwa Waziri aweze kutueleza mambo machache yaliyotukuta. Kuna suala hili la huyu mwekezaji kuchukua wanyama wetu kuwapeleka nje nitaomba nilijue.Suala lingine ni suala la wafanyakazi waliobinafsishwa na ile Soronera wafanyakazi wanapata mateso makubwa sana. Nitapenda kujua hao wawekezaji wanapokuja hapa wanakuja kunyanyasa wananchi wetu au wanakuja kuweza hawaji kuwekeza wanakuja kuwanyanyasa. Ni matatizo makubwa sana tuliyoyaona kwa wawekezaji ni kwa sababu mikataba mingi haipitii hapa Bungeni mimi naomba mikataba yote ya wawekezaji ipite hapa na iwe na sheria ya kuwalinda wale wafanyakazi watakaoajiriwa na hao wawekezaji. (*Makofi*)

Tumekuta mzee analia hiyo sehemu ya hoteli Soronera alipewa nauli tu ya kwenda nyumbani peke yake hakulipwa chochote kile na mpaka sasa hivi anashinda pale kwenye hoteli, kweli huo ni uungwana Naibu Spika? (*Makofi*)

Suala linginge naona hiki kiburi walichonacho kufika mahali kutuzuia sisi kuingia mle kwenye hoteli wana kiburi, nitaomba Mheshimiwa Waziri kinatoka wapi kama kiko kwenye Mkataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine kuna sehemu moja inaitwa Ikoma. Hiyo sehemu iko Serengeti wanasema kwamba kuna madini pale wanazuia na watu kwenda sasa tusipoenda sisi Watanzania nani atakwenda tena. Nani atakwenda kuangalia mali zetu.Matatizo ya wawekezaji yanatokana na sisi wenyewe. Mimi nilikuwa nimemwomba Mheshimiwa Mwenyekiti Cheyo nikasema twende atupige ili ijulikane kwamba ametuzuia sisi. Lakini wenzetu wakina Rished Abdallah wakasema hili suala tulipeleke mpaka Bungeni tukalijue kwa sababu labda kuna kitu kilichopo ndani yake wamekificha kile kilichopo humo ndani sasa tunaomba twenda pale tukakione hicho wanachozuia au Waziri mwenyewe atuongoze ndiyo atupeleke pale wampige yeye atutangulie ndiyo tujue labda kuna matatizo ndani. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge hapa yuko Waziri wa Fedha kwa Muswada huu wa *audit.* Hayo mnayozungumza nadhani yako kwenye Wizara ya Maliasili na Utalii. Kwa hiyo, ukisema Serikali utakuwa ume-*cover* yote ukisema Waziri huyu aende kule hawezi sio mwenyewe sasa sema Serikali, kwa sababu ukisema Serikali watajijua wenyewe ni nani Waziri anayehusika.

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante lakini ninalolisema sio kusema namsema Waziri peke yake hata Serikali inasikia kwa sababu Waziri yuko Serikali wataambizana wao wenyewe. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa nakuelekeza jinsi unavyozungumza Muswada huu ni wa *audit* mimi nikipenda naweza kukuambia usiseme kwa sababu huzungumzi habari ya Muswada huu nimekuacha useme. Kwa hiyo, *refer* kwa Serikali sio kwa Waziri huyu Waziri Muswada wake ni huu wala hawezi kujibu haya mnayosema kwa sababu hayamhusu katika hili. Kwa hiyo, sema kwa Serikali kwa sababu Serikali itajibu hatubishani tunakuelekeza kwa sababu ukimwambia huyu hawezi kujibu haya humu hayamo.

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo umeshanifanya mpaka nisahau niliyotaka kusema ahsante sana. (*Kicheko*)

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii mimi nina suala moja tu katika Muswada huu kwanza naunga mkono kwa huu Muswada kuwasilishwa leo hii hapa.

Ninalotaka kuzungumza kuhusu ukurasa wa 18 kifungu cha 28 ambacho kinasema *the controller and audit general shall for purpose of the establishing the economy efficiency and effectiveness of any expenditure or use of resources of intuitive inquire examine investigate and report in so far as he considers necessary on* kuna vipengele vinne hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa mimi kuna suala ambalo kushauri hapa mimi niko kwenye Kamati ya *POC* na katika kaguzi zetu sehemu nyingi tumekuwa tukiangalia utakuta maeneo mengi wanato hati safi wakati hayo maeneo yana matatizo kibao ambayo hayastahili kupata hati safi. Kwa hiyo kwa kipengele hiki nilivyoangalia natoa tu msisitizo kwamba hili eneo liangaliwe na lifanyiwe kazi kwa umakini.

Nitatoa mfano mmojawapo au mifano miwili ambayo inaonyesha kwamba kaguzi nyingine zinatoa hati safi bila sababu ambazo hazistahili kupewa hati safi mfano kuna Halmashauri ya Kilwa ambayo pia katika wenye wakaguzi ilifanya matatizo ambayo mtu ambaye anakusanya mapato alinyofoa makaratasi.

Lakini kila wakati inapokuja kaguzi inaonekana ina hati safi. Mfano mwingine tena nitachukulia mfano wa *EPA* nao, *EPA* kila mtu anaelewa matatizo gani lakini humu wote ukiangalia utakuta kuna hati safi zimepewa. Kwa hiyo, kwa kipengele hiki cha 28 napenda kutoa msisitizo kwamba kiangaliwe na watu wafanye kazi kulingana na hali

halisi inayotakiwa kufanya kazi na sio kupeleka peleka tu kwa sababu ili mradi ukaguzi umepita.

Kwa hiyo mimi la kwangu lilikuwa ni hilo tu kwamba maeneo mengi yanakuwa yanapewa hati safi wakati kuna matatizo makubwa ambayo yanasabisha wasipate hati safi na hawana haki ya kupata hati safi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. (*Makofi*)

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuwa msemaji wa mwisho kwa mchana huu. Mimi naunga mkono na nasema Muswada huu ulichelewa sana Serikali inapanga matumizi, Serikali inapanga Bajeti, Wabunge wanapitisha lakini usimamizi wake unakuwa ni mdogo sana kwa sababu sheria hii ilikuwa haijaja Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutoa mfano, mahesabu yanapotolewa ni kwamba huko nyuma wakaguzi wanakagua hesabu hawakagui je, zile pesa zimefanya nini? Wanakagua je, pesa zime-*balance* au hazija-*balance*. Kwa hiyo, mfanyakazi anasema nimepata shilingi milioni 100, milioni 100 nimezitumia kwa kununua vitu kadha wa kadha. Lakini inatakiwa wakaguzi waende kuona je, zile mali zilizonunuliwa zinalingana na zile pesa zilizotolewa? Sheria hii sasa hivi inampa nguvu Mkaguzi wa Hesabu za Serikali aweze kuajiri watu ambao wataenda kukagua yale maeneo ambayo zile pesa zimetumika. Je, hizi pesa zimetumika sawa sawa? Kama ilikuwa ni shilingi milioni 200 kujenga nyumba. Je, hiyo nyumba ni ya shilingi milioni 200 kweli? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo ninamwomba mkaguzi aliangalie sawa sawa ni manunuzi ya Serikali, nani anaamua gari ya Serikali inunuliwe ya milioni 100, au milioni 60, au milioni 40? Haitoshi tu kusema nimenunua gari ya milioni 60. Kwa nini wewe ulipanga kununua gari ya milioni 60? Je, ya milioni 40 haikutosha kufanya kazi hiyo. Kwa hiyo, lazima Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali aweze kuona je, Serikali inatumia pesa zake vizuri? Maana pesa ndio inayoleta maendeleo kama wanapelekewa wanatumia tu wanavyotaka, hatuwezi tukapiga hatua. Naomba nizungumzie kazi ambazo hizi Idara za Bunge, Kamati za Bunge zinazofanya. Kuna Kamati ya Fedha za Serikali, Kamati hii inapaswa kuangalia je, zile pesa ambazo Serikali imetoa kwa mashirika yake, Serikali imetoa kwa Wizara zake je, zimetumika kama ilivyopaswa kwa kushirikiana na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kwa hiyo, Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anapaswa kuwa chini ya Bunge maana anafanya kazi ambazo Bunge ndilo liliidhinisha zile pesa. Kwa hiyo, tunamwambia hebu nenda katuangalie. Je, zile pesa tulizoidhinisha ni kweli zimetumika kama inavyopaswa?

Kwa hiyo, Kamati hizi zinapoamua kutembelea miradi ya Serikali ni lazima ziheshimiwe. Kamati hizi zinapotembelea, Bunge limetembelea na mojawapo ya kazi ya Bunge ni kusimamia Serikali, Wabunge wamekuja hapa Bungeni kwa kuchaguliwa na wananchi ili waje wasimamie shughuli za Serikali na waisimamie Serikali ifanye kazi kwa mujibu wa sheria na Serikali iko kwa niaba ya wananchi. Kwa hiyo, Bunge

linapoamua linaamua kwa niaba ya wananchi na Serikali lazima itekeleze kwa niaba ya wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, imenisikitisha sana kwamba Kamati ya Hesabu za Serikali kwa kutumia pesa za Serikali imeenda mpaka Grummet ambapo hoteli ya *VIP* ipo wanafika pale wako na maofisa kutoka Ofisi ya *CAG*, Mkaguzi Mkuu wa Serikali, wako na maofisa kutoka *Tanzania National Parks* mwekezaji wa hoteli hiyo anasema hamuwezi kuingia mtasumbua wageni. Kwa masikitiko makubwa mimi nasema ni dharau kubwa. Dharau kwa Serikali, dharau kwa Bunge, dharau kwa wananchi. Wawekezaji wa namna hiyo kweli tunawahitaji? Kama mwekezaji anaweza kudharau Bunge. Je, wale wananchi wanaomzunguka pale atawaambia nini? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Atawanyanyasa kweli kweli.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Naibu Spika, na ni kweli huyo mwekezaji taarifa nilizonazo ni kwamba ana jeshi ambalo liko linatembelea maeneo yake. Amepata Ikorongo *Game Reserve* na Grummet *Game Reserve*. Kwa hiyo, Serikali imemruhusu awe na askari kule, askari wa kwake askari hao wananyanyasa wananchi. Mwekezaji huyo alitaka vijiji vile vihame, vijiji vile vimeenda mahakamani wakashinda. Kwa hiyo wakaruhusiwa kuendelea kukaa pale na matokeo yake sasa anatumia askari kuwanyanyasa. Sasa ninaiomba Serikali, ni wajibu wake hakuna mtu yeyote anaruhusiwa kuwa na jeshi lake. Kama ni kulinda Ikorongo *Game Reserve* na Grummet *Game Reserve* Serikali ipeleke askari kule siyo yule mwekezaji awe na askari wake. Ikorongo *Game Reserve* imepakana sana na Bunda na Grummet ndio iko Bunda na Ikorongo iko Serengeti lakini amepewa huyo mtu mmoja kumiliki zote. Hataki wananchi watembelee maeneo yale, huyo bwana mimi nilikutana naye New York mwaka jana, ni rafiki wa Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kiburi chote alichonacho ni kiburi cha Serikali. Lakini Serikali imewekwa na wananchi lazima ifanye kazi za wananchi na sisi Bunge tunaagiza sasa Serikali ifanye kazi za wananchi. Huyo mwekezaji kama ni rafiki wa Serikali ametukosea sana. Kwa hiyo, hana tena sifa ya kuendelea kuwekeza pale. Kwa hiyo, ninaisihi Serikali tena ningeomba Serikali itoe tamko kuhusu hilo na Kamati ya Hesabu za Serikali tumwite aje akajieleze imekuwaje mpaka akadharau Serikali kwa kiasi hicho. Kwa sababu kudharau Bunge ni kudharau Serikali ni kudharau wananchi wa Tanzania ambao ndio wangepaswa kufanya kazi kwa niaba yao. Kwa hiyo, ndugu zangu mimi ninaliomba Bunge hili, ni Bunge la kisasa, Bunge limeshabadilika siyo lile Bunge la miaka iliyopita. Ni Bunge ambalo linataka kufungua ukurasa upya. Bunge ambalo linataka kutenda haki kwa Serikali na kwa wananchi wake. Serikali vile vile lazima itende haki kwa Wabunge na itende haki kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nirudie kama huyo mtu ni rafiki wa Serikali na ameshatukosea kiasi hicho ni kwamba amekosea Serikali ambayo ndio rafiki yake. Kwa hiyo, Bunge liazimie kwamba itolewe tamko huyo mtu afanyweje. Maana kama

ameweza kudharau kiasi hicho wale walioko kule Grummet, kule Ikorongo ni tabu gani wanapata na kwa kutumia jeshi hilo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache naomba niunge mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu utaratibu.

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu Kanuni ya 68, Mheshimiwa Mbunge kanuni ya 68 kifungu namba 1 (1). Mheshimiwa Mbunge ametaja mara kwa mara katika maelezo yake kwamba mwekezaji huyu ni rafiki wa Serikali, nimejaribu kujiuliza ana maana gani pengine afafanue zaidi hili kwa sababu Serikali haina urafiki ni uhusiano tu na wawekezaji. Pengine angetufafanulia urafiki huu maana yake ni nini?

**NAIBU SPIKA:** Tukishaletewa utaratibu anayeomba utaratibu anataja kifungu kinachohusika akishamaliza ni juu ya Spika kusema sasa wewe useme au atajibu yeye. Sasa tunakutaka utueleze tunataka ufafanuzi tu, urafiki wa huyo mtu na Serikali ni kitu gani hicho?

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nasema huyu ni rafiki wa Serikali kwa kuwa mwaka jana nikiwa New York kwenye *dinner* ambayo kiingilio ilikuwa ni dola 1000, kwa hali niliyoiona ambapo maofisa wa Serikali walikuwepo ilionyesha kabisa huyu mwekezaji ana uhusiano wa karibu na Serikali na picha ninazo kama nikitakiwa maelezo zaidi ninaweza nikatoa. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge kama nilivyokuwa nimejaribu kumshauri Mheshimiwa Mwijage hapa unapoongea ukisema Serikali inatosha. Kwa hiyo, mnachokitaka ni maelezo kwa nini aliizuia Kamati ya Bunge kufanya kazi zake na ndio maana nikamtaka Mheshimiwa Mwijage asimwelekeze zaidi Waziri huyu kwa sababu hana jibu.

Lakini mkisema Serikali yuko Waziri wa Nchi na wengine watajipanga ni nini hiki kilichotokea, kwa sababu huyu ataendelea kushughulikia Muswada wake huu, humu ndani utakuta kukataliwa hawa jamaa kutokuona pale halimo humu katika Muswada.

Lakini *issue* iliyotokea kwa Kamati yetu na Kamati yetu muhimu. Kwa hiyo, Serikali lazima iji-*address* na hilo maana ukiingiza urafiki wa Serikali, Serikali ni chombo maalum au ni nani huwezi kusema ndio maana nasema ukisema Serikali inatosha hawa lazima walete maelezo na juu ya hapo Serikali inaweza kujibu ikipenda. Lakini mngetaka nguvu zaidi nyie mngeleta hoja hapa kwamba suala hili wote mzingatie moja.

Lakini hivi Waziri anaweza kujibu, Serikali inaweza kujibu ikipenda wakati wake kwa sababu hakuna uzito. Uzito lazima utokane na hoja ambayo mnasema sisi wote Wabunge tumeamua kuzungumzia suala hili na kama kuna maamuzi yatakuwepo hapo mnaamua kama Bunge. Hapo mmetoa mawazo yenu nyie wote, mazuri tu. Kwa hiyo, Serikali itaweza kujibu lakini atakapojibu Waziri wa Fedha hilo hatataja siyo sehemu ya Muswada. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, nadhani waliokuwa wanachangia katika orodha yangu wameisha na muda pia kwa mchana huu umeisha. Ningependa Waziri wa Fedha, mtoa hoja, hoja zilizotolewa na Wabunge kuhusu mabadiliko mbalimbali ndani ya Muswada mkayafanyie kazi vizuri mchana huu na ikibidi kama mnataka msaada mnaweza kuomba kwa sababu tunataka tukifika tusiwe na mahali watu wanashindwa kueleza.

Kwa hiyo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

*(Saa 6.58 Bunge liliahirishwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Tulikuwa tumebakia na mchangiaji wetu mmoja Mheshimiwa Waziri wa Elimu. Wengine wana majina marefu! Mheshimiwa *Prof.* Jumanne Maghembe, yeye alishakuwa Waziri wa Maliasili zamani kabla ya mabadiliko, kwa hiyo, maneno mengine mliyozungumza atakuwa na maelezo.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nikushukuru sana kwa kunipa nafasi kuchangia katika Muswada huu ulio mbele yetu. Kwanza, ninaipongeza Wizara ya Fedha kwa kutayarisha Muswada huu ambao kwa kweli ni wa kihistoria hapa nchini kwetu, ni Muswada mzuri na umekuja kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nia yangu ni kutoa maelezo mafupi juu ya maelezo na hotuba zilizotolewa kuhusu Hoteli ya Sasakwa iliyoko Gurumeti. Hoteli hii ya Sasakwa iko Gurumeti na inahudumia wageni wanaokuja Gurumeti na Serengeti ya Magharibi na Ikorongo Mkoani Mara. Imejengwa kwa uwekezaji wa dola milioni 90 na ni hoteli ya nyota saba.

Hoteli za kawaida zinakuwa ni nyota moja mpaka nyota tano, zingine chini ya hapo zinakuwa ni *guest houses;* lakini hii ni hoteli maalum iliyojengwa kwa kiwango cha nyota saba na katika mwaka 2006 katika hoteli 20 nzuri duniani, hoteli hii ilikuwa ni moja ya hoteli hizo. Pia katika mwaka huo ilikuwa ni hoteli bora kupita zote katika Bara la Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoteli hii ina vyumba 15 tu na imejengwa kwa ajili ya wakuu wa nchi *(needs of state and government)* wanaokuja kwenye nchi yetu kwa ajili ya utalii au kwa viongozi ambao wanahitaji hoteli ya ubora nyota saba. Kuwa na nafasi katika hoteli ile, lazima uchukue vyumba vyote na gharama yake kwa siku ni dola 35,000 za Marekani kwa kukodi hoteli yote kwa siku. Hoteli ile ina *booking* kuanzia tarehe 1 Januari mpaka tarehe 31 Desemba. Ukitaka nafasi pale inabidi u-*book* kwa mwaka mzima mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, madhumuni ya hoteli ile ni kuwapokea na kuwapa mahali pa kukaa wakuu wa nchi wanaokuja kwa madhumuni ya kupumzika au kwa utalii hapa Tanzania, Wakuu wa Mashirika makubwa ya Kimataifa ambao pia wanahitaji ulinzi na wanataka kufanya utalii hapa nchini kwetu na Bodi za mashirika makubwa ya Kimataifa ambayo yanahitaji kufanya mikutano yao katika maeneo ambayo yana utulivu na ubora ambao hauna ulinganisho katika dunia hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikitoa mfano, Mheshimiwa Thabo Mbeki Rais wa Afrika Kusini alikaa pale mwezi Desemba, 2006 na baada ya hapo alikuja tena mara nyingine, Naibu Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje wa Marekani naye ni mmoja wa wageni ambaye najua alikuja pale. Lakini pia, kumekuwa na mikutano ya Bodi za Wakurugenzi nyingi kama Bodi ya *Time Warner* ya *CNN* na Bodi ya shirika kubwa la *TATA* wamefanya mikutano hapo.

Mwenye shirika kama TATA ni mtu ambaye ni wa pili duniani kwa utajiri na *celebrity* wengine na wakuu wa nchi mbalimbali wamekuja nchini kwetu wakakaa sasa kwa namna yoyote wasingependa kutangazwa kwamba wako nchini kwa sababu wamekuja kupumzika.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha muhimu ni kwamba wanatoa taarifa kwenye Serikali na Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje inajua na inaweka Maofisa wa Serikali katika eneo lile pamoja na ulinzi unaolingana na ugeni ambao uko pale. Sasa kwa kuwa kunakuwa na wakuu wa nchi, wakati mwingine kunakuwa na wakuu wa nchi na *delegation* zao ambao wako pale, ulinzi unakuwa mkali kwa kweli. Kwa hiyo, wale ambao wanapenda kwenda kutembelea pale ni lazima watoe taarifa na hasa kama wanataka kwenda kule na kuna wakuu wa nchi wakielezwa na Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje, basi wapewe ruhusa maalum na Wizara inayohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa wageni wanaokuja pale ni *entourage* au ni Bodi nzima wanatumia kila kitu, yaani wananunua huduma ya kila kitu kilichoko pale. Kwa hiyo, kwa kawaida hawategemei wageni wale ambao wanakuja tu *casually*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu kushauri kwamba sisi watu wakubwa tunapokwenda kwenye maeneo kama haya, ni vizuri tutoe taarifa na tujue kama kuna nafasi au hakuna, ili tuweze kwenda na kama ni *convenient* na kama ni lazima twende, basi tutafute utaratibu wa kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kutoa taarifa kidogo kuhusu mapato na matumizi ya hoteli ile. Tangu ile hoteli imeanza, hakuna fedha ambayo imepatikana pale

ambayo imetolewa nje ya Tanzania.  Fedha zote ambazo zimepatikana zinalipia miradi ya maendeleo katika Wilaya ya Serengeti na katika Wilaya ya Bunda kujenga visima vya maji, kujenga Shule za Msingi, Shule za Sekondari na kulinda maliasili ya wanyamapori, tangu imeanza jumla ya dola milioni 36 zimetumika katika miradi mbalimbali ya maendeleo katika eneo lile.  Aidha, kampuni ile imetoa *scholarship* 20, mbili kwa kila mwaka kwa Watanzania kusoma katika Vyuo Vikuu vya Marekani, kusomea Elimu ya *Conservation* katika Vyuo Vikuu vya Marekani kwa kiwango cha Uzamili au *Master of Science.*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitoe tu maelezo kwamba sio vizuri kwa kweli, kwa namna utamaduni wetu ulivyo, kuambiwa huwezi kuingia hapa! Lakini kwa jinsi ambavyo tuna-*interact* na mataifa mengine hasa katika utalii na kukubali kwamba wageni na wakuu wa nchi waje kwenye utalii ni vizuri tuelewe kwamba katika kufanya hivyo wakati mwingine tunaweza kupata *inconvenience.*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini *some of these inconvenience* zinatokana na mkakati wa kuongeza mapato katika sekta hii ya utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, yangu yalikuwa ni hayo mafupi.  Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii nichangie Muswada huu ambao umeletwa kwa dharura.

Mheshimiwa Sitaki kuwarudisha Waheshimiwa Wabunge tulikotoka, lakini kwa jambo ambalo linaonekana linatuletea matatizo makubwa kikatiba iwapo Muswada utapita. Muswada huu kama ulivyoletwa umetokana na Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo inazungumzia kazi ya *CAG* kwa undani kabisa.

Sasa ukiangalia Muswada ulivyoletwa inaonekana haugusi Zanzibar, maana ripoti ya leo ya *CAG* tuliyonayo haizungumzii Zanzibar na Zanzibar imekuwa ni chanzo cha matatizo makubwa katika muungano wetu miaka nenda rudi hivyo hivyo! Nataka kujua, hii sheria ita-*extend* kwenda Zanzibar au hapana? Kama hai-*extend* Zanzibar na fedha zinazokwenda Zanzibar zinatoka kwenye *consolidated fund* chini ya Ibara ya 136 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tunakwenda wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ndio maana ukiangalia *exemption* za Zanzibar ni nyingi mno kuliko za Bara.  *Collection* ya kodi Zanzibar ni ndogo sana, inabidi muungano ndio uchangie kule na *CAG* hana makucha kule, yuko hapa anatanda hapa *mainland* tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kujua kama kweli sheria hii ita-*extend* Zanzibar.  Kama ita-*extend*, basi tuseme hivyo wazi wazi kwamba "*these act shall extend to Zanzibar.*" Vinginevyo, kwa kuwa iko *silent* ni ya kwetu tu, tunapeleka wapi Jamhuri hii? Wanaotozwa kodi wako hapa na fedha zinakwenda kutumika Zanzibar na Zanzibar

*CAG* hana meno, tunafanya nini? Sina mengi isipokuwa nilitaka kujua kama kuna maelekezo kuhusu suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana, mmechangia, siyo kwamba umetaka uamuzi wa Spika, mmechangia watawajibu. Sasa tulishamaliza wachangiaji wote na tuanze kupata majibu kutoka kwa Naibu Waziri wa Fedha.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (OMAR Y. MZEE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza na mimi nataka nikushukuru kwa kupata fursa hii ili nami nichangie Muswada ulio mbele yetu. Lakini kabla sijachangia na mimi naunga mkono hoja mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nichangie Muswada uliowasilishwa mbele yetu kwanza kwa kujenga misingi ili sote tuweze kufahamu na kuelewa kwa nini tumewasilisha Muswada huu. Nasema hivyo kwa sababu Wajumbe wengi wamegusa Katiba na baadhi wamesema ipo haja ya kuifanyia marekebisho na baadhi wamesema kwa sasa twende taratibu.

Kwanza Katiba yetu Ibara ya 143 imetupa nguvu na uwezo wa kutunga Sheria ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Nasema tumechelewa! Lakini kama hilo halitoshi, mwaka 2006 wenzetu wa *AFROSAI* walikuja Tanzania kututathmini huu uzuri ambao tunaouzungumza wa Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Kufanya Mahesabu na kuyawasilisha na kuyatoa kwa wakati ukoje. Walipowasili, cha kwanza kabisa waliuliza:

“Huyu Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu ya Serikali yupo kwa mujibu wa sheria? Tulipomwambia hana sheria, *classification* ambayo tumepewa ni wa mwisho. Juu ya uzuri wote ambao tulikuwa nao, tukasema kama hivyo ndivyo, mwaka 2009 wenzetu wanakuja tena kututathmini, tukasema kwanza tutunge sheria ili Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu awe na sheria yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitajaribu kujibu baadhi ya hoja, hata Zanzibar wana sheria yao ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu. Sisi Jamhuri ya Muungano hatuna. Tulikuwa tunatumia *the Public Finance Act* kwa mambo yote ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu. Kulikuwa kuna mapungufu.

Kwa hiyo, tulisema tuilete sheria hii lakini tulijua kwamba, sheria hii tunaileta lakini kwa kuwa hesabu haianzi kwenye kumi, ila inaanza kwenye moja. Kwa maana hiyo, tulisema twende taratibu. Hatukutaka tuje na marekebisho ya katiba kwa sababu hesabu inaanza moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katiba inatutaka tuwe na sheria, sheria hakuna, ndio tukasema wacha kwanza tuje na sheria. Kwa hiyo, tumeelewa, tumefahamu kwamba Waheshimiwa Wabunge baadhi wameeleza juu ya wasiwasi wao uwasilishaji wa ripoti ya *CAG*. Nataka niwaambie kwamba marekebisho yoyote utakayoyafanya maana yake utaigusa Katiba kwa wakati huu.

Tulisema, kwa sababu hakuna dosari *CAG* kumaliza ripoti yake na kuiwasilisha kwa Rais na Rais atampa mtu atakayemwona anafaa wa kuiwasilisha Bungeni, tulisema tufuate hiyo kwa sababu hakutakuwa na dosari yoyote kwa sababu Bunge litaipata ripoti ile kwa wakati muafaka kama Katiba ilivyoweka.

Kwa hiyo, hoja hii ilizungumzwa na ilijadiliwa sana na Waheshimiwa ambao naomba niwataje wachache tu. Mheshimiwa Fatma Fereji, Mheshimiwa *Dr*. Wilbrod Slaa, Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa George Simbachawene na sasa hivi Mheshimiwa Nimrod Mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema kwamba sheria hii itakapokuwepo itatupa nafasi kuanza kuondoka kuwa wa mwisho angalau kufikia ile hatua ambayo na sisi tunaitegemea. Lakini tulizungumza kwa umoja wetu, kwa nguvu zetu tunataka kumpa meno Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu. Sasa hivi nataka niseme amekuwa kama mzee ana meno mawili ya kutafuna, Muswada huu ndio utakaompa meno.

Kwanza, nataka nitoe maelezo mafupi tu au nionyeshe vifungu au vichache, hivi sasa ripoti za *CAG* zinaonekana kama ripoti za kawaida tu lakini sheria hii mlipaji mkuu *paymaster general* atalazimika kujibu hoja za *CAG* kama yeye atalazimika kujibu hoja za *CAG* kuna *Accounting Officers* katika maeneo mengine atawabana. Kwa hiyo, tunasema kwamba tutapunguza upotevu wa fedha zetu sivyo kama tunavyokwenda sasa hivi, lakini kama hilo halitoshi sheria ya fedha hivi sasa mnavyoiona *section 26* mpaka *section 42* ndio inayomweleza Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Shughuli za Serikali, haijatoa *provision* ya kuandaa kanuni kwa ajili ya Mdhibiti.

Sheria hii itatoa *provision* hiyo na zitaandaliwa kanuni. Tumezungumza mengi humu ndani kuhusu kuimarisha hiki na hiki, mengi yatajitokeza katika ile kanuni ambayo itakayotungwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama hilo nalo halitoshi, Sheria ya *Public Finance* inasema: “Waziri wa Fedha ndiye atakayeteua Mkaguzi wa kumkagua *CAG.”* Hapa pana mawazo yanapingana, *CAG* anamkagua Waziri wa Fedha, Waziri wa Fedha ateue amkague *CAG*, pana mgongano wa mawazo. Tukasema haiwezekani tuweke katika sheria hii. Bunge liingie kwa kupitia Kamati zake wateue mkaguzi kwa ajili ya Ofisi ya *CAG*. Kwa hiyo, utaona kwamba hapa tunataka nini. Tunachokitaka katika Muswada huu ni kuhakikisha kwamba suala zima la upotevu wa fedha za umma kama hatulimalizi tunalipunguza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo tulilizungumza katika asubuhi hii wakati tunachangia na limechangiwa sana na Mheshimiwa John Cheyo na Mheshimiwa Athumani Janguo na Waheshimiwa wengineo, suala la kwamba *Auditor and Controller General* hivi sasa anakuwa kama ni *post-mortem*, watu wanafanya uharibifu yeye anakwenda mwisho kukagua, anatuambia hapa pameharibika. Tukasema katika sheria hii, tutumie *Internal Auditor Reports*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa *Internal Auditors* kwa sababu wana-*produce quarterly reports* watakuwa wanaziwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu. *Suppose* unakagua *project, project* haiwezi kumalizika kwa miezi mitatu. Kwa hiyo, unaweza ukajua hapa patakuwa na upotevu na *Controller and Auditor General* anaweza akachukua hatua haraka sana. Kwa hiyo, katika sheria hii, tunacho hicho kipengele na kitaweza kutusaidia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo lilizungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wengi, Mheshimiwa Zubeir, Mheshimiwa Estherina Kilasi na wengine, walitaka *Controller and Auditor General* a-*audit* mashirika hata kama tuna hisa chini ya *50 percent.* Nasema hivi, kwanza ulimwengu mzima haufanyi hivyo. Anayeteua *auditor* wa ku-*audit* lile shirika ni yule ambaye ana *share* nyingi, hata sisi Serikali tukitaka, bodi ndio inayoteua, wewe huna *share* nyingi kwenye bodi huwezi ukashinda.

Kwa hiyo, tumesema sisi kwa sababu msajili wa hazina ana uwezo na kiutaratibu, ndivyo ilivyo wa kupata sheria za *auditor* kwa yale mashirika yote ambayo Serikali ina hisa, tukasema katika sheria hii tuangalie kama kuna uwezekano wa kuongeza kifungu ambacho hii ripoti iliyokuwa *audited* kwenye lile shirika atapatiwa *Auditor and Controller General* ataipitia na kutoa ushauri kwa Serikali juu ya shirika linalohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine limezungumzwa na Waheshimiwa wengi juu ya kutangazwa kwa sheria hii na kuanza kufanya kazi na kanuni, nataka niseme tumewasilisha Muswada huu wa sheria hii kipindi hiki, Muswada huu wa Sheria kwa sababu ya umuhimu wake na ninadhani tukimaliza kuipitisha Mheshimiwa Rais hatasita ataiweka saini kwa sababu ya umuhimu wake na ninadhani ikawekwa saini tu, hilo nina uhakika, Mheshimiwa Waziri atatangaza katika *GN* ili sheria iweze kufanya kazi na sisi tunasema ikishafikia maamuzi hayo, ikishawekwa saini tuko njiani tutakamilisha kanuni na kanuni zitatoka *with no time.*

Lingine ambalo limezungumzwa ni adhabu, tumesema milioni moja ni ndogo. Tumetoa *amendment* milioni tano, lakini wengine wanasema kwamba milioni tano tumepandisha adhabu kwa shilingi, lakini miaka ya kufungwa ni ile ile miaka miwili hatukupandisha.

Kwa hiyo, zile ni adhabu mbili tofauti! Huwezi ukazioanisha! Tumesema Watanzania jamani ukiambiwa leo ulipe Sh.10,000/= na ukalale ndani siku moja, utalipa Sh.10,000/=, suala la adhabu ya kifungo kwa kweli Watanzania wanaliogopa sana. Kwa hiyo, hili tumelirekebisha na badala ya shilingi milioni moja tumeweka shilingi milioni tano kulingana na uzito wa suala lenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho nataka niseme suala la *procurement*, Waheshimiwa Wabunge wengi wameeleza kwamba fedha nyingi zinapotea katika manunuzi na wameeleza kwamba hatuna wataalam wa kutosha katika taasisi zetu. Sisi tunasema tumelipokea na tutalifanyia kazi ili kuhakikisha kwamba katika Taasisi za Serikali tuna watalaam wa *procurement* ili waweze kufanya manunuzi kulingana na

sheria za manunuzi, hili limezungumzwa na Mheshimiwa Janeth Massaburi katika taarifa yake ya maandishi na Mheshimiwa George Simbachawene.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, naunga mkono hoja iliyowasilishwa mbele yetu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri, sasa nitamwita mtoa hoja Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi.

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika**,** awali ya yote napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia Muswada huu kwa kuzungumza hapa Bungeni na wale waliochangia kimaandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwatambue Waheshimiwa Wabunge hawa kwa majina kama ifuatavyo:-

Waliochangia kwa kuzungumza ni Mheshimiwa Hamza Abdallah Mwenegoha - Mbunge wa Morogoro Kusini na Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi kwa niaba ya Mheshimiwa Dr. Dr. Abdallah Omar Kigoda - Mbunge wa Handeni. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Fatma A. Fereji - Mbunge wa Viti Maalum na Msemaji kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Kamati wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah - Mbunge wa Pangani, Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa - Mbunge wa Karatu, Mheshimiwa Estherina J. Kilasi - Mbunge wa Mbarali na Mheshimiwa George B. Simbachawene - Mbunge wa Kibakwe na Mheshimiwa Athuman Janguo - Mbunge wa Kisarawe. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa William Shellukindo - Mbunge wa Bumbuli, Mheshimiwa Savelina Silvanus Mwijage - Mbunge wa Viti maalum, Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi - Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Aloyce B. Kimaro Mbunge wa Vunjo, Mheshimiwa Zubeir A. Maulid - Mbunge wa Kwamtipura, Mheshimiwa John M. Cheyo Mbunge wa Bariadi mashariki na Mheshimiwa Mgana I. Msindai Mbunge wa Iramba Mashariki. *(Makofi)*

Waliochangia kwa maandishi walikuwa ni hawa wafuatao: Mheshimiwa Athuman Janguo - Mbunge wa Kisarawe, Mheshimiwa Mwanne Mchemba - Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Martha Mosses Mlata – Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Lucy Mayenga - Viti Maalum na Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa - Mbunge wa Lupa, *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. MERYCE M. EMANNUEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami ningependa kuchangia kidogo tu huu Muswada ulioko mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikiwapatia wakandarasi kazi lakini tatizo kubwa ni kutotoa pesa kwa wakati unaotakiwa. Hivyo kusababisha kazi hiyo kuchelewa kukamilika na kuchukua muda mrefu sana.

Hivyo, nashauri Serikai ijitahidi sana kutoa pesa kwa wakati au kama pesa haitoshi basi bora kusubiri pesa ipatikane ndo watoe kazi kwa mkandarasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna wawekezaji waliowekeza hapa kwetu nchini Tanzania ambapo imefikia mahali wamejisahau sana na wameshindwa kujua kuwa wako chini ya Serikai yetu ya Tanzania. Hii imepelekea hata kutoheshimu ngazi mbalimbali kama vile Kamati za Bunge, naomba Serikali itoe elimu kwa hao wawekezaji waheshimu basi mamlaka za nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba niseme kuwa, Serikali ijaribu angalau kutoa mikataba hiyo kwa Wabunge ili waweze kuipitia, wakati mwingine unaweza kupatikana ushauri au maoni kabla ya mkataba kuanza kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono Muswada. Ahsante.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu kwani utaiwezesha Serikali kusimamia vizuri matumizi ya pesa za umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa ushauri wangu katika maeneo yafuatayo:

Mheshimiwa Naibu Spika, Ukaguzi wa *CAG* ufuate popote zilipo pesa/hisa za umma. Isijali asilimia zilipo nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri angalau palipo na asilimia kuanzia 10 za umma, pakaguliwe na kuona matumizi mazuri ya mapato ya umma.
Wafanyakazi wamenyanyaswa sana mfano *WAZO Engineering* paangaliwe na Serikali na ukaguzi na Serikali na ukaguzi ufanyike.

Napenda kushauri nguzu za Kamati zipate kibali. Pale anapokaguliwa Afisa Mhasibu na kukutwa anayo mapungufu ni vizuri adhabu yake iwe ni wazi na isiyo na mizunguko mingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati zimefanya kazi kubwa na kutumia gharama kubwa ya muda na fedha, lakini zinaishia kupendekeza tu adhabu. Menye kudhibiti adhabu naye ana maoni yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii inadhoofisha nguvu za Kamati na kufanya maafisa Wahasibu waone hii ni routine tu, haina meno na haina athari yoyote moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, pesa za Serikali zisiliwe tu na yeyote. Iwapo tu Afisa Mhasibu amethibitika, kutosimamia vizuri fungu lake, awajibike mara moja kurudisha/kukatwa pesa hizo mara moja. Jicho pia liangalie kwa maafisa ugavi ni tatizo kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti ijikite kuwezesha Kamati zote zinazokagua pesa za umma kutembelea miradi yote inayopata pesa za Serikali. Miradi yetu mingi inapata pesa lakini pesa hizo hazitumiki vizuri. Mahali pengine hata hazitumiki palepale palipopangwa na maneo mengine mengi viwango vinakuwa vya chini sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, inapokuwa Kamati zinakagua Mahesabu bila kuona miradi, udanganyifu unakithiri.

Mwisho, naiomba Serikali iendelee kusimamia kwa nguvu zake zote suala zima linalohusu matumizi mazuri ya pesa za umma ikiwa ni pamoja na kutoa adhabu stahili kwa wasiotenda sawa.

**MHE. VUAI A. KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nakupongeza wewe kwa kusimamia Kikao hiki cha Mkutano wa Kumi na Mbili Mungu akubariki uendelee kuongoza na kusimamia vema

Mheshimiwa Naibu Spika, Pia nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri wa Wizara ya Fedha na Uchumi pamoja na watendaji wote kwa ushirikiano wao na kuwezesha kuwasilishwa Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria hii inahusu jamii ambayo ndiyo Serikali, bila fedha maendeleo hakuna, naiomba Serikali isimamie vyema malengo yake kwa faida ya Watanzania kama nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MWINCHOUM A. MSOMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napongeza kwa kuwasilisha Muswada wa sheria ya Ukaguzi wa Hesabu za Umma wa mwaka 2008 baada ya kuona kuna mapungufu yanayohitaji marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Nchi yetu inakabiliwa na tatizo kubwa kutokana na Maofisa wanunuzi wa kutosha na waliobobea katika kazi za Umma, hivyo hatuna budi kuliangalia hili kwa nia ya kumsaidia kufanya kazi zake vizuri za Ukaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa ushauri kwa Waziri wa Fedha kwamba liwekwe pendekezo la kuanzishwa kwa Naibu Mkaguzi na Mchunguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambaye ndiye atakayekuwa Msaidizi Mkuu wa Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kuipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu ambao ni muhimu sana katika kusimamia, kudhibiti na kulinda mali ya umma kwa kufanya ukaguzi na kushauri inavyopasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tunahudhuria mafunzo ya usimamizi wa bajeti, tuliona katika nchi nyingi *CAG* amekua akifanya kazi chini ya Bunge kuikagua Serikali kwa niaba ya wananchi na kuwasilisha taarifa katika Bunge na siyo kwa Serikali ambayo ndiyo imekaguliwa. Ni matumaini namaoni yangu kwamba iwapo taarifa hiyo ya CAG itapelekwa Bungeni, Serikali wakati wote itafanya kazi zake kwa tahadhari na uangalifu mkubwa na itachangia katika maendeleo kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, natarajia kwamba Serikali itakubaliana na kuridhia taarifa hizo kupelekwa Bungeni moja kwa moja badala ya utaratibu uliopendekezwa katika Muswada huu. Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana.

**MHE. DR. HARRISON GEORGE MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Spika, naomba nitamke toka awali kuwa naunga mkono hoja pamoja na kumtaka mtoa Hoja kuzingatia masuala kadhaa ninayoyaainisha katika mchango wangu huu.

Kwanza, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali (*CAG*) ana wajibu mkubwa na mzito katika mfumo mzima wa uwajibikaji na demokrasia ya uwakilishi. ndiyo maana hadhi yake kikatiba inalingana na kada nyingine ya watendaji waobeba majukumu mazito katika mfumo wetu wa utawala kama Majaji wa Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani. wote hawa ajira zao zinalindwa kwa taratibu za maalum za Kikatiba zinazohakikisha uhuru kamili katika utendajikazi wao.

Hivyo basi, napendekeza kuwa Ibara ya 1(1) ya Muswada wa Sheria ya Ukaguzi wa Hesabu za Umma itoe mamlakaya kumteua *CAG* kwa Rais lakini kutokana na majina matatu yaliyopendekezwa na Kamati ya Bunge (*PAC*). Utaratibu huu ambao unafuatwa sehemu mbalimbali duniani unainua hadhi ya nafasi ya *CAG* kuwa ya muafaka wa mihimili miwili ya dola; *executive* na *legislature*. njia nyingine ni jina alilopendekeza Rais huletwa Bungeni *for approval.*

Pili, ibara ya 1 (2) na (3) inahitaji marekebisho ya lugha tu: 1 (2) isomeke: *The appointment of the controller and Auditor General Shall take into account relevant professional qualifications, experience and leadership skills commensurate with the job.* Katika Ibara ya (1) (3), neno *of* baada ya neno *appointment* liondolewe.

Tatu, ikiwa *CAG* anaapishwa na Rais kwa mujibu wa Ibara ya 1 (3). Kiapo kilichopo kwenye *schedule* mbele ya *State Attorney* ni cha nini tena?

Nne, na mwisho, *CAG* hana madaraka kisheria kuwapeleka mahakamani (kuwashitaki) wale wote wanaokiuka taratibu za matumizi ya fedha za umma. ni vema Serikali ikaangalia uwezekano huo wa kumpa meno zaidi *CAG*. Ahsante.

**MHE. ATHUMANI JANGUO:** Mheshimiwa Spika, kutoka meza ya Mbunge wa Kisarawe, S. L. P. 28001 Kisarawe, 11 Juni, 2008. Katibu wa Bunge S. L. P. 941 Dodoma. Kwa mujibu wa Kanuni 86 (ii) napenda kushauri marekebisho katika jedwali la Marekebisho na Muswada wenyewe kwenye maeneo yafuatayo:

A. MUSWADA

Kifungo 9 (b) na (c) ukurasa wa 10;
Kifungu cha 11(2)(f);
Kifungu 14 (3);
Kifungu 37 (2) na 38;
Kifungu 48 (4).

B. Jedwali la Marekebisho

Kifungu 9 (d) sahihisho sawa na kwenye A
Kifungu 17 (6);
Kifungu 30 (3) (a);
Kifungu 32 L na N;
Kifungu 49 Q;
Kifungu 44 R [44](2)(3)(4);
Kifungu 44 (3) na (4);
Kifungu T (Kifungu 47 (4).

**MHE. JANETH M. MASSABURI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu muhimu kwa maslahi ya Taifa. Mchango wangu ni kama ifuatavyo:-

Moja, *CAG* akague Mpango wa Manunuzi (*Procurement Plan*) na matumizi yake.

Pili, Kutokana na utaalamu mdogo wa Kitengo cha manunuzi na ukosefu wa wataalam wa fani ya ugavi na ununuzi, ni vema Serikali ikatenga fungu maalum kwa ajili ya mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu katika fani hii ya *Contract and Procurement Management.*

Tatu, kwa kuwa asilimia 80 ya fedha za Serikali hutumika katika ununuzi wa umma, ni vema Serikali ; ikalitazama eneo hili kwa unyeti zaidi ili kupunguza malalamiko yanayotokana na kutofanya kazi inayolingana na gharama halisi (*value for money*)

Nne, mpango wa manunuzi uzingatiwe katika Idara zote za Serikali lili kubaini mahitaji halisi ya kila Kitengo na kupunguza matumizi yasiyo kuwa ya lazima. *Procurement Plan* ni sialaha ya kuisaidia Serikali kubana matumizi.

Tano, Makatibu Wakuu, Wakuu wa Taasisi za Umma, Mawaziri, Wabunge, wangepatiwa japo semina ya *Procurement and Contract Management* ili kupata uelewa katika fani hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono asilimia kwa mia. Nichukue nafasi hii kuwapongeza kwa kuleta Muswada huu mapema na kwa wakati. Mheshimiwa Mustafa Mkulo, Mbunge, Waziri, Naibu Waziri Mheshimiwa Yussuf Mzee, Mbunge, Naibu Waziri Sumari, Mbunge, Mkaguzi Mkuu na Wataalam wote wa Ofisi hizo.

Ushauri – Wakaguzi wa Ndani wa Halmashauri wapewe nyenzo za kufanyia kazi ili wasiwe tegemezi kwenye Halmashauri au kutegemea ufadhili wa *DED*, wapewe gari na nyumba na kadhalika, wakifanyiwa huduma hizo watafanya kazi bila kishawishi. Pamoja na hayo watafanya ukaguzi kwenye maeneo ya miradi kama ijulikanavyo jiografia ya Halmashauri zetu na miradi iliko ni mbali. Pia kuwaondolea woga wa kufanya kazi.

Wakaguzi kwenye Halmashauri zetu wasikae muda mrefu ili wasijenge mazoea na kushawishika kupokea rushwa.

Mkaguzi Mkuu aangaliye jinsi ya kutoa adhabu kali kwa wale wanaopata hati chafu (kukosa hati safi) ili kuwafanya wathamini fedha za umma.

Mkaguzi Mkuu akague miradi yote mikubwa inayotolewa na wafadhili badala ya kuwatuma wakaguzi wa Halmashauri pekee, kwani fedha na miradi hiyo ni ya kimataifa.

Elimu – Waheshimiwa Madiwani waendelee kupewa semina ili kuwawezesha kufuatilia hesabu kwenye maeneo husika ili angalau wasaidiane na Wakaguzi kutokana na Halmashauri zetu kutokuwa na uzoefu na elimu ya hesabu na ujenzi.

Kila Halmashauri isisitizwe kuunda Bodi ya Ukaguzi kwenye kila Wilaya, ili isiwe ni hiyari kama ilivyo sasa wengine wameunda na wengine bado iwe (amri) na sheria ya ukaguzi.

Mkaguzi Mkuu anapokagua miradi na kugundulika ujenzi umejengwa chini ya kiwango ni vema mkandarasi ashitakiwe na kulipa gharama zote kwa riba ili iwe fundisho kwa makandarasi wote, kwani ujenzi wa sasa umekwenda mpaka vijijini ambako wao hawana uwezo na kutoa amri au elimu. Kwa sasa majengo mengi ya madarasa/nyumba za walimu zina ufa na mbovu. Naunga mkono.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Maoni – mikataba mingi ya wawekezaji ina ibana Serikali kupata takwimu sawa sawa za mapato halisi, kwani uwezekano wa kuficha mapato yao kwa kukwepa kulipa kodi ni mkubwa. Hivyo iangaliwe upya.

Kuwekwe utaratibu maalum wa kuweza kuyakagua makampuni yaliyowekeza katika nyaraka za Taifa, ili kupunguza utata wa mapato yasiyo halali ya uchumi wa Taifa letu.

Maswali – je ni kwa nini miradi mikubwa inayosimamiwa na Serikali inachukua muda mrefu? Je, Serikali haioni kwamba kwa kufanya hivyo kunayumbisha pato na pato la Taifa? Mfano mradi wa bwawa la Mugumu Serengeti. Pia kunakuwa na ongezeko kubwa la matumizi ya pesa kinyume na bajeti iliyowekwa wakati wa mkataba. Je, hayo ni mahesabu ya wapi?

Je, ni sheria gani inayomruhusu mwekezaji kuzuia, viongozi wa Serikali kukagua shughuli zake anazoendesha katika eneo lake ambalo liko chini ya mkataba wa wawekezaji uchumi?

Mfano, mwenye hoteli ya Guruneti, ile sehemu imeshakuwa ni mali ya Marekani? Je, tunahitaji kupata *visa.* Je, Serikali inasema nini kwa wawekezaji wa namna hii? Naunga mkono hoja 100%.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naipongeza Serikali kuleta muswada huu wa *"The Public Audit act 2008"*.

Mheshimiwa Naibu Spika, taakuma hii ni muhimu sana kwa maendeleo ya uchumi wa nchi zetu hizi zinazoendelea, hivyo kifedha na ukaguzi wake kwa kumtumia vizuri Mkaguzi wake wa Serikali, utatupatia uwezo wa kuchambua hali ya matumizi ya fedha za umma. Ni kwa msingi huo ninashauri;

1. Tuanze na kuimarisha ofisi hii ili tuwapate wakaguzi wazuri wenye moyo safi na wenye maslahi mazuri ili wasirubuniwe na taasisi nyingine zinazotoa maslahi mazuri zaidi. Tuwalinde na tuwaenzi ili watufanyie kazi nzuri.
2. Tuandae mikakati ya kuimarisha ofisi za kanda, mikoa na wilaya ili kuwe na mtiririko wa usimamizi wa ukaguzi kuanzia ngazi za chini kabisa.

3. Madaraka ya Mkaguzi Mkuu katika uwajibikaji wake kwenye Bunge, kuendana sambamba na wakaguzi wa mikoani ili wawajibike na kwenye vikao badala ya kuwajibika kwa Mkuu wa Mkoa au *RAS*, na katika Wilaya kuwajibika kwenye vikao vikuu vya Wilaya. Hili linasaidia *transparency* katika kufikia maamuzi kwa utawala bora.

4. Nashauri tuwe waangalifu zaidi juu ya pendekezo la kumtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu kupewa *contract* ya miaka 5/5/5. Hali hii inaweza kumfanya akijua ana miaka michache kumaliza kipindi chake, akaanza kulegeza kamba ili kujiandaa kustaafu baada ya miaka 5. Kwanini asiachwe akaingia kwenye mkataba wa kudumu bila kupewa muda maalum.

Vinginevyo ingefaa kumhakikishia kuwepo kwake bila vitisho au wasiwasi wa kuondoka au kuondolewa.

Naunga mkono Muswada huu.

**MHE. PHILEMON NDESAMBURO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu umekuja wakati muafaka wakati nchi hii inapita katika kipindi kugumu, hasa kuhusu hujuma zinazofanywa na wawekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, imenitisha kusikia mwekezaji wa Gurumeti *VIP* akizuia Kamati halali ya Bunge inayowakilisha Bunge nzima kwa niaba ya Watanzania wote kukagua mali zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii siyo dharau tu, bali ni matusi kwa Watanzania wote japokuwa wawekezaji wanapewa ardhi kwa muda maalum, lakini ardhi yote ni mali ya Rais kwa niaba ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima Serikali ichukue hatua kali kwa kampuni hii ili iwe onyo kwa wengine wenye dharau kama wao. Kama siyo kuwafukuza, itafutwe njia nyingine kali ya kuwafanya waelewe nchi hii ina Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kukagua siyo kukagua pesa tu, ziko mali nyingi ambazo zinahitaji ukaguzi. Fedha za Serikali zimewekezwa katika sehemu nyingi kuseme eti ukaguzi ufanyike pale Serikali ina *50 percent shares*, siyo sawa.

Mheshimwia Naibu Spika, hali hii itawafanya maeneo yale Serikali imewekeza chini ya asilimia 50 watatuhujumu kwani wanajua hawakaguliwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ushauri wangu, pale Serikali ina maslahi, hata kama ina asilimia mbili tu *CAG* awe na nguvu ya kisheria ya kuweza kufanya ukaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukitaka kuwa na chombo huru, *CAG* aripoti Bungeni bila kuwa na ulazima wa kuripoti kwa Waziri wa Fedha na Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama itakuwa lazima kuripoti kwa Waziri wa Fedha, Bunge halitapata ripoti ambayo haijachezewa kwa makusudi ya kulinda maslahi fulani fulani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naunga mkono Muswada na naomba ipitishwe na ifanye kazi mara moja ili kulinda maslahi ya nchi hii. Kwa haya machache naounga mkono hoja.

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Mheshimiwa ningeshauri sehemu ya (iv) kifungu cha 28, kizingatiwe kwani utakuta sehemu inayokaguliwa hupewa hati safi wakati kuna matatizo kadhaa ambayo yangeweza kuathiri upatikanaji wa hati safi.

Mfano wa kwanza; Halmashauri ya Kilwa kuna mkusanyaji ushuru (Kampuni ya Nongwa) ili chana stakabadhi za Serikali na kuiba fedha za makusanyo, kesi ikafika Mahakamani na hatimaye kufutwa kesi. Lakini hati safi zimeendelea kutolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano wa pili ni wa Benki Kuu. EPA. Haya yote yanaonyesha kutokuwa makini katika kutekeleza kile ambacho ukaguzi unatakiwa kiwe. Hivyo basi *accounting officers* wafanye kazi zao kwa makini na uwazi.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naunga mkono hoja katika kudhibiti matumizi bora ya fedha za umma, kuimarisha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu ni jambo zuri sana. Naipongeza sana Serikali kwa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwangu mimi, panya buku anayekula fedha za umma bila yeye kuonekana ni "*Public Procurement*". Sasa basi wakati kuna mianya mingi ya kuangaliwa kwenye Sheria ya Manunuzi ya 2004, naomba sana Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu aweke nguvu za ziada kwenye *"Performance Audits"* kwenye Wizara, Idara na Taasisi zote za Umma.

Wakati huo huo naiomba Serikali ifikirie kuanzisha *Procurement Agency*. Taasisi hii ndiyo inaweza kununua kwa ajili ya Serikali, vifaa vya gharama kubwa.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naunga mkono Muswada huu kwa asilimia 100.

Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kuleta Muswada huu muhimu kwa manufaa ya Serikali yetu na Watanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu ni muhimu kwa kuwa utasaidia kwa kiwango kikubwa umeweza kuweka bayana nafasi ambayo atakuwa nayo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika kudhibiti na kusimamia vyema masuala ya usimamizi, mgawanyo na udhibiti wa fedha za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni yangu ni kwamba kwa muda mrefu kumekuwepo na tatizo katika baadhi ya taasisi za Serikali kuhusu suala zima la matumizi mabaya ya fedha za umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waziri wa Fedha kwa kutumia Muswada huu asaidie kwa kiwango kikubwa kudhibiti tatizo la matumizi mabaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwepo na *Value for money*. Ofisi ya CAG licha ya kuwa na uwezo kukagua na kudhibiti iwe makini kujua pia kuhusu matumizi halisi ya fedha zilizotolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kuendekeza Wakandarasi wasio na uwezo kwa kigezo cha uzalendo liachwe limekuwa likileta matatizo kwa wananchi kwa kushindwa kutekeleza kazi wanazopewa.

Naunga mkono hoja asilimia 100.

**NAIBU SPIKA:** Tulikuwa tumebakia na mchangiaji wetu mmoja Mheshimiwa Waziri wa Elimu. Wengine wana majina marefu! Mheshimiwa *Prof*. Jumanne Maghembe, yeye alishakuwa Waziri wa Maliasili zamani kabla ya mabadiliko, kwa hiyo, maneno mengine mliyozungumza atakuwa na maelezo.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nikushukuru sana kwa kunipa nafasi kuchangia katika Muswada huu ulio mbele yetu. Kwanza, ninaipongeza Wizara ya Fedha kwa kutayarisha Muswada huu ambao kwa kweli ni wa kihistoria hapa nchini kwetu, ni Muswada mzuri na umekuja kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nia yangu ni kutoa maelezo mafupi juu ya maelezo na hotuba zilizotolewa kuhusu Hoteli ya Sasakwa iliyoko Gurumeti. Hoteli hii ya Sasakwa iko Gurumeti na inahudumia wageni wanaokuja Gurumeti na Serengeti ya Magharibi na Ikorongo Mkoani Mara. Imejengwa kwa uwekezaji wa dola milioni 90 na ni hoteli ya nyota saba.

Hoteli za kawaida zinakuwa ni nyota moja mpaka nyota tano, zingine chini ya hapo zinakuwa ni *guest houses;* lakini hii ni hoteli maalum iliyojengwa kwa kiwango cha nyota saba na katika mwaka 2006 katika hoteli 20 nzuri duniani, hoteli hii ilikuwa ni moja ya hoteli hizo. Pia katika mwaka huo ilikuwa ni hoteli bora kupita zote katika Bara la Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoteli hii ina vyumba 15 tu na imejengwa kwa ajili ya wakuu wa nchi *(needs of state and government)* wanaokuja kwenye nchi yetu kwa ajili ya utalii au kwa viongozi ambao wanahitaji hoteli ya ubora nyota saba. Kuwa na nafasi katika hoteli ile, lazima uchukue vyumba vyote na gharama yake kwa siku ni dola 35,000 za Marekani kwa kukodi hoteli yote kwa siku. Hoteli ile ina *booking* kuanzia tarehe 1 Januari mpaka tarehe 31 Desemba. Ukitaka nafasi pale inabidi u-*book* kwa mwaka mzima mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, madhumuni ya hoteli ile ni kuwapokea na kuwapa mahali pa kukaa wakuu wa nchi wanaokuja kwa madhumuni ya kupumzika au kwa utalii hapa Tanzania, Wakuu wa Mashirika makubwa ya Kimataifa ambao pia wanahitaji ulinzi na wanataka kufanya utalii hapa nchini kwetu na Bodi za mashirika makubwa ya Kimataifa ambayo yanahitaji kufanya mikutano yao katika maeneo ambayo yana utulivu na ubora ambao hauna ulinganisho katika dunia hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikitoa mfano, Mheshimiwa Thabo Mbeki Rais wa Afrika Kusini alikaa pale mwezi Desemba, 2006 na baada ya hapo alikuja tena mara nyingine, Naibu Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje wa Marekani naye ni mmoja wa wageni ambaye najua alikuja pale. Lakini pia, kumekuwa na mikutano ya Bodi za Wakurugenzi nyingi kama Bodi ya *Time Warner* ya *CNN* na Bodi ya shirika kubwa la *TATA* wamefanya mikutano hapo.

Mwenye shirika kama TATA ni mtu ambaye ni wa pili duniani kwa utajiri na *celebrity* wengine na wakuu wa nchi mbalimbali wamekuja nchini kwetu wakakaa sasa kwa namna yoyote wasingependa kutangazwa kwamba wako nchini kwa sababu wamekuja kupumzika.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha muhimu ni kwamba wanatoa taarifa kwenye Serikali na Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje inajua na inaweka Maofisa wa Serikali katika eneo lile pamoja na ulinzi unaolingana na ugeni ambao uko pale. Sasa kwa kuwa kunakuwa na wakuu wa nchi, wakati mwingine kunakuwa na wakuu wa nchi na *delegation* zao ambao wako pale, ulinzi unakuwa mkali kwa kweli. Kwa hiyo, wale ambao wanapenda kwenda kutembelea pale ni lazima watoe taarifa na hasa kama wanataka kwenda kule na kuna wakuu wa nchi wakielezwa na Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje, basi wapewe ruhusa maalum na Wizara inayohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa wageni wanaokuja pale ni *entourage* au ni Bodi nzima wanatumia kila kitu, yaani wananunua huduma ya kila kitu kilichoko pale. Kwa hiyo, kwa kawaida hawategemei wageni wale ambao wanakuja tu *casually*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu kushauri kwamba sisi watu wakubwa tunapokwenda kwenye maeneo kama haya, ni vizuri tutoe taarifa na tujue kama kuna nafasi au hakuna, ili tuweze kwenda na kama ni *convenient* na kama ni lazima twende, basi tutafute utaratibu wa kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kutoa taarifa kidogo kuhusu mapato na matumizi ya hoteli ile. Tangu ile hoteli imeanza, hakuna fedha ambayo imepatikana pale ambayo imetolewa nje ya Tanzania. Fedha zote ambazo zimepatikana zinalipia miradi ya maendeleo katika Wilaya ya Serengeti na katika Wilaya ya Bunda kujenga visima vya maji, kujenga Shule za Msingi, Shule za Sekondari na kulinda maliasili ya wanyamapori, tangu imeanza jumla ya dola milioni 36 zimetumika katika miradi mbalimbali ya maendeleo katika eneo lile. Aidha, kampuni ile imetoa *scholarship* 20, mbili kwa kila mwaka kwa Watanzania kusoma katika Vyuo Vikuu vya Marekani, kusomea Elimu ya *Conservation* katika Vyuo Vikuu vya Marekani kwa kiwango cha Uzamili au *Master of Science.*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitoe tu maelezo kwamba sio vizuri kwa kweli, kwa namna utamaduni wetu ulivyo, kuambiwa huwezi kuingia hapa! Lakini kwa jinsi ambavyo tuna-*interact* na mataifa mengine hasa katika utalii na kukubali kwamba wageni na wakuu wa nchi waje kwenye utalii ni vizuri tuelewe kwamba katika kufanya hivyo wakati mwingine tunaweza kupata *inconvenience.*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini *some of these inconvenience* zinatokana na mkakati wa kuongeza mapato katika sekta hii ya utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, yangu yalikuwa ni hayo mafupi. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii nichangie Muswada huu ambao umeletwa kwa dharura.

Mheshimiwa Sitaki kuwarudisha Waheshimiwa Wabunge tulikotoka, lakini kwa jambo ambalo linaonekana linatuletea matatizo makubwa kikatiba iwapo Muswada utapita. Muswada huu kama ulivyoletwa umetokana na Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo inazungumzia kazi ya *CAG* kwa undani kabisa.

Sasa ukiangalia Muswada ulivyoletwa inaonekana haugusi Zanzibar, maana ripoti ya leo ya *CAG* tuliyonayo haizungumzii Zanzibar na Zanzibar imekuwa ni chanzo cha matatizo makubwa katika muungano wetu miaka nenda rudi hivyo hivyo! Nataka kujua, hii sheria ita-*extend* kwenda Zanzibar au hapana? Kama hai-*extend* Zanzibar na fedha zinazokwenda Zanzibar zinatoka kwenye *consolidated fund* chini ya Ibara ya 136 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tunakwenda wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ndio maana ukiangalia *exemption* za Zanzibar ni nyingi mno kuliko za Bara. *Collection* ya kodi Zanzibar ni ndogo sana, inabidi muungano ndio uchangie kule na *CAG* hana makucha kule, yuko hapa anatanda hapa *mainland* tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kujua kama kweli sheria hii ita-*extend* Zanzibar. Kama ita-*extend*, basi tuseme hivyo wazi wazi kwamba "*these act shall extend to Zanzibar.*" Vinginevyo, kwa kuwa iko *silent* ni ya kwetu tu, tunapeleka wapi Jamhuri hii? Wanaotozwa kodi wako hapa na fedha zinakwenda kutumika Zanzibar na Zanzibar *CAG* hana meno, tunafanya nini? Sina mengi isipokuwa nilitaka kujua kama kuna maelekezo kuhusu suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana, mmechangia, siyo kwamba umetaka uamuzi wa Spika, mmechangia watawajibu. Sasa tulishamaliza wachangiaji wote na tuanze kupata majibu kutoka kwa Naibu Waziri wa Fedha.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (OMAR Y. MZEE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza na mimi nataka nikushukuru kwa kupata fursa hii ili nami nichangie Muswada ulio mbele yetu. Lakini kabla sijachangia na mimi naunga mkono hoja mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nichangie Muswada uliowasilishwa mbele yetu kwanza kwa kujenga misingi ili sote tuweze kufahamu na kuelewa kwa nini tumewasilisha Muswada huu. Nasema hivyo kwa sababu Wajumbe wengi wamegusa Katiba na baadhi wamesema ipo haja ya kuifanyia marekebisho na baadhi wamesema kwa sasa twende taratibu.

Kwanza Katiba yetu Ibara ya 143 imetupa nguvu na uwezo wa kutunga Sheria ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Nasema tumechelewa! Lakini kama hilo halitoshi, mwaka 2006 wenzetu wa *AFROSAI* walikuja Tanzania kututathmini huu uzuri ambao tunaouzungumza wa Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Kufanya Mahesabu na kuyawasilisha na kuyatoa kwa wakati ukoje. Walipowasili, cha kwanza kabisa waliuliza:

“Huyu Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu ya Serikali yupo kwa mujibu wa sheria? Tulipomwambia hana sheria, *classification* ambayo tumepewa ni wa mwisho. Juu ya uzuri wote ambao tulikuwa nao, tukasema kama hivyo ndivyo, mwaka 2009 wenzetu wanakuja tena kututathmini, tukasema kwanza tutunge sheria ili Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu awe na sheria yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitajaribu kujibu baadhi ya hoja, hata Zanzibar wana sheria yao ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu. Sisi Jamhuri ya Muungano hatuna. Tulikuwa tunatumia *the Public Finance Act* kwa mambo yote ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu. Kulikuwa kuna mapungufu.

Kwa hiyo, tulisema tuilete sheria hii lakini tulijua kwamba, sheria hii tunaileta lakini kwa kuwa hesabu haianzi kwenye kumi, ila inaanza kwenye moja. Kwa maana hiyo, tulisema twende taratibu. Hatukutaka tuje na marekebisho ya katiba kwa sababu hesabu inaanza moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katiba inatutaka tuwe na sheria, sheria hakuna, ndio tukasema wacha kwanza tuje na sheria. Kwa hiyo, tumeelewa, tumefahamu kwamba Waheshimiwa Wabunge baadhi wameeleza juu ya wasiwasi wao uwasilishaji wa ripoti ya *CAG*. Nataka niwaambie kwamba marekebisho yoyote utakayoyafanya maana yake utaigusa Katiba kwa wakati huu.

Tulisema, kwa sababu hakuna dosari *CAG* kumaliza ripoti yake na kuiwasilisha kwa Rais na Rais atampa mtu atakayemwona anafaa wa kuiwasilisha Bungeni, tulisema tufuate hiyo kwa sababu hakutakuwa na dosari yoyote kwa sababu Bunge litaipata ripoti ile kwa wakati muafaka kama Katiba ilivyoweka.

Kwa hiyo, hoja hii ilizungumzwa na ilijadiliwa sana na Waheshimiwa ambao naomba niwataje wachache tu. Mheshimiwa Fatma Fereji, Mheshimiwa *Dr*. Wilbrod Slaa, Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa George Simbachawene na sasa hivi Mheshimiwa Nimrod Mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema kwamba sheria hii itakapokuwepo itatupa nafasi kuanza kuondoka kuwa wa mwisho angalau kufikia ile hatua ambayo na sisi

tunaitegemea. Lakini tulizungumza kwa umoja wetu, kwa nguvu zetu tunataka kumpa meno Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu. Sasa hivi nataka niseme amekuwa kama mzee ana meno mawili ya kutafuna, Muswada huu ndio utakaompa meno.

Kwanza, nataka nitoe maelezo mafupi tu au nionyeshe vifungu au vichache, hivi sasa ripoti za *CAG* zinaonekana kama ripoti za kawaida tu lakini sheria hii mlipaji mkuu *paymaster general* atalazimika kujibu hoja za *CAG* kama yeye atalazimika kujibu hoja za *CAG* kuna *Accounting Officers* katika maeneo mengine atawabana. Kwa hiyo, tunasema kwamba tutapunguza upotevu wa fedha zetu sivyo kama tunavyokwenda sasa hivi, lakini kama hilo halitoshi sheria ya fedha hivi sasa mnavyoiona *section 26* mpaka *section 42* ndio inayomweleza Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Shughuli za Serikali, haijatoa *provision* ya kuandaa kanuni kwa ajili ya Mdhibiti.

Sheria hii itatoa *provision* hiyo na zitaandaliwa kanuni. Tumezungumza mengi humu ndani kuhusu kuimarisha hiki na hiki, mengi yatajitokeza katika ile kanuni ambayo itakayotungwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama hilo nalo halitoshi, Sheria ya *Public Finance* inasema: "Waziri wa Fedha ndiye atakayeteua Mkaguzi wa kumkagua *CAG."* Hapa pana mawazo yanapingana, *CAG* anamkagua Waziri wa Fedha, Waziri wa Fedha ateue amkague *CAG*, pana mgongano wa mawazo. Tukasema haiwezekani tuweke katika sheria hii. Bunge liingie kwa kupitia Kamati zake wateue mkaguzi kwa ajili ya Ofisi ya *CAG*. Kwa hiyo, utaona kwamba hapa tunataka nini. Tunachokitaka katika Muswada huu ni kuhakikisha kwamba suala zima la upotevu wa fedha za umma kama hatulimalizi tunalipunguza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo tulilizungumza katika asubuhi hii wakati tunachangia na limechangiwa sana na Mheshimiwa John Cheyo na Mheshimiwa Athumani Janguo na Waheshimiwa wengineo, suala la kwamba *Auditor and Controller General* hivi sasa anakuwa kama ni *post-mortem*, watu wanafanya uharibifu yeye anakwenda mwisho kukagua, anatuambia hapa pameharibika. Tukasema katika sheria hii, tutumie *Internal Auditor Reports*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa *Internal Auditors* kwa sababu wana-*produce quarterly reports* watakuwa wanaziwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu. *Suppose* unakagua *project*, *project* haiwezi kumalizika kwa miezi mitatu. Kwa hiyo, unaweza ukajua hapa patakuwa na upotevu na *Controller and Auditor General* anaweza akachukua hatua haraka sana. Kwa hiyo, katika sheria hii, tunacho hicho kipengele na kitaweza kutusaidia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo lilizungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wengi, Mheshimiwa Zubeir, Mheshimiwa Estherina Kilasi na wengine, walitaka *Controller and Auditor General* a-*audit* mashirika hata kama tuna hisa chini ya *50 percent*. Nasema hivi, kwanza ulimwengu mzima haufanyi hivyo. Anayeteua *auditor* wa ku-*audit* lile shirika ni yule ambaye ana *share* nyingi, hata sisi Serikali tukitaka, bodi ndio inayoteua, wewe huna *share* nyingi kwenye bodi huwezi ukashinda.

Kwa hiyo, tumesema sisi kwa sababu msajili wa hazina ana uwezo na kiutaratibu, ndivyo ilivyo wa kupata sheria za *auditor* kwa yale mashirika yote ambayo Serikali ina hisa, tukasema katika sheria hii tuangalie kama kuna uwezekano wa kuongeza kifungu ambacho hii ripoti iliyokuwa *audited* kwenye lile shirika atapatiwa *Auditor and Controller General* ataipitia na kutoa ushauri kwa Serikali juu ya shirika linalohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine limezungumzwa na Waheshimiwa wengi juu ya kutangazwa kwa sheria hii na kuanza kufanya kazi na kanuni, nataka niseme tumewasilisha Muswada huu wa sheria hii kipindi hiki, Muswada huu wa Sheria kwa sababu ya umuhimu wake na ninadhani tukimaliza kuipitisha Mheshimiwa Rais hatasita ataiweka saini kwa sababu ya umuhimu wake na ninadhani ikawekwa saini tu, hilo nina uhakika, Mheshimiwa Waziri atatangaza katika *GN* ili sheria iweze kufanya kazi na sisi tunasema ikishafikia maamuzi hayo, ikishawekwa saini tuko njiani tutakamilisha kanuni na kanuni zitatoka *with no time.*

Lingine ambalo limezungumzwa ni adhabu, tumesema milioni moja ni ndogo. Tumetoa *amendment* milioni tano, lakini wengine wanasema kwamba milioni tano tumepandisha adhabu kwa shilingi, lakini miaka ya kufungwa ni ile ile miaka miwili hatukupandisha.

Kwa hiyo, zile ni adhabu mbili tofauti! Huwezi ukazioanisha! Tumesema Watanzania jamani ukiambiwa leo ulipe Sh.10,000/= na ukalale ndani siku moja, utalipa Sh.10,000/=, suala la adhabu ya kifungo kwa kweli Watanzania wanaliogopa sana. Kwa hiyo, hili tumelirekebisha na badala ya shilingi milioni moja tumeweka shilingi milioni tano kulingana na uzito wa suala lenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho nataka niseme suala la *procurement*, Waheshimiwa Wabunge wengi wameeleza kwamba fedha nyingi zinapotea katika manunuzi na wameeleza kwamba hatuna wataalam wa kutosha katika taasisi zetu. Sisi tunasema tumelipokea na tutalifanyia kazi ili kuhakikisha kwamba katika Taasisi za Serikali tuna watalaam wa *procurement* ili waweze kufanya manunuzi kulingana na sheria za manunuzi, hili limezungumzwa na Mheshimiwa Janeth Massaburi katika taarifa yake ya maandishi na Mheshimiwa George Simbachawene.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, naunga mkono hoja iliyowasilishwa mbele yetu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri, sasa nitamwita mtoa hoja Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi.

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika**,** awali ya yote napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia Muswada huu kwa kuzungumza hapa Bungeni na wale waliochangia kimaandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwatambue Waheshimiwa Wabunge hawa kwa majina kama ifuatavyo:-

Waliochangia kwa kuzungumza ni Mheshimiwa Hamza Abdallah Mwenegoha - Mbunge wa Morogoro Kusini na Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi kwa niaba ya Mheshimiwa Dr. Dr. Abdallah Omar Kigoda - Mbunge wa Handeni. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Fatma A. Fereji - Mbunge wa Viti Maalum na Msemaji kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Kamati wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah - Mbunge wa Pangani, Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa - Mbunge wa Karatu, Mheshimiwa Estherina J. Kilasi - Mbunge wa Mbarali na Mheshimiwa George B. Simbachawene - Mbunge wa Kibakwe na Mheshimiwa Athuman Janguo - Mbunge wa Kisarawe. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa William Shellukindo - Mbunge wa Bumbuli, Mheshimiwa Savelina Silvanus Mwijage - Mbunge wa Viti maalum, Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi - Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Aloyce B. Kimaro Mbunge wa Vunjo, Mheshimiwa Zubeir A. Maulid - Mbunge wa Kwamtipura, Mheshimiwa John M. Cheyo Mbunge wa Bariadi mashariki na Mheshimiwa Mgana I. Msindai Mbunge wa Iramba Mashariki. *(Makofi)*

Waliochangia kwa maandishi walikuwa ni hawa wafuatao: Mheshimiwa Athuman Janguo - Mbunge wa Kisarawe, Mheshimiwa Mwanne Mchemba - Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Martha Mosses Mlata – Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Lucy Mayenga - Viti Maalum na Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa - Mbunge wa Lupa, *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Mwinchoum Abdulrahman Msomi - Mbunge wa Kigamboni, Mheshimiwa Ruth B. Msafiri – Mbunge wa Muleba Kaskazini, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo - Mbunge wa Moshi Mjini, Mheshimiwa Janeth Mourice Massaburi - Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Paul P. Kimiti - Mbunge wa Sumbawanga Mjini na Mheshimiwa Mwanawetu S. Zaraf - Mbunge wa Viti Maalum. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Said Amour Arfi - Mbunge wa Mpanda Kati, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis - Mbunge wa Magogoni, Mheshimiwa Dr. George H. Mwakyembe - Mbunge wa Kyela, Mheshimiwa Meryce Mussa Emmanuel - Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Andrew Chenge - Mbunge wa Bariadi Magharibi na Mheshimiwa Prof. Jumanne Abdallah Maghembe - Waziri wa Elimu na Ufundi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nimrod Mkono umemtaja?

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, na Mheshimiwa Nimrod Mkono - Mbunge wa Musoma Vijijini. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Pia Naibu Waziri wako amechangia.

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, wa mwisho alikuwa ni Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee - Naibu Waziri wa Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa shukrani za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi kwa kuunga mkono Muswada huu.

Aidha, napenda pia kutoa shukrani zangu kwa Kambi ya Upinzani kwa kuunga mkono Muswada huu. Ninaahidi kwamba Serikali itaifanyia kazi michango na mawazo yaliyotolewa na Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi pamoja na yale yaliyotolewa na Kambi ya Upinzani.

Naomba kujibu hoja chache kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge ambazo hazikuweza kujibiwa kwa ukamilifu na Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mengi yaliyozungumzwa na hasa pale ambapo Wabunge wengi walizungumzia vifungu fulani fulani, kwa kweli mengi yalikuwa ni ushauri kwamba mahali fulani pamekosewa, tunaahidi kwamba yale yote ambayo yamekosewa yatarekebishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri amejibu karibu hoja zote, lakini ningependa kusisitiza mambo matatu. La kwanza, ni lile ambalo Mheshimiwa Nimrod Mkono amelizungumzia. Aliyoyazungumza yana mantiki, lakini ukweli ni kwamba Zanzibar wana Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali wa kwao wenyewe ambaye anawajibika kwa Rais na pia anawajibika kwa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

Lakini nataka nikubali pia kwamba iko dosari ambayo itabidi tuitazame kwa sababu sio tu mgao wa fedha za bajeti ambazo tunazipeleka Zanzibar, zipo pia pesa nyingi kuliko zile za mgao ambazo Serikali ya Muungano inazipeleka Zanzibar na hasa pesa ambazo zinapitia Serikali ya Muungano ambazo zinahusiana na madeni, misaada na mikopo.

Kwa hiyo, nadhani hili inawezekana hatukuliangalia vizuri wakati tunakamilisha Muswada huu. Naahidi kwamba Serikali tutalifanyia kazi na tutaangalia jinsi gani ambavyo linaweza likashughulikiwa. Tutawasiliana na wenzetu wa Zanzibar kuona jinsi ambavyo tunaweza tukalighulikia hilo na Mheshimiwa Nimrod Mkono tunamshukuru kwa kulileta hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ningependa nilisisitize ni muda gani Sheria hii itaanza? Serikali imeleta Muswada huu *under certificate of agency* kwa sababu ya umuhimu wake.

Mtazamo wa Serikali ni kwamba Sheria hii ianze kutumika kuaanzia tarehe 01 Julai, 2008 na kwa sababu hiyo, mara tu Waheshimiwa Wabunge mtakapotupa idhini

kwamba mmeidhinisha Muswada huu tutahakikisha kwamba tunampelekea Mheshimiwa Rais kwa hatua zake na mimi kwa yale yanayonihusu kama Waziri wa Fedha, nitahakikisha kwamba Kanuni zinatungwa na kanuni nyingi zimeshatungwa, kilichobakia tu ni kwamba Muswada ukipitishwa ikawa sheria sasa ndiyo nitaweza kutunga Kanuni na kuhakikisha kwamba zinafanyika mapema iwezekanavyo. Lakini nia ya Serikali ni kwamba Muswada huu uanze kutumika kuanzia tarehe 1 Julai, 2008. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wengi walizungumzia lakini hasa Mheshimiwa Dr. Willbrod P. Slaa alizungumzia kutaka kujua kwamba tunazungumzia *qualifications* lakini vizuri ieleweke kwamba unapozungumzia sifa ni sifa gani. Namhakikishia kwamba hizi zitajitokeza katika Kanuni. Kwa hiyo, hili litashughulikiwa na litajitokeza kwa kirefu kabisa katika Kanuni kwamba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anatakiwa awe na ujuzi gani, anatakiwa awe amesoma nini, amefanya kazi miaka mingapi na siyo hilo tu bali pia hata tabia yake kwa sababu kama ni mtu ambaye itabiti akague watu wengine, basi na yeye mwenyewe itabidi tumfanyie *vetting* kuhakikisha kwamba ni mtu ambaye kijamii anakubalika.

Kwa hiyo, licha ya *qualifications* za kusoma, viko pia vigezo vingine ambavyo pia vitaonyeshwa katika Kanuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo lilizungumzwa sana ni kwamba kwa nini Mkaguzi Mkuu na Mdhibiti Mkuu wa Serikali ashughulikie Mashirika au Kampuni ambako Serikali ina hisa zaidi ya 50.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria hii ni lazima ioane na Sheria nyingine. *Public Cooperation Act* inatamka ni lini kampuni au shirika linakuwa na *Public Cooperation* na *definition* mojawapo ni *over 50%*. Kwa hiyo, Kampuni yoyote ambayo tuna *shares* chini ya *50% is not public* na kwa hiyo wenzetu wale wenye zaidi ya 40% ndiyo wanaokuwa na uwezo wa kufanya mambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme kwamba hoja zilizojitokeza kwa kweli ni za msingi na tutalitazama kwa sababu chini ya 50% yapo Makampuni ambayo tuna 45% na ni Makampuni makubwa. Sasa je, kwa sababu ni 45% *CAG* asiende kulikagua shirika hilo? Nadhani hayo tutayatazama na kuona ni jinsi gani tunaweza tukaboresha Sheria hii. Lakini kwa sasa tunasema kwamba ni hiyo 50% mpaka tutakapofanya utafiti mzuri na kuona nini kifanyike.

Mheshimiwa Naibu Spika, mengi yamezungumzwa na Naibu Waziri na mengine ambayo pengine yatabaki tutayazungumza wakati tukipitia ile *schedule.*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)*

## KAMATI YA BUNGE ZIMA

### Muswada wa Sheria kwa ajili ya Ukaguzi wa Hesabu za Umma

Kifungu cha 1.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu hicho cha kwanza ukurasa wa nane sehemu ya *interpretation* ile ya pili kutoka mwisho palipoandikwa *Public Moneys* ina *"ies"*. Kwa hiyo, kuna sehemu nyingi nimeziona kuna zimeandikwa hivyo, kwa hiyo tukubaliane kwamba pote palipoandikwa kwa wingi, basi ile *"y"* inaondoka halafu inawekwa *"ies"* yaani *"Monies"*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge tuko katika Kifungu cha Kwanza, umesema ni ukurasa wa nane au wa sita? Kifungu cha kwanza ni mstari mmoja tu. Tumeelewana?

Kifungu cha 2.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 3

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema ni kwamba nimeona katika maeneo mengi ile *"money* ambayo inaandikwa kwa wingi imeandikwa *" ys"* sasa pote ambapo umetumia hiyo kuna sehemu kama tatu hivi, basi tukubaliane kwamba iandikwe *"monies"*.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu jilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 4

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya *Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 5

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 6

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya*

*Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 7

Kifungu cha 8

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 9

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 9 Kifungu kidogo (a)(vi) ule mstari unaofuata ni kurekebisha tu. "*Consolidated fund*", ile *"F"* iwe kubwa. Halafu pale inafuata ile *"monies"* izingatiwe kama nilivyoshauri.

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI :** Mheshimiwa Mwenyekiti, Sawa!

**MWENYEKITI:** Unakubaliana?

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Ndiyo!

**MHE. ATHUMANI S. JANGUO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokuwa nachangia nilitoa masahihisho katika kifungu hiki kuhusiana na kifungu cha 9(b) na (c) kubadilisha mpangilio ama unaziondoa zile inabaki kuwa zote chini ya (a) au sivyo unaongeza maneno mengine kwenye (b) na (c) ili yasomeke vizuri.

**MWENYEKITI:** Itasomekaje?

**MHE. ATHUMANI S. JANGUO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama zinabaki kama (b) na (b) ukifika (b) pale unasema: "*Examining inquiring into Auditing and Reporting on the Accounts have."* Katika (c) unarudia maneno hayo hayo au sivyo, lile neno "*conduct"* inakuwa *conducting* halafu itakuwa ina maana ya kwamba ina *support* ile *into* ya kule juu ya namba tisa.

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kukipitia kifungu hicho tumebaini kwamba kulikuwa na *typing problem*. Hicho kifungu (b) kilipaswa kiwe (vii) na hicho (c) kilipaswa kiwe (b). Sijui kama nimeeleweka?

**MWENYEKITI:** Bado!

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Hicho Kifungu (b) kilipaswa kiwe (vii) kwa mtiririko huo kiko chini ya (a) na hicho Kifungu (c) ndiyo kitakuwa (b). Baada ya kupitia na kuona marekebisho hayo!

**MHE. ATHUMANI S. JANGUO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na pendekezo la kifungu, lakini kifungu (b) kama kinabaki, bado kinahitaji neno la "*Conduct"* libadilike kuwa "*Conducting"* kwa sababu naisoma kuanzia kule juu: "*The Controller and Auditor General shall be conducting."* Huwezi kusema "*shall be conduct."*

**MWENYEKITI:** Nadhani sawa!

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa!

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 10

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 11

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo mawili katika kifungu cha 11 katika Kifungu kidogo cha (3) na kifungu kidogo cha (7). Sasa kwa kuwa ili nisisimame mara mbili namaliza yote kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kifungu kidogo cha (3) kinazungumza juu ya utoaji wa *report* na wakati ninazungumza ndani ya Bunge hili kwenye mchango wangu nilitaka Waziri anihakikishie kwamba kilichotokea kinalindwa na kifungu hiki kisitokee tena na nilitaka kujua Waziri atoe maelezo kilitokeaje, kwamba taarifa ya mwaka 2007 imo ndani ya ya kitabu cha 2006.

Sasa ili niwe na uhakika kwamba kifungu kinatulinda, basi nilitegemea Waziri angefafanua ili nijue kwamba kifungu hiki kinalinda kile ambacho kilitokea kisitokee tena. Kwa hiyo, nilifikiri kwa ajili ya *record purpose* atatusaidia Waziri.

Lakini la pili, katika kifungu kidogo cha (7) kazi ya Kamati ya *PAC, LAAC* na *POC* inatamkwa hapa na katika kazi hii moja ni kwamba *Auditor General* anapotoa taarifa yake kifungu kinasema: "*In determining whether to carry out any such examination he shall take into account any proposals made by*…." Kwa hiyo, inataja *committee*.

Sasa kwa majibu anayotoa Mheshimiwa Prof. Jumanne Abdallah Maghembe - Waziri wa Elimu wakati akisaidia kufafanua, mimi imenipa wasiwasi kidogo kwamba mambo mawili yanaweza kuwa yametokea hapa.

La kwanza, iwapo mtu amewekeza na amewekeza fedha nyingi: Je, anaruhusiwa kukiuka maadili na kufanya anachotaka kwa sababu tu amewekeza hela nyingi au mtu amewekeza hela nyingi kwa hiyo alindwe, sasa na taratibu zetu? Kama misingi ni hiyo, Kamati zetu zitashindwa kufanya kazi. Kwa hiyo, nilitaka kupata ufafanuzi ili kifungu hiki kiweze kufanya kazi.

Lakini la pili, *dignity* ya nchi iko juu ya fedha, *whether* mtu amewekeza kiasi fulani haina maana ya kwamba *dignity* ya nchi sasa inauzwa kwa thamani ya fedha aliyoweka pale. Mimi nilifikiri Bunge linapofanya kazi yake inafanya kazi kwa mujibu wa Sheria na hata Kamati inapokwenda mahali inakwenda kwa taratibu.

Sasa je, kwa majibu yale Serikali inatuhakikishiaje kwamba kifungu hiki kitawezesha Kamati zetu kufanya kazi zake kwa mujibu wa Sheria ili na *CAG* anapofanya kazi yake achukue zile *proposals* na hizo *proposals* ni baada ya Kamati kutembelea maeneo? Katika hali hiyo, Serikali inatoaje kauli baada ya kauli ambayo kidogo ni tata ya Mheshimiwa Prof. Jumanne Abdallah Maghembe?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dr. Slaa nimeelewa *concern* zako katika vifungu vyote viwili. Ukianza na tatu, unachokisema wewe hapa ni kwamba kifungu hiki hakina dosari, tatizo ni kwamba ile taarifa uliyoisoma wewe ambayo uliitoa kama mfano katika suala hili itapatikana katika utaratibu mwingine. Tukiingia kuzungumzia taarifa ya *Controller and Auditor Genera*l ile iliyokosewa au sijui ilifanya nini katika kifungu hiki, hatutungi Sheria hii.

Hata hili la pili alilotoa Mheshimiwa Prof. Jumanne Abdallah Maghembe alilitoa kwa sababu kulikuwa na malalamiko kwamba Kamati yetu moja haikutendewa vizuri katika shughuli ile ndiyo maana nilikuwa nawaambia toka asubuhi kwamba haitajibiwa kama sehemu ya kutunga Sheria na kwa sababu tuna muda tena wa kuzungumza mambo mengine ambayo siyo lazima yafuate mtitiriko wa kutunga Sheria.

Nawaomba hili swali mrudie baadaye. Lakini kwa kusema tuanze kusema maneno aliyoyasema Mheshimiwa Prof. Jumanne Abdallah Maghembe yana-*fit* au haya-*fit,* tutakwenda mbali sana juu ya Sheria. Je, kifungu hiki ninyi mnaona kinatosha kwa kumweka *Controller and Auditor General* kufanya kazi? Hilo ndiyo swali.

Katika kifungu hicho cha 7 tulisema ile Kamati nyingine inaitwa *Parastatal Organisation Accounts Committee,* nadhani mliacha kusema hivyo.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni katika…..

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shellukindo niko bado na Mheshimiwa Dr. Willbrod P. Slaa!

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** *Okay*!

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hatupo mbali. Mimi nilichokuwa nataka kwenye kifungu hiki, kinasema: "…*Shall apply to every such report but nothing in this sub section shall be construed as preventing.*"

Mimi nilikuwa na *doubt* na hiyo ndiyo maana nilikuwa nataka anihakikishie hii *phrasing* hapa. Sasa huwezi kuipata *except* kwa kwenda kwenye ule mfano tulioutoa. Kwa hiyo, ninachotaka ni kwamba anihakikishie kwamba kifungu hiki kina-*cover* kile ambacho kilitokea, sasa hatikatokea. Kwa sababu ukishasema *nothing shall be construed as preventing*, tayari inakuwekea kwenye *doubt* kwamba anaweza kupeleka *report* kwa vyovyote vile.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha hayo ndiyo maswali yako.

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, analolitaka Mheshimiwa Dr. Willbrod P. Slaa litakuja. Kuna hoja maalum ilitolewa na Mheshimiwa Lucy T. Mayenga, tulipowasilisha hapa zile hesabu ikatolewa hoja kwamba hesabu hizo ziongozwe na Waheshimiwa Wabunge. Kwa hiyo, mimi ningependekeza kwamba kwa sababu kuna hoja maalum tungezungumza kule.

**MWENYEKITI:** Hapana! Nilichojibu mimi ndicho nilichosema. Sasa hapa anakuuliza suala *specific*. Hapa umeulizwa *specific* haya yaliyoandikwa na kwamba ile itakuja wakati huo na siyo hapa. Hapa labda akuulize tena.

Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, uliza tena.

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nilitaka Mheshimiwa Waziri anihakikishie kwamba unapoweka hiyo kitu kama *proviso but nothing in this sub section shall …*

**MWENYEKITI:** Katika Kifungu gani?

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha (3). Iko kwenye mstari wa nne toka chini. *"But nothing in this sub section shall be construed as preventing the Controller and Auditor General from submitting a report to the President of any audit matter relating to any public authority or other body."* Kwa hiyo, inaweza kupelekwa tu hata ikiwa katika hali fulani, mimi ndiyo nilikuwa na-*doubt* na hicho kifungu kwamba labda kinaweza kupelekwa tu badala ya kupita Bungeni. Ndiyo hofu yetu hiyo.

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri *spirit* ya Sheria nzima hii ni kwamba taarifa zitakazotoleWa na *Controller and Auditor General* zitapelekwa kwa Rais na katika kipindi cha siku saba Rais atamteua mtu wa kupeleka taarifa hizo Bungeni. Hii nadhani ndiyo *spirit* ya Sheria nzima hii na ndiyo Katiba ilivyo na ndivyo ilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama kulitokea matatizo yale yaliyotokea ya *typing* kwa mwaka na kadhalika yale tutayasahihisha katika namna nyingine, lakini kwa sheria hii, haya yaliyopo hapa ndiyo yatakayotekelezwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa nadhani tumeelewana! Mheshimiwa hilo suala alitoa mfano, kwa nini unarudia kutunga Sheria? Halipo humu.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu nilikuwa nimegusia maeneo matatu ya kifungu hiki cha 11.

La kwanza ilikuwa ni 11(1)(a) pale ambapo imeandikwa *seek the professional opinion or advice of the Attorney General* nilikuwa nimesema kwamba katika *interpretation hakuna interpretation ya Attorney General*, kwa hiyo, ni vizuri ikawekwa kama ilivyowekwa *interpretation ya Controller and Auditor General* na tungechukua ile ya Katiba na ningesaidia hapa kusema *Attorney General the Officer referred to in Article 59 of the Constitution.*

La pili, ….

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa tukubaliane kwanza hilo. Nadhani halina madhara. Endelea la pili.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni kifungu hicho hicho 11(4) katika ukurasa wa 12 pale palipoandikwa: "…*in every case where the Controller and Auditor General makes a report under this section he shall notify the Treasury*." Mimi nikasema uhusiano wake *Treasury* ni *Pay Master General*, ni vizuri tukawa *specific* maana *Treasury* ni ile Wizara yote nzima, pale kifupi chake. Kwa hiyo, tungeweka *Pay Master General* ambaye ndiye anahusika na ule uhusiano wa hizo taarifa.

Halafu nikiendelea na …..

**MWENYEKITI:** Katika *paragraph* hiyo hiyo?

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo nimemaliza.

**MWENYEKITI:** Basi tunakubaliana kwanza. Tuna tatizo? Hamku-*note* wakati ule? Kwa hiyo, hiyo pia tunaikubali kama ilivyo *Pay Master General* badala ya *Treasury*. Tunaendelea Mheshimiwa Shellukindo!

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna moja vile vile ulinisaidia kuliendeleza muda mfupi uliopita kifungu kidogo cha (7) cha kifungu hicho cha 11 ukurasa wa 13 pale palipoorodheshwa Kamati hizo za *over sight* ile

iliyoandikwa *Parastatal Organisation Committee* ambayo uliweza kuikumbusha kwamba iwe ni *Parastatal Organisations Accounts Committee.*

**MWENYEKITI:** Hilo ndilo jina la Kamati hii inayoitwa *Parastatal Organisations Accounts Committee* Mheshimiwa Shellukindo.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

**MWENYEKITI:** Samahani Mheshimiwa Salim sikukuona. Tuko kifungu cha 11.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Msemaji wa Kambi ya Upinzani anawasilisha maoni ya Kambi alitaka ufafanuzi wa baadhi ya maneno katika kifungu cha 11(2)(d) kinachosema: "*Policy of the highest thrift*", lakini katika maelezo ya Mheshimiwa Waziri sikuona ufafanuzi huo. Kwa hiyo, napenda nipate ufafanuzi wa maneno haya yaliyotumika.

**MWENYEKITI:** Kifungu gani? Rudia tena.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Kifungu cha 11(2)(d).

**MWENYEKITI:** Kinasema nini?

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Kinasema: "*Any failure of the observed policy of the highest thrift has occurred; or…*", yale maneno yanayosema: "*…policy of the highest thrift…*" katika maelezo ya hotuba yetu tuliomba ufafanuzi juu ya maneno hayo yaliyotumika.

**MWENYEKITI:** Lazima uanzie kule mwanzo: "*Where at any time it appears to the controller and Auditor General that: (d) Any failure to observe a policy of the highest thrift has occurred; or*" ni *conditions* zile. Enhe, Waziri.

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *thrift* ni uaminifu. Kwa sababu ni neno la kisheria, ningeomba labda Mwanasheria Mkuu aweze kunisaidia kulieleza vizuri zaidi lakini ninachojua mimi ni uaminifu kama huna uaminifu.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ameshalielezea, hili ni neno la Kiingereza tu.

**MWENYEKITI:** Tueleze kidogo.

**MWENYEKITI:** Tueleze kidogo.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Ni neno la Kiingereza ambalo linamaanisha kama alivyosema Mheshimiwa Waziri. Hili neno ukienda kwenye *dictionary* yoyote unapata kwamba ni *policy* ya uaminifu.

**MWENYEKITI:** Tunabishania hii hii!

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sina hakika kama neno *policy* pale lipo sahihi, nilidhani ingelikuwa *principle of the highest thrift* kuliko *policy* kwa sababu hapa kinachozungumzwa ni *principle* siyo *policy*.

**MWENYEKITI:** *Actually* ukisema *policy* halafu ukasema uaminifu, *policy* haiwezi kuingiza kwenye uaminifu, *principle* ndiyo. Kwa hiyo, hapa iwe *principle*. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 12

Kifungu cha 13

Kifungu cha 14

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 15

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 15(3) kina marekebisho, kwanza niwashukuru wameweka ile dhana tuliyopendekeza, nawashukuru sana kwa hilo. Tatizo langu hapa limekuwa la lugha.

Nafikiri lugha inaweza kurekebishwa lakini kwa kuwa tunatunga sheria, ni vizuri tukasema nini kinapaswa kuwepo. Nafikiri ilitakiwa isomeke:

"*Shall submit copies of quarterly internal audit report he issues before the…*", tena wameandika *beging* badala ya *beginning*, hii naiona sasa hivi, lakini tunawasamehe kwa sababu hii wameifanya mchana huu, lakini nadhani kunahitajika kazi pale.

**MWENYEKITI:** Dr. Slaa hebu ukae chini Naibu Waziri aseme marekebisho hayo kwa sababu alishafanya.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, hicho kifungu tumekiona kidogo kulikuwa kuna utata kidogo lakini tumekirekebisha kama hivi nitakavyoisoma: "*The Internal Auditor of any audit which is subject to be audited by the Controller and Auditor General shall*

*submit copies of internal audit quarterly report before the beginning of the next quarter to the Controller and Auditor General*".

**MWENYEKITI:** Inabidi urudie kwa sababu hatujaandika mahali.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kurudia.

**MWENYEKITI:** Ndiyo.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** "*The Internal Auditor of any audit which is subject to be audited by the Controller and Auditor General shall submit copies of Internal Audit quarterly report before the beginning of the next quarter to the Controller and Auditor General*".

**MWENYEKITI:** Nadhani yalikuwa ni marekebisho juu ya *schedule of amendments*.

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 16
Kifungu cha 17
Kifungu cha 18
Kifungu cha 19

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 20
Kifungu cha 21
Kifungu cha 22
Kifungu cha 23
Kifungu cha 24
Kifungu cha 25
Kifungu cha 26
Kifungu cha 27

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 28

**MHE. WILLIAM F. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 28(b) mstari wa pili unaosema: "*Officers, Head of Departments and Chief Executives*

*Officers….".* Hapa kuna *option* katika hiyo *Chief Executives Officers,* unaweza kuishia *Chief Executives au Chief Executive Officers,* haziwezi kutumika zote mbili hivyo hivyo.

**MWENYEKITI:** Nawe ondoa moja unayotaka. *Chief Executive Officers* nadhani.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 29

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiko yoyote)*

Kifungu cha 30

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 31

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 32
Kifungu cha 33
Kifungu cha 34

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 35

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 36

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 37

**MHE. WILLIAM F. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 37(3), ile sentensi ya mwisho: "*Minister to the National Assembly,*" *pale Assembly* wangeweka *'m'*, nadhani imeandikwa "*Assebly.*"

**MWENYEKITI:** Kuna *typing error*. Mheshimiwa Janguo nimekuona.

**MHE. ATHUMAN S. M. JANGUO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokuwa nachangia nilieleza kwamba yaliyokuwemo katika kifungu cha 37(2) na kifungu cha 38 ni yale yale yamerejewa, katika marekebisho *in fact* hali inakuwa ngumu zaidi urejeo wenyewe, nitasoma marekebisho na kwenye marekebisho…

**MWENYEKITI:** Kwanza nisaidie, sisi huku tumefuta kifungu cha 38.

**MHE. ATHUMAN S. M. JANGUO:** Aah, basi nashukuru, ahsante sana.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 38

**MHE. WILLIAM F. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu nilikuwa nimezungumzia hapo kwamba tuna zile *oversight committees* tatu, *Public Accounts Committee, Local Authorities Accounts Committee, Parastatal Organizations Accounts Committee,* sasa hapa inaelezwa kwamba baada ya *Controller and Auditor General* kuleta taarifa hizo na baada ya kuwa-*tabled on the National Assembly* basi zinaweza kuzungumzwa na Kamati hizo tatu halafu na *other Parliamentary Sectoral Committees,* hapa ndiyo nilikuwa na wasiwasi wana maana ya *Sectoral Committees* zipi? Kwa sababu kila *Committee* ina majukumu yake imegawiwa ya kuyashughulikia kwa mujibu wa kanuni za Bunge.

Sasa hii ya kuingiza tena hapa inaingilia tena kazi ya hizo Kamati, hapa nadhani labda wanazungumza Mbunge mmoja mmoja sasa anaweza kuchangia hizo. Nilitaka ufafanuzi kwenye hilo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri ilikuwa na maana gani? Lakini mmeelewa swali lake?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeelewa. Hapa tulichokusudia ni kwamba tumeongeza majukumu ya *Controller and Auditor General* na moja ambalo atakalolifanya ni *performance audit*. tumesema kama sekta husika kwa mfano amekwenda kufanya *performance audit* katika sekta ya afya au elimu, wamesema kwamba wanataka kuona, basi kwa hiyo tumetoa nafasi hiyo vile vile waweze kui-*discuss* ripoti hiyo ya *Auditor and Controller General*.

**MHE. WILLIAM F. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani kuiweka hapa kwenye sheria tuta-*demand* sisi kwamba tutazungumza hizo maana yake imewekwa kisheria. Kwa hiyo, ikitolewa Kamati labda ya Shirika fulani ambalo lipo

katika sekta ninayosimamia, basi hakuna kizuizi, mimi nitaishughulikia hiyo maana imewekwa kisheria. Nadhani tungekuwa wazi kama kuna hizi *special or performance audit report,* basi iwe *specific* lakini tusizungumze tu kama *reports of Controller and Auditor General* kwa ujumla, italeta mchanganyiko hasa ikiwekwa katika sheria kama hivi.

**MWENYEKITI:** Wewe ulifikiri maneno gani yangeingia badala yake.

**MHE. WILLIAM F. SHELLUKINDO:** Kama nia ndiyo hiyo ya kuweza kuongeza ufanisi zaidi, basi kungekuwa na kifungu kingine kinachoeleza kwamba: "*In the case of a performance audit reports can be discussed or may be discussed by Parliamentary Sectoral Committees".* Tusije tukaingilia yaani *Sectoral Committees* zikafanya *duplication* na zile Kamati, tungekuwa *specific* katika hili.

**MWENYEKITI:** Nadhani kuna maneno: "*as the case may be…*" nadhani yana-*cover* wasiwasi wako.

**MHE. WILLIAM F. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama wote tunakubaliana hivyo sina tatizo. Hoja yangu ni kwamba kusije kukawa na Kamati kuchukua ripoti ya sekta yake, *audited report* wakaishughulikia tukasema *as the case may be*.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Shellukindo kwamba kifungu hicho kingeondolewa kabisa, kwa sababu *Parastatal* zote ambazo unaweza kusema ndiyo zinatokana na sekta sasa zina Kamati inayoshughulikia mahesabu.

Pili, ripoti ikishakamilika ikaja Bungeni itajadiliwa na Wabunge wote. Kwa hiyo, naona hapa tunataka kuongeza urasimu usio wa lazima.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pia nataka kuongezea kwamba katika utaratibu wa kawaida *Public Accounts Committee* haitashughulikia tu mambo ya hesabu peke yake, *you know financial statement or financial audit*, ulimwengu wa sasa una-*move completely* zaidi kwenda kwenye *value for money audit* na ndiyo inavyofanyika ulimwenguni kote. Kwa hiyo, *is true* kwamba jambo hili likiwekwa kama lilivyowekwa litaleta *confusion* kubwa zaidi kama likiwa katika sheria.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, mapendekezo yako?

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Nakubaliana na Mheshimiwa Mzindakaya hii *area* ingekuwa *deleted*.

**MWENYEKITI:** Wizara ya Fedha mnasema nini?

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** *(Hapa hakutumia microphone).*

**MWENYEKITI:** Tumia chombo Mheshimiwa Waziri hapa tunatunga sheria, hatukukusikia.

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukubaliana kwamba italeta *duplication*, kwa hiyo, tuna-*delete*.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, tunacho-*delete* ni nini?

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Inaanza "*and*" mpaka "*may be*".
**MWENYEKITI:** Tuna-*delete* maneno yanayofuata "*and any other Parliamentary Sectoral Committees as the case may be.*"

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 39

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 40

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya *numbering* inawezekana nimechanganya kifungu kipya lakini ….

**MWENYEKITI:** Sema ya zamani halafu tukupe namba.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mimi niko kwenye kifungu cha zamani cha 43?

**MWENYEKITI:** Bado kidogo.

**MHE. WILBROD P. SLAA:** Bado hatujafika?

**MWENYEKITI:** Ndiyo.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 41

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyaa vipi? Umechelewa kusimama?

**MHE. MOHAMMED JUMA HABIB MNYAA:** Hapana sijachelewa Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Hiki ni kifungu cha 42 cha zamani.

**MHE. MOHAMMED JUMA HABIB MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo hapo nina matatizo.

**MWENYEKITI:** Sawa.

**MHE. MOHAMMED JUMA HABIB MNYAA:** Katika kifungu hiki sina matatizo na (a), (b), (d), (e) kuhusu *funds and resources za National Audit*, lakini matatizo yangu yamekuja katika kifungu cha (c) hii *income from the investment*, bado nina wasiwasi nayo na hatujapata maelezo kama Kambi ya Upinzani ilivyotaka, hawa *National Audit* wana-*invest* wapi? Au *income from investment* imetoka wapi? Naomba maelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nitoe tu mfano wa haraka haraka ili Mheshimiwa Mbunge aweze kufahamu. Kifungu hiki kwa mfano *Audit General* watakuwa na jengo lao na inawezekana kwamba jengo hilo wasiweze kulitumia lote na wakakodisha baadhi ya maeneo ya nafasi walizonazo katika jengo hilo. Kwa hiyo, ile *income* itakayopatikana ndiyo itabidi iende katika hesabu zao na ndiyo ita-*cover* hiki kifungu, vinginevyo bila kuwa na kifungu hiki ile *income* itakayopatikana huwezi kuiweka katika sheria hii.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 42

**MHE. DR. WILBROAD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niombe radhi kwamba hiki ninachokisema nimekigundua sasa hivi, naomba wataalam wetu, Mheshimiwa Waziri na wataalam wake labda wanisaidie. Katika kifungu hiki kuna maneno ambayo yananistua, kinasomeka: "*The Pay Master General shall appoint the Accounting Officer of the National Audit Office who shall control and be accountable for the expenditure of money…*" na hiki kinaendelea mpaka kwenye kifungu cha 48 ambapo pia kinasema: *"The Accounting Officer of the National Audit Office shall within a period of three month…*"

Sasa kama ninakumbuka *spirit* ya Sheria hii ni kuwa na *CAG* ambaye ana nguvu na kwamba ndani ya Sheria hii tuna *CAG* ambaye hana mtu mwingine juu yake, haiku-*clear* huyu anayeteuliwa na *Pay Master General* kuwa *Accounting Officer* anatoka wapi? Je, anatoka nje ya wale *staff* ambao kwa kawaida wapo chini ya *CAG?* Na akija: Je, anasimamiaje yale mafungu ambayo *CAG* anayahitaji kuyafanyia kazi na kwa *experience* ya huko nyuma kwenye mashirika mengi yule Mkurugenzi au kwa jina lolote tunalomwita yeye ndiye *Accounting Officer* wa fedha zinazokuwa *appropriated* na Bunge?

Sasa hapa nimestuka kidogo, labda ningeomba nisaidiwe kama ni sahihi na ndiyo ilitegemewa hivyo au imeingia kwa bahati mbaya?

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni sahihi na kufuatana na Sheria ya *Exchequer* kwamba popote ambapo pesa zilizokuwa *appropriated* na Bunge zinatumika, *Pay Master General* huteua *Accounting Officer*.

Kwa mfano pale Hazina *Pay Master General* ni *Accounting Officer* wa Taifa zima lakini Wizara ya Fedha tuna *Accounting Officer* ambaye ni *Deputy Pay Master Secretary*. Sasa kwa *Controller and Auditor General* yeye kama *Chief Executive Officer* hatakiwi kuwa Mhasibu Mkuu wa *National Audit Officer*. Kwa hiyo, Mhasibu Mkuu wake ndiye ambaye atateuliwa na *Pay Master General* kuwa *Accounting Officer*.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 43

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 44

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 45

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 46

**MHE. WILLIAM F. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu nilihoji *Public Accounts Committee* kupewa kazi ya kum-*appoint Auditor*. Nilikuwa nimesema Bunge lisiingie kwenye ajira hizo. Kazi hii angeifanya *Pay Master General* ambaye anamteua *Accounting Officers*, itakuwa ni vizuri zaidi.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili tulilizungumza na tulilijadili kwa kina, tumesema kwamba Sheria ile ya *Public Finance Act* ilikuwa inampa uwezo Waziri, sasa kusema *Pay Master General* apewe uwezo yeye kumteua *Auditor* kwa ajili ya *CAG*, tutakuwa tunarudi kule kule!

Tumesema kwamba, kwa maana hiyo tutoe uwezo kwa Kamati ya *PAC* wao ndio wamteue huyu *Auditor* kwa ajili ya kuki-*audit* hiki chombo, isiwe tunarudi kule ambapo Waziri ndiye anayemteulia halafu sasa hivi tumwambie *Pay Master General* amteulie. Hili ndilo wazo tulilokuwa nalo.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 47

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu kipya cha 47…

**MWENYEKITI:** Ambacho ni kifungu cha 48 cha zamani.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Eee, kifungu cha 48 cha zamani ambacho ni kifungu kipya cha 47, kifungu kidogo kile cha (e) ile sentensi ya mwisho inayosema: "*Required to do so by court'*. Nadhani pale ingekuwa:

"*By a court of law.*" Nadhani *Attorney General* atakubaliana nami hapa, hatuwezi kuiachia *court* tu, *court can be anything*.

**MWENYEKITI:** *Attorney General* ndiyo umetajwa unasema nini? Naona wanaafiki. Mheshimiwa Janguo.

**MHE. ATHUMANI S.M. JANGUO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sina uhakika kama pendekezo nililotoa katika kifungu cha 47, yaani 48 ya zamani, kifungu kidogo cha (4) kimefanyiwa marekebisho, kama hakijafanyiwa nilisema kwamba adhabu ya faini ya Shilingi milioni moja ilikuwa imewekwa sawasawa na miaka miwili ya kifungo.

Sasa kwa kuwa imerekebishwa kufanywa miaka mitano, haiyumkiniki kwamba uzito wa Shilingi milioni tano uwe sawasawa na kifungo kile cha miaka miwili. Nikashauri kama Waziri atapandisha hiyo miaka ikawa minne au mitano ingekuwa inakwenda sawasawa na badiliko la kwenye fedha.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nilipokuwa natoa maelezo, nimesema kwamba sheria inasema awali ilikuwa inasema Shilingi milioni moja au miaka miwili. Lakini tukaona hiyo Shilingi milioni moja ni ndogo na tukapandisha kuwa Shilingi milioni tano, ila hatukuona sababu ya kupandisha miaka kwa sababu *nature* ya Mtanzania hata siku moja ukimwambia unamfunga kwake yeye anaona ni dhiki kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti ,kwa hiyo, hatukuona sababu ya kupandisha miaka, tumeona tupandishe hicho kiwango cha fedha lakini miaka ibaki pale pale. Lakini tusisahau hii sheria inasema kwamba Jaji anaweza kumhukumu vyote. Kwa hiyo, tuliona hiyo miaka miwili tuiache hivyo hivyo. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 48

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu nilikuwa nimezungumza kwamba ili mambo yaende sawasawa au kuwa *consistency* katika kifungu hiki kipya cha 48(3)(b) pale panasema:

"*The taking of an oath is contrary to his religious beliefs….*", nilisema kuna sehemu nyingine ametumia *his/her, she/he*, sasa ni vizuri tungekubaliana kama tunakubali kwamba tukisema *his*, basi inaunganisha na *her*, basi itumike hiyo kwa sababu tumechanganya katika hizo nilizozisema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nilitaka kulisisitiza hapa hii "*moneys*" imetumika sana, kwa hiyo, tutumie ile *monies* ambayo ni *plural* sahihi.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mbaya kwamba mimi sio Mwanasheria, lakini kisheria unapoweka *his,* inakuwa na *implications* ndani kwamba hata kama aliyekosa ni *her* ina-*imply* lakini nitamwachia Mwanasheria atusaidie kwa hili.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Sheria inaitwa *Interpretation of Laws* ambayo ni Sura ya Kwanza ya Sheria za nchi, inaelezea juu ya jambo hili, kwenye kifungu cha nane inasema kwamba:

"*In any written law words importing the masculine gender includes the feminine, words importing the feminine gender includes the masculine*." Kwa hiyo, hili tatizo aliloeleza linazungumzika, kuna sheria inalizungumzia kabisa kwamba kama ni *he* ina-*include she*, kama ni *she* ina-*include he*.

**MWENYEKITI:** Sawa. Mheshimiwa Shellukindo.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni kwamba kama tunakubaliana iwe moja, basi tuwe *consistency* kama ni *his* basi iwe *his* lakini humu umetumia *his* halafu *he/she* katika Muswada huu, ndiyo hoja yangu.

**MWENYEKITI:** *Conscious* yao kwamba wanaonea watu, inawasuta, ndiyo maana wanababaika cha kuandika. Kwa hiyo, tunakubali hivyo lakini tu-*keep consistency*.

**MHE. BASIL P. MRAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hicho hicho cha 48(3)(b) kinazungumzia: "*In the form state out in the schedule*, ukienda ukurasa wa

28, utaona hiyo *schedule* ipo pale mwisho, *schedule* hiyo inaishia tena kwa kusema: "*so help me God*." Mtu huyu anaamini dini na kutatokea mtu ambaye haamini dini wala Mungu halafu tunamwambia hapa aseme *so help me God*, haiwezekani ni *contradiction.* Kwa hiyo, tufute hiyo *"so help me God."* Sijui kama nimeeleweka?

**MWENYEKITI:** Umeeleweka, lakini viapo vyote vinasema hivyo.

**MHE. BASIL P. MRAMBA:** Aah, kwenye hii kwa sababu hapa ni *provision* kwa mtu ambaye haamini dini, hana dini.

**MWENYEKITI:** Kuna 3(a) na (b): "*Has no religious belief or taking of oath*…." Tusaidie Mwanasheria Mkuu.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nimemwelewa vizuri Mheshimiwa Mramba, nafikiri kama mtu hamwamini Mungu hatasema hilo neno.

**MWENYEKITI:** Lakini viapo vyetu vyote vipo hivyo ndiyo, maana wameli-*bold* hapo kwenye *schedule so that* asiyetaka kusema asiseme.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 49
Kifungu cha 50

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 51

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Jedwali

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imepitia Muswada wa Sheria ya Ukaguzi wa Hesabu za Umma *(Public Audit Act, 2008)* kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yake. Kwa hiyo, naomba kutoa hoja kwamba taarifa hiyo sasa ikubaliwe rasmi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kupitishwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu)*

**NAIBU SPIKA:** Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, Muswada huu unasubiri *assent* ya Rais na kwa sababu unatakiwa sana na Rais amesema unaanza kutumika tarehe 01 Julai, 2008 tunamtakia kheri.

Waheshimiwa Wabunge shughuli tulizopanga leo kuhusu Miswada zimekwisha. Kesho ni siku ya Alhamisi, kufuatana na kanuni zetu tungekuwa na maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, lakini kwa sababu ni siku maalum ya Bajeti lakini asubuhi inatanguliwa na taarifa ya Mipango, kwa hiyo, kesho hatutakuwa na maswali ya papo kwa hapo kwa Waziri Mkuu. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge nguvu zetu zote ziingie katika kufikiria mpango wa nchi na kipindi cha bajeti. Maswali hayo kwa Waziri Mkuu yatakuwepo wiki ijayo. Waheshimiwa Wabunge wa *SADC* tutakutana sasa hivi katika Ofisi ya Naibu Spika.

Baada ya kusema hayo, naahirisha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 12:40 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Alhamisi, Tarehe 12 Juni, 2008, Saa Tatu Asubuhi)*